

YESU KATIKA INDIA

*Ikiwa ni taarifa ya kuepukana kwake
Yesu na kifo juu ya msalaba na safari
yake ya kwenda India*

Kimetungwa na:

**HADHRAT MIRZA GHULAM AHMAD
WA QADIAN**

Mwanzilishi wa Jumuiya ya Ahmadiyya katika Islam

Kimetafsiriwa kutoka Kiingereza na Bwana Mohammed
Saidi Kibindu wa Dar es Salaam

Tafsiri ya Kiswahili imetangazwa na:

JUMUIYA YA WAISLAMU WAAHMADIYYA TANZANIA
S.L.P. 376
SIMU: 2110473 FAX: 2121744
DAR ES SALAAM.

YESU KATIKA INDIA

Mwandishi: Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s.

Mfasiri: Bwana Muhammed Said Kibindu

© Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania

Chapa ya kwanza: 2000
Nakala: 3000

Kimechapwa na
Ahmadiyya Printing Press
P.O. Box 376
Simu: 2110473, Fax 2121744
Dar us Salaam
Tanzania.

YALIYOMO

1.	Neno la Mbele	4
2.	Utangulizi	7
3.	Sura ya Kwanza	21
4.	Sura ya Pili	56
5.	Sura ya Tatu	62
6.	Sura ya Nne	72
I.	Sehemu ya Kwanza	72
II.	Sehemu ya Pili	78
III.	Sehemu ya Tatu	98
7.	Viambatanisho	112

NENO LA MBELE

"YESU NCHINI INDIA" ni tafsiri ya KISWAHILI ya "Masihi Hindustan Mein" ambacho ni kitabu cha Kiurdu kilichoandikwa na Mwanzilishi Mtukufu wa Jumuiya ya Ahmadiyya katika Islam, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. (1835-1908).

Mada kubwa iliyofafanuliwa katika kitabu hiki ni kuepushwa kwake na kifo cha fedheha juu ya msalaba na safari yake ya kwenda India kuyatafuta makabila yaliyopotea ya wana wa Israeli ambao ilikuwa lazima awakusanye na kuwaingiza katika zizi lake kama ilivyotajwa katika Agano Jipya.

Ushahidi chungu nzima umekwisha patikana katika Maandiko ya Kikristo na pia ya Kiislamu, vitabu vya zamani vya tiba na pia vya historia, ikiwa ni pamoja na kumbukumbu za kale za Kibuddha katika kulifafanua jambo hili.

Akiwa ameianza safari yake kutoka Yerusalem na akiwa amepitia Nasibus, na Iran, Yesu anaonyeshwa kuwa alifika Afghanistan ambako alikutana na Wayahudi waliokaa pale baada ya kutolewa utumwani kwa Nebachadnezzar.

Kutoka Afghanistan Yesu alikwenda Kashmir ambako pia baadhi ya makabila ya Waisraeli yalikaa. Alipofanya mahali hapa kuwa maskani yake na ndipo mahali alipofia. Kaburi lake limetafutwa na kukutwa katika mtaa wa Khanyar, mjini Srinagar.

Kwenye sehemu inayoshughulika na ushahidi uliopatikana katika kumbukumbu za kale za Kibuddha Hadhrat Ahmad ametatua swalio ambalo kutohana na hali yake ya ugumu limekuwa kwa muda mrefu likiwatatiza waandishi wengi wa Kimaghari.

Waandishi hawa wamefumbwa na kufanana kwa ajabu kunakopatikana baina ya mafundhisho ya Kibuddha na yale ya Kikristo na kati ya matukio ya maisha ya wote wawili Yesu na Buddha kama ilivyofunuliwa katika maandiko ya kila mmoja wao.

Baadhi ya waandishi hawa wanashikilia maoni kwamba kwa vyo vyote vile mafundisho ya Kibudha ni lazima yawe yalifika

Falastwini na kutumiwa na Yesu katika mahubiri yake. Lakini hakuna kabisa uthibitisho wa kihistoria wa kuunga mkono nadharia hii.

Msafiri wa Kirusi aitwae Nicolas Notovitch aliishi kwa kipindi kirefu na Walama wa Tibet na wakamtafsiria vitabu vyao vitakatifu. Yeye ana maoni kwamba Yesu lazima alikuja Tibet kabla ya kusulubiwa kwake na kurudi Falastwini baada ya kujifunza mafundisho ya Kibuddha. Haya pia ni matamshi tu ambayo hayaungwi mkono na ushahidi wa kihistoria wenye kuaminika.

Akiyakanusha maoni hayo ya namna mbili, Hadhrat Ahmad anaandika kwamba Yesu alikuja India siyo kabla ya tukio la Msalaba bali baada yake na kwamba si yeye aliyekopa mafundisho ya Kibuddha bali ni wafuasi wa Buddha wanaoonekana kuwa wameichapisha upya picha ya Injili zote katika vitabu vyao.

Kulingana na Hadhrat Ahmad, Yesu pia alitembelea Tibet wakati wa safari zake nchini India akiyatufuta makabila yaliyopotea ya Israeli. Alihubiri ujumbe wake kwa watawa wa Kibuddha ambaa baadhi yao walikuwa Wayahudi waliojiunga na dini hiyo ya Kibuddha. Wafuasi wa Buddha waliathirika sana na mafundisho yake na wakamchukulia yeye kuwa ni udhihirisho wa Buddha na mwali muhimu wao Aliyahidiwa. Wakiwa wanamwamini kama Bwana wao, wakayachanganya mafundisho yake na yale yaliyomo katika kumbukumbu zao na wakayahesabu yote kwa pamoja ni ya Buddha. Ushahidi wa kutosha wa kuunga mkono maoni haya unapatikana katika kumbukumbu za kale za Kibuddha.

'Masih Hindustan mein' kiliandikwa mnamo mwaka 1899 na ni kiishilizio cha zama ambamo kwa karne nyingi Waislamu na Wakristo waliamini Yesu kupaa mbinguni. Kikiwa ni kitabu cha kwanza pekee kilichoandikwa kuhusu suala hili kwa mji wa kiakili, kitabu hiki kilileta kishindo kikubwa.

Hoja zake zilitangazwa na katika nusu karne iliyopita kimepata mafanikio ya kutosha katika kumwondolea Yesu sifa za uwongo za kiungu na kumwonyesha hadharani mbele ya ulimwengu akiwa nabii mtakatifu ambavyo kwa hakika ndivyo alivyokuwa.

Katika nyanja za Kiislamu kishindo cha kitabu hiki kilikuwa kikubwa sana kiasi kwamba Mufti wa Chuo Kikuu cha Al-Azhar jijini Cairo, alitoa *Fatwa* kwamba kulingana na Qur'an Tukufu Yesu alikufa kifo cha kawaida. Mvuto wake wa kuzishawishi fikra za Kikristo pia ulikuwa wa kusumbua sana.

Ingawa hakuna kitabu kingine mionganoni mwa maandiko yake chenye jina hili, hata hivyo Hadhrat Ahmad aliyajadili kikamilifu masuala yote haya pamoja na mengine mengi muhimu kuhusu ukweli wa Islam, ukweli wa madai yake na ukweli kuhusu kifo cha Yesu katika vitabu vingi tu alivyoviandika baada ya hicho kilichotajwa hapo juu.

Tafsiri ya Kiingereza ilifanywa na Qazi Abdul Hamid aliyekuwa mhariri wa jarida la kila juma liitwalo: "*The Sunrise*" la Lahore ambamo ilichapishwa kwa mfululizo katika kipindi cha miaka ya 1938 hadi 1939. Ilitangazwa kwa mara ya kwanza katika sura ya kitabu mnamo mwaka 1944 na Nashrul-Ishaat Sadr Anjuman Ahmadiyya, Qadian.

Pamoja na wengine wote waliotusaidia kwa njia moja au nyingine katika uchapishaji wa kitabu hiki, shukrani zetu nyingi zimwendee Bwana Mauloud Ahmad Khan, aliyekuwa Imam wa Msikiti wa London ambaye alijitolea sana kuzikusanya nukuu zinazohusika kutoka katika vitabu vya asili vilivyorejewa na Hadhrat Ahmad katika kulithibitisha jambo hili. Nukuu hizo zimeunganishwa na kitabu hiki kwa mpangilio wa viambatanisho namba 1 hadi namba 18.

Mei, 1962

*Wakilut - Tabshir
Tahrik Jadid,
Rabwah, Pakistan*

**KWA JINA LA MWEZI MUNGU, MWINGI WA REHEMA,
MWINGI WA UKARIMU. TUNAMHIMIDIA YEYE
NA TUNAMSALIA MTUME WAKE MTUKUFU S.A.W.**

*Ee Mola! Hukumu baina ya watu wetu kwa haki.
Hakika wewe U m`bora wa mahakimu.*

UTANGULIZI

Nimeandika kitabu hiki ili, kwa kuleta uthibitisho kutoka kwenye ukweli ambao umekwisha kubalika na kutoka kwenye ushuhuda wa kihistoria usiokuwa na shaka na wenye kuthaminiwa, na kutoka kwenye nyaraka za kale za wasiokuwa Waislamu, niweze kuondoa mawazo potofu sana ambayo yamezagaa mionganini mwa Waislamu na mionganini mwa takriban madhehebu zote za Kikristo kuhusu maisha ya mwanzoni na ya baadaye ya Yesu (amani juu yake) - mawazo potofu ambayo athari zake za hatari siyo tu zimelidhuru na kuliteketeteza wazo la kuwako kwa umoja wa Mungu, bali pia ushawishi usiofaa na wenye sumu kwa muda mrefu umekuwa ukionekana katika maadili ya Waislamu wa nchi hii (India). Maradhi ya kiroho, yaani utovu wa maadili mema, mawazo machafu, ukatili na utovu wa huruma vinaendelea mionganini mwa firqa za Kiislamu na ni matokeo ya kuziamini hadithi na hekaya kama hizi zisizokuwa na msingi. Huruma ya binadamu, majuto na kupenda haki, upole na unyenyekevu - sifa zote nzuri zinatoweka siku hadi siku, kana kwamba hivi karibuni zitaiaga jamii hii. Ukatili huu na utovu huu wa maadili mema unawafanya Waislamu wengi waonekane kama wanyama wa porini. Mfuasi wa Buddha ambaye katika dini ya Kibuddha huitwa Jain huogopa na hujiepusha na kuua hata mmbu au kiroboto, lakini lo! wako wengi mionganini mwa sisi Waislamu ambao wanaua mtu asiyekuwa na hatia au kufanya mauaji yasiyokuwa na mipaka, hawamuogopi Mwenyezi Mungu mwenye nguvu ambaye ameyakadiria maisha ya binadamu kuwa ya daraja la juu kuliko yale ya wanyama wote. Lakini huu ukatili na dhuluma na utovu wa huruma vinasababishwa na nini? Vinasababishwa na jambo

hili - kwamba tangu wakati wa utoto wao, hekaya na hadithi na fikra potofu za itikadi ya Jihadi vinaimbwa ndani ya masikio yao na kushinikizwa katika miyo yao, matokeo yake yakiwa kwamba polepole wanakufa kiroho na kutokuhisi ubaya wa vitendo vyao vya kuchukiza; la, bali yule mtu anayemwua mtu mwингine bila kutarajiwa na hivyo kuleta maangamizi kwenye familia ya mtu aliyeuawa, hudhania kwamba amefanya kitendo kinachostahili; au tuseme, kwamba ameitumia vema fursa ya kujipatia upendeleo kutoka kwa jamii yake. Kwa vile hakuna mafundisho au hotuba zinazotolewa nchini mwetu kuzuia uovu wa namna hiyo - na iwapo kuna mafundisho yo yote ya namna hiyo yana viini vya unafiki ndani yake - watu - wa kawaida huwa na fikra za kuviunga mkono vitendo hivyo viovu. Kwa hiyo basi, kwa kuwahurumia watu wangu mwenyewe, nimetunga vitabu kadhaa, kwa Kiurdu, Kiajemi na Kiarabu ambamo nimesema kwamba maoni yanayoshikiliwa na watu wote kuhusu Jihadi ambayo yamezagaa mionganii mwa Waislamu, yaani, kusubiriwa kwa Imamu mwenye kumwaga damu aliyejawa na chuki na uadui kwa watu wengine ni mfumo wa imani potofu zilizofundishwa na maulamaa wasioona mbali; vinginevyo, Islam hairuhusu utumiaji wa upanga kuieneza Imani hii; isipokuwa wakati wa vita vya kujihami au wakati wa vita zinazopiganwa ili kumwadhibu mdhalimu au kutetea uhuru. Haja ya kuwepo kwa vita ya kujihami inakuja wakati ambapo uchokozi wa adui unahatarisha maisha ya mtu. Basi hizo ndizo aina tatu za Jihadi zinazoruhusiwa na sheria, na kinyume cha hizi aina tatu, hakuna aina nyingine ya vita ambayo inaruhusiwa na Islam katika kuizagaza Imani. Kwa kifupi nimetumia kiasi kikubwa cha fedha katika kuvichapisha vitabu hivyo na nimevitangaza humu nchini, na nchini Arabia na Syria na Khurasan na kadhalika. Lakini kwa msaada wa Mwenyezi Mungu sasa nimegundua hoja zenyе nguvu sana ambazo zitatumika katika kuzifutilia mbali imani hizi potofu miyoni mwa watu. Ninao uthibitisho ulio wazi, ninao ushahidi wa kimazingira usiokuwa na shaka, na ninao ushahidi wa kihistoria ambao nuru ya ukweli wake inaleta matumaini makubwa kwamba mara baada

ya kutangazwa kwa ushahidi huo patatokea mabadiliko ya ajabu katika nyoyo za Waislamu dhidi ya imani hizo potofu. Na natumaini bali nina hakika kwamba baada ya mambo haya ya kweli kufahamika, zitabubujika kutoka katika mioyo ya wachamungu wana wa Islam zile chemchem tamu na safi za unyenyekevu, huruma na amani, na kwamba yatatokea mabadiliko ya kiroho ambayo yatakuwa na ushawishi mzuri na wenye baraka nyingi katika nchi hii (India). Nina uhakika pia kwamba wachunguzi wa Kikristo na watu wengine wote wanaoutamani na wenye kiu ya kuupata ukweli huu, watafaidika sana na vitabu vyangu. Na huu ukweli nilioutaja hivi punde, kwamba shabaha halisi ya kitabu hiki ni kuzisahihisha imani potofu ambazo zimekuwa sehemu ya kanuni za imani za Waislamu na Wakristo, unahitaji maelezo kidogo ambayo nayatoa hapa chini.

Naifahamike kwamba takriban Waislamu na Wakristo wote wanaamini kwamba Yesu (amani ya Mungu juu yake) alipaa mbinguni akiwa hai; watu wote hawa waliendelea kuamini kwa muda mrefu kwamba Yesu (amani juu yake) yungali hai huko mbinguni na baadaye katika siku za mwishoni atashuka ardhini. Tofauti iliyopo katika maoni yao, yaani maoni ya wafuasi wa Islam na yale ya Wakristo ni hii tu kwamba Wakristo wanaamini kwamba Yesu (amani juu yake) alifia msalabani, alifufuliwa, na alipaa mbinguni akiwa na mwili wake, aliketi mkono wa kulia wa Baba yake, na atakuja duniani katika siku za baadaye ili kuja kuhukumu, wanasema pia kwamba Mwumbaji na Bwana wa ulimwengu huu ni huyu huyu Masihi Yesu na si mwingine ye yote; yeye ndiye yule ambaye katika siku za mwisho wa dunia atashuka ardhini kwa mshuko wa utukufu ili kuja kutoa adhabu na thawabu; kisha, wale wote ambao hawatamwamini yeye au mama yake kama Mungu, watakotwa na kutupwa jahanamu ambamo kazi yao itakuwa kulia na kuomboleza. Lakini firqa zilizokwisha semwa za Waislamu zinasema kwamba Yesu (amani juu yake) hakusulubiwa; isipokuwa, wakati Mayahudi walipomtia mbaroni ili kumsulubu malaika wa Mungu alimchukua na kumpeleka mbinguni akiwa na mwili wake wa kidunia na bado yungali hai

huko mbinguni - ambayo wanaiita mbingu ya pili ambako pia yuko nabii Yahya, yaani Yohana. Zaidi ya hayo Waislamu wanasema pia kwamba Yesu (amani juu yake) ni nabii mashuhuri wa Mwenyezi Mungu, lakini si Mungu wala si mwana wa Mungu na wanaamini kwamba katika siku za akheri zamani atashuka ardhini karibu na Mnara wa Demeshki au karibu na sehemu nyingine akiwa amebebwa juu ya mabega ya malaika wawili, na kwamba ye ye na Imam Muhammad Mahdi ambaye atakuwa tayari yuko ulimwenguni, na ambaye atakuwa ametokana na uzao wa Faatimah, watawaua wote wasiokuwa Waislamu bila kumwacha ye yote hai isipokuwa wale ambao pale pale na bila kuchelewa watasilimu.

Kwa ufupi shabaha halisi ya kushuka duniani kwa Yesu (amani juu yake) isemwavyo na firqa za Kiislamu zii twazo Ahli-Sunna au Ahli-Hadithi ambazo watu wa kawaida wanaziita Wahabii - ni hii kwamba, kama alivyofanya Mahadev wa Wahindu, ni lazima auteketeze ulimwengu wote; kwamba ni lazima kwanza awalazimishe watu kusilimu na kisha iwapo wataendelea kutokuamini awaae wote kwa upanga; zaidi ya hayo wanasema kwamba ye ye yu hai mbinguni akiwa na mwili wake wa kidunia ili nguvu za Kiislamu zitakapodhoofika ateremke na kuwaua wasiokuwa Waislamu au kuwalazimisha kwa kuwatia uchungu mkali ili wasilimu. Kuhusiana na Wakristo, hususan viongozi wa firqa hizo zilizokwisha tajwa, wanasema kwamba wakati Yesu (amani juu yake) atakapoteremka kutoka mbinguni atavunja misalaba yote ulimwenguni, atafanya vitendo vingi vya kikatili kwa kutumia upanga, na ataujaza ulimwengu kwa mafuriko ya damu. Na kama nilivyokwisha sema, hawa watu, yaani Ahli-Hadithi na kadhalika watokao mionganoni mwa Waislamu wana jazba kubwa sana kuhusu hii imani yao kwamba muda mfupi kabla ya kuteremka Masihi atatokea Imam kutoka mionganoni mwa Banii Faatima ambaye jina lake litakuwa Muhammad Mahdi. Huyu ndiye atakayekuwa Khalifa na Mfalme wa wakati ule, na kwa kuwa atatokana na Wakureshi, shabaha yake halisi itakuwa kuwaua wote wasiokuwa Waislamu isipokuwa wale ambao wataitamka

Kalima mara moja. Yesu (amani juu yake) atateremka ili kumsaidia huyu Imam katika kazi hiyo; na ingawa Yesu mwenyewe (amani juu yake) atakuwa Mahdi, la, bali Mahdi mkubwa zaidi -hata hivyo kwa kuwa Khalifa wa zama hizo lazima awe Mkureshi, Yesu (amani juu yake) hatakuwa Khalifa wa zama hizo. Khalifa wa zama hizo atakuwa huyo huyo Muhammad Mahdi. Wanasema kwamba hawa wawili kwa pamoja wataijaza dunia kwa damu ya binadamu, na watamwaga damu nydingi zaidi kuliko iliyowahi kumwagwa hapo kabla katika historia ya ulimwengu huu. Mara tu watakapo jitokeza wataanza kampeni hii ya umwagaji damu. Hawatahubiri wala kumsihi mtu wala kuonyesha ishara yo yote. Na pia wanasema kwamba ingawa Yesu (amani juu yake) atakuwa kama mshauri au naibu wa Imam Muhammad Mahdi, na ingawa hatamu za uongozi zitakuwa mionganoni mwa Mahdi peke yake, Yesu (amani juu yake) atamchochea Hadhrat Imam Muhammad Mahdi kuua watu wote ulimwenguni na atamshauri kuchukua hatua kali, yaani atayafanya marekebisho yale mafundisho yake ya kuhurumiana aliyojatoa hapo kabla, yaani, usishindane na shari yo yote na maovu, na "ukipigwa shavu moja ugeuze jingine pia."

Hivi ndivyo Waislamu na Wakristo waaminivyo kumhusu Yesu (amani juu yake), na wakati ambapo ni kosa kubwa wafanyakayo Wakristo kumwita binadamu mnyonge "Mungu," imani za baadhi ya wafuasi wa Islam, mionganoni mwao ikiwamo hii firqa inayoitwa Ahli-Hadithi ambayo pia inajulikana kama Wahabii, kuhusu Mahdi mwenye kumwaga damu na Masihi mwenye kumwaga damu, zinaathiri maadili yao vibaya sana, kwa kiasi hiki ambapo kutokana na ushawishi mbaya wa imani hizo, ushirikiano wao na watu wengine hauko katika misingi ya uaminifu na nia nzuri wala hawawezi kuwa watiifu kikwelikweli na kikamilifi kwa serikali isiyokuwa ya Kiislam. Watu wote wenye busara watatambua kwamba imani kama hiyo, yaani kwamba wasiokuwa Waislamu washurutishwe, kwamba imma wasilimu mara moja au wauawe ni lazima itapingwa kwa njia zote. Kila mtu mwenye kupenda mema atakubali mara moja kwamba kabla mtu

hajatambua nya kutosha ukweli wa imani fulani, na kabla hajatambua uzuri wa imani hiyo na mafundisho yake safi, haifai kabisa kumshurutisha kwa njia ya kumtia machungu makali ili aikubali Imani hiyo. Kinyume kabisa cha kuchangia katika ukuwaji wa Imani hiyo, kitendo hicho kitawapatia wapinzani fursa ya kuitoa makosa. Matokeo ya mwisho ya kanuni hii ni kwamba nyoyo zitakuwa zimehamwa na ile sifa ya huruma ya kibinadamu na kwamba amani na haki ambazo ni sifa kuu za maadili ya kibinadamu zinamhama mtu kabla na badala yake chuki na uadui vinaelekeza kuota mizizi; zinazosalia nyuma ni silika za kinyama tu zikiendelea kufutilia mbali maadili yote mema. Lakini itatambulika kwamba fundisho kama hilo halitakuwa limetoka kwa Mwenyezi Munngu, ambaye hashushi adhabu Yake isipokuwa tu baada ya kukamilisha hoja Zake.

Kwa hiyo jambo hili ni lazima lifikiriwe kwa makini: Kwamba iwapo kuna ambaye haikubali Imani ya kweli kwa sababu bado yungali mjinga na hajui ukweli wake, hajui mafundisho yake na hajui uzuri wake, je, itakuwa jambo la busara kumwua mtu wa namna hiyo mara moja? Sivyo, mtu huyu anastahili kuhurumiwa; anastahili kufundishwa polepole kwa heshima kuhusu ukweli, uzuri na faida za kiroho za imani ile; siyo akikataa basi kukataa kwake kujibiwe kwa upanga au bunduki.

Kwa hiyo, itikadi ya Jihadi inayopendekezwa na firqa hizi na pia ile imani kwamba wakati umekaribia ambapo patatokea Mahdi mwenye kumwaga damu ambaye jina lake litakuwa Imam Muhammad, na kwamba Masihi atateremka kutoka mbinguni ili kuja kumsaidia, na kwamba hao wawili kwa pamoja watawaua watu wote wasiokuwa Waislamu iwapo wataukataa Uislam, yote haya ni kinyume kabisa na maadili ya kiakili. Je imani hii siyo ile imani ambayo inaua sifa zote nzuri na maadili mema ya binadamu na kutilia nguvu sifa za maisha ya porini? Wale wanaoshikilia imani kama hizi wanaishi maisha ya kinafiki kwa kulinganishwa na watu wengine, kwa kiasi hiki kwamba hawawezi kuonyesha utii wa kweli kwa viongozi wa serikali wa Imani nyininge, wanaapa kiudanganyifu kuwa watiifu kwa viongozi hao, ambalo ni kosa.

Hii ndiyo sababu baadhi ya firqa za Ahli-Hadithi nilizozitaja hivi punde zinaishi maisha ya namna mbili chini ya serikali ya Kiingereza katika India inayotawaliwa na Uingereza. Kisirisiri wanawapa matumaini watu wa kawaida kuhusu ujaji wa siku za umwagaji damu za Mahdi mwenye kumwaga damu na kuwafundisha jinsi watakiwavyo kufanya wakati huo, lakini wanapokwenda kwa viongozi wa serikali wanawasifu kwa sifa za uwongo na kuwahakikishia kwamba wao hawaungi mkono mawazo ya namna hiyo. Lakini kama ni kweli kwamba wao hawaungi mkono mawazo ya namna hiyo, kwa nini hawatangazi msimamo wao huo kimaandishi na kwa nini wao waendelee kusubiri ujaji wa yule Mahdi na Masihi ambao kama isemwavyo wako kwenye kizingiti cha mlango tu, wakiwa tayari kuja kuungana nao katika kampeni zao?

Kwa kifupi imani kama hizo zimeharibu kwa kiwango kikubwa sana tabia za Mashekhe hawa; hawana uwezo wa kuwafundisha watu adabu wala amani. Kwa upande mwingine, kuwaua watu wengine bila sababu ya msingi, kwao ni wajibu mkubwa wa kidini. Ningefurahi sana kama firqa yo yote ya Ahli-Hadithi ingezipinga imani hizi, lakini kwa masikitiko makubwa siwezi kujizuia kusema kwamba mionganoni mwa hizi firqa za Ahli-Hadithi⁽¹⁾ wako wale ambao kwa sirisiri wanaamini kufika kwa Mahdi mwenye kumwaga damu na dhana zilizoenea kuhusu Jihadi. Hawazikubali fikra sahihi na wanakihesabu kitendo cha kuua kwamba ni chenye kustahili pale wapatapo fursa ya kuwaua watu wanaoungama imani zingine, wakati ambapo hizi imani za kuwaua watu wengine kwa jina la Islam, au kuziamini tabiri kama huu utabiri wa kuja Masihi mwenye kumwaga damu na kutaka kuiendeleza silsila ya

(1) Baadhi ya Ahli-Hadithi wanasema isivyopasa na bila haki yo yote katika vitabu vyao kwamba kufika kwa Mahdi kumekaribia sana: Kwamba atawatia gerezani watawala wa Kiingereza wa India na kwamba mfalme wa Kikristo atakamatwa na kuletwa mbele yake. Vitabu kama hivyo bado vinaweza kupatikana katika nyumba za hawa Ahli-Hadithi, kimojawapo kikiwa Iqtarabus-Sa'at cha Ahli-Hadithi aliye mashuhru sana, ambamo katika ukurasa wa 64 taarifa kama hiyo inaweza kuonekana.

Islam kwa umwagaji damu au kwa vitisho, ziko kinyume kabisa na Qur'an Tukufu na Hadithi zenyе kuaminika. Mtume wetu Mtukufu (amani na rehema za Mwenyezi Mungu juu yake) alipata mateso makali sana mikononi mwa makafiri akiwa Makka na pia baadaye. Miaka kumi na mitatu aliyokaa Makka ilikuwa miaka ya usumbu na mateso ya kila aina - kuifikiria miaka hiyo kunasababisha machozi yatiririke katika macho ya mtu. Lakini yeye hakuinua upanga dhidi ya maadui zake, wala hakuujibu uchokozi wao mpaka wengi miongoni mwa masahaba zake na rafiki zake wapenzi walipouawa kinyama; na mpaka yeye mwenyewe alipotiwa katika mateso ya kila namna kama vile kutiliwa sumu mara nyingi; na mpaka majoribio mengi ya kutaka kumwua yalipofanywa. Lakini ulipizaji wa Mwenyezi Mungu ulipowadia, ikatokea kwamba wazee wa Makka na machifu wa makabila mbalimbali kwa pamoja waliamua kwamba kwa vyo vyote vile mtu huyu ni lazima auawe. Wakati ule ule, Mwenyezi Mungu ambaye Ndiye Msaidizi wa wapendwa Wake na Msaidizi wa wakweli na wachamungu, Alimjulisha yeye kwamba hakuna kilichosalia katika mji ule isipokuwa ouvu, na kwamba watu wa mji ule walikuwa wamejiandaa kumwua na kwamba ni lazima auhame mara moja. Kisha kulingana na amri ya kimbingu alihamia Madina, lakini pamoja na hatua zote hizo maadui zake hawakumwachilia; wakamfuta kule na wakataka kuuteketeza Uislam kwa njia yo yote ile. Wakati urukaji wao mipaka ulipofikia kikomo, na walipokuwa wao wenyewe wamejihalalishia adhabu kwa kuwaua watu wengi wasiokuwa na hatia, ambao waliwaua siyo katika ugomvi au vita bali hivi hivi tu, kutokana na utundu wao wa kuleta madhara, na ambao waliwanyang`anya mali zao. Lakini, licha ya yote haya, wakati Makka ilipotekwa Mtume wetu Mtukufu (amani na rehema za Mwenyezi Mungu juu yake) aliwasamehe wote hao. Kwa hiyo ni makosa makubwa na si jambo la haki kudhani kwamba Mtukufu Mtume (amani na rehema za Mwenyezi Mungu juu yake) au Masahaba zake waliwahi kupigana kwa nia ya kueneza Imani, au kwamba waliwahi kumlazimisha mtu ye yote kuijunga na silsila ya Islam.

Ni jambo la kuzingatiwa pia kwamba kwa kuwa wakati ule watu wote walikuwa na chuki dhidi ya Islam, na kwa kuwa wapinzani walikuwa wanafanya mpango wa kuuteketeza Uislam ambao waliudhania kuwa ni dini mpya ambayo wafuasi wake ni jumuiya ndogo tu, na kwamba kila mtu alikuwa na shauku ya kuona Waislamu wakiteketeza mapema au kusambaratishwa ili pasiachwe hofu ya hao kuongezeka zaidi na kujiendeleza, Waislamu wa wakati ule waliwekewa vipingamizi hata katika mambo madogo sana, na mtu ye yote kutoka katika kabilia lo lote aliyeupokea Uislam na akawa Mwislamu, imma aliuawa mara moja na watu wa kabilia lake au aliishi katika hatari ya kudumu. Katika wakati kama huu, Mwenyezi Mungu, Akiwahurumia wale waliojiunga na Islam, Aliwatwisha adhabu watawala wadhalimu, yaani wawe wasaidizi kwa Islam na hivyo kufungua milango ya uhuru wa Islam. Hii ilikuwa na shabaha ya kuondoa vipingamizi katika njia ya wale waliotaka kuikubali Imani hii; ilikuwa ni huruma ya Mwenyezi Mungu kwa ulimwengu na haikumdhuru mtu ye yote. Lakini ni jambo lililo bayana kwamba watawala wasiokuwa Waislamu wa siku hizi hawajiingizi katika masuala ya Islam; hawapigi marufuku sunna muhimu za Kiislam. Hawawaui Waislamu wapya; hawawatii gerezani au kuwatesa; kwa nini basi Islam iinue upanga wake dhidi ya watu hawa? Ni dhahiri kwamba Islam haijawahi kushabikia ulazimishaji. Iwapo Qur`an Tukufu, vitabu vyta Hadithi na kumbukumbu za historia vitachunguzwa kwa uangalifu na pale inapowezekana iwapo vitasomwa au kusikilizwa kwa makini, itafahamika kwa yakini madai kwamba Islam ilitumia upanga ili kueneza Imani hiyo kwa nguvu ni madai ya aibu na yasiyokuwa na msingi dhidi ya Islam.

Dai kama hilo dhidi ya Islam linafanya na watu ambao bado hawajaisoma Qur`an, Hadithi na taarikhi za kuaminika za Islam katika hali ya kujitegemea wao wenywewe, bali wameutegemea sana uwongo na kwa hiyo wakaleta madai yenye makosa dhidi ya Islam. Lakini najua kwamba wakati umeisha karibia ambapo wale wenye njaa na kiu ya kutafuta ukweli watatiwa nuru ya kujua iwapo kuna ukweli wo wote katika madai haya. Je tunaweza

kuielezea Imani hii kuwa ni imani ya kutumia nguvu wakati kitabu kitakatifu Qur'an, kinaelekeza wazi kwamba hakuna ushurutishaji katika mambo ya dini na kwamba hairuhusiwi kutumia shuruti au nguvu katika kumfanya mtu ajunge na Islam? Je tunaweza kumshitaki Mtume yule Mkuu kwamba alitumia mabavu dhidi ya watu wengine, ambaye usiku na mchana kwa miaka kumi na mitatu aliwahimiza Masahaba zake wote mjini Makka wasirejeshe uovu waliotendewa na maadui, bali wavumilie na kusamehe? Lakini wakati fujo ya maadui ilipopita kiasi na wakati kila mtu alipokuwa anajitahidi kuufutilia mbali Uislam, Mwenyezi Mungu mwenye ghera Aliamua kwamba ulikuwa ni wakati muafaka wale watu waliopigana kwa upanga lazima wateketezwe kwa upanga. Waila Qur'an Tukufu haijaidhinisha kulazimisha. Kama kulazimisha kungeidhinishwa na Islam, Masahaba wa Mtume wetu Mtukufu (amani na rehema za Mwenyezi Mungu juu yake) wasingeonyesha tabia ya watu wakweli na wanyoofu, wakati wa majaribu. Lakini utiifu na uaminifu wa masahaba wa Bwana wetu Mtukufu Mtume (amani na rehema za Mwenyezi Mungu juu yake) ni jambo ambalo sina haja ya kulitaja. Si jambo la siri kwamba mionganoni mwao kuna mifano ya msimamo imara ambao ni vigumu kupata cha kuwalinganisha nao katika taariki za mataifa mengine; kundi la waaminio halikutetereka katika utiifu na msimamo wao imara hata walipokuwa chini ya kivuli cha upanga. Bali wakiwa pamoja na Mtume wao Mkuu na Mtukufu walitoa uthibitisho wa ule msimamo imara ambao hakuna mtu awezaye kwa vyo vyote vile kuuonyesha mpaka moyo wake na kifua chake viwe vimetiwa nuru ya imani ya kweli. Kwa kifupi hakuna kulazimisha katika Islam. Vita katika Islam ni vya aina tatu: (1) vita ya kujihami, yaani vita kwa sababu ya kujilinda; (2) vita ya kuadhibu, yaani damu kwa damu; (3) vita ya kupata uhuru, yaani vita ya kuvunja nguvu ya wale wanaowaua wale wanaojiunga na Islam.

Kwa hiyo kwa kuwa hakuna maelekezo katika Islam kwamba kila mtu aingizwe huku kwa kulazimishwa au kwa kutishiwa kuuawa, ni jambo la upuuzi mtupu kusubiri kutokea kwa Mahdi au Masihi ye yote mwenye kumwaga damu. Haiwezi kutokea

kamwe kwamba katika ulimwengu huu atokee mtu ambaye kinyume na mafundisho ya Qur'an atumie upanga kuwasilimisha watu. Hili si jambo gumu kutambua wala haliko nje ya uwezo wa mtu wa kufahamu. Ni watu wajinga tu walioangukia imani hii kutokana na uchoyo wao. Kwani takriban Mashekhe wetu wote wanajihangaisha na fikra zao potofu kwamba vita atakazopigana huyu Mahdi zitawaletea utajiri mwangi sana kiasi kwamba watakuwa hawana mahali pa kuhifadhiya utajiri huo, na kwa kuwa takriban Mashekhe wote wa hivi sasa ni watu walio fukara sana, wanasubiri usiku na mchana kutokea kwa huyo Mahdi ambaye wanadhani atakuja kukidhi hizo tamaa zao za kiuchoyo. Kwa hiyo watu hawa humpinga kila mtu ambaye haamini kutokea kwa Mahdi wa namna hiyo; mtu wa namna hiyo atatangazwa mara moja kuwa ni Kaafir na yuko nje ya wigo wa Islam. Kwa hiyo mimi pia nimekuwa Kaafir machoni pa watu hawa; na nimepewa ukafiri huo kwa misingi hiyo hiyo. Kwani, mimi siamini kutokea Mahdi mwenye kumwaga damu na Masihi mwenye kumwaga damu. La, bali nayachukia mawazo ya kipuuzi ya namna hiyo na nayadharau sana. Na nimetangazwa kuwa Kaafir siyo tu kwa sababu ya kukanusha kwangu kutokea kwa huyo anayesemekana kuwa Mahdi na huyo anayesemekana kuwa Masihi ambao wanaamini, bali pia nimetangaza hadharani baada ya kujulishwa jambo hili na Mwenyezi Mungu kwa njia ya ufunuo kwamba Masihi Aliyahidiwa halisi na wa kweli ambaye pia ndiye Mahdi wa kweli ambaye ishara za kutokea kwake zinapatikana katika Biblia na Qur'an na ambaye kuja kwake kumeahidiwa pia katika Hadithi, ni mimi mwenyewe; lakini ni mimi ambaye sikupewa upanga wo wote wala bunduki. Nimeamrishwa na Mwenyezi Mungu kuwaita watu kwa unyenyekevu na upole kwa Mwenyezi Mungu Ambaye ndiye Mungu wa kweli, na milele na Asiyebadilika Ambaye ana Utakatifu uliokamilika, Ujuzi uliokamilika, Amani iliyokamilika na Haki iliyokamilika.

Mimi ndiye nuru ya zama hizi za giza; yule ambaye atanifuata mimi ataokolewa katika kutumbukia ndani ya shimo lililotayarishwa na Shetani kwa ajili ya wale wanaotembea katika giza.

Nimeletwa na Mwenyezi Mungu ili kuwaongoza watu wa ulimwengu huu kwa Mungu wa kweli kwa njia ya amani na upole na kuzifunga upya hatamu za maadili mema katika Islam. Mwenyezi Mungu amenipatia ishara za kimbingu kwa ajili ya kuwaridhisha wale wenye kutafuta haki. Amefanya mambo ya ajabu katika kuniunga mkono; Amenifunulia siri za mambo ya ghaibu na za mambo yajayo baadaye ambayo kulingana na vitabu vitakatifu ni ishara za mdai wa kweli wa ofisi ya kimbingu, na Akanijaalia elimu safi na takatifu. Kwa hiyo, zile nafsi ambazo zinachukia ukweli na zinafurahishwa na giza zikaamua kunipinga. Lakini niliamua kuwahurumia binadamu - kwa kadiri nilivyoweza. Kwa hiyo huruma kubwa zote wawezazo kufanyiwa Wakristo katika zama hizi ni kuyaelekeza mawazo kwenye Mungu wa kweli Ambaye ameepukana na zile kasoro kama vile kuzaliwa na kufa na kupata mateso; Yule Mungu ambaye aliziumba sayari zote za awali huko mbinguni katika umbo la mviringo na katika kanuni Yake ya hali ya asili aliweka kigezo hiki cha mwongozo wa kiroho kwamba kama vile liliyuo umbo la mviringo, kuna Umoja ndani Yake Yeye na kwamba ndani ya Yeye hakuna welekeea. Hii ndiyo sababu vitu vilivyomo mbinguni havikutengenezwa kwa umbo la pembe tatu, yaani vitu ambavyo Mwenyezi Mungu aliviumba hapo awali kama vile ardhi, mbingu, jua na mwezi, nyota zote na viini vyta asili vya kila kitu - vyote viko katika umbo la mviringo, ambapo hali yao ya asili ya kuwa mviringo inaashiria kwenye Umoja. Kwa hiyo hapawezi kuwa na kuwahurumia Wakristo zaidi kuliko kwamba waelekezwe kwenye Ambaye alivyoviumba vinamtangaza Yeye kuwa ameepukana na wazo la utatu.

Na huruma kubwa kuliko zote kwa Waislamu ni lazima wageuzwe kimaadili na kwamba lazima juhudi ifanywe kuondoa matumaini ya kiudanganyifu wanayoyashikilia kuhusiana na kutokea kwa Mahdi na Masihi mwenye kumwaga damu, ambayo yako kinyume kabisa na mafundisho ya Kiislamu. Na nimekwisha sema hivi punde kwamba mawazo ya baadhi ya Maulamaa wa siku hizi kwamba patatokea Mahdi mwenye kumwaga damu ambaye ataeneza Uislam kwa ncha ya upanga, yote hayo yako

kinyume cha mafundisho ya Qur'an na ni matokeo yasiyo cho chote isipokuwa uroho na uchoyo.

Ili mtu mwenye akili timamu na Mwislamu mpenda ukweli aweze kuachana na imani na mawazo kama hayo, itamtosha tu kuisoma Qur'an kwa uangalifu na kutafakari, na ataona kwamba Neno Takatifu la Mwenyezi Mungu liko kinyume kabisa na utoaji wa vitisho vya kuua ili kumlazimisha mtu ye yote kuingia katika boma la Islam. Kwa kifupi, hoja hii moja tu inatosha kabisa kuyakanusha mawazo haya ya udanganyifu. Hata hivyo, kutokana na hisia za huruma nimeamua kuyakanusha mawazo hayo yaliyokwisha tajwa kwa uthibitisho madhuhuti na ulio wazi kutoka katika historia, na kadhalika. Kwa hiyo, nitajaribu kuthibitisha katika kitabu hiki kwamba Yesu (amani juu yake) hakufia msalabani, hakwenda juu mbinguni wala isidhaniwe kamwe kwamba atakuja tena ardhini akitokea mbinguni, bali alikufa akiwa na umri wa miaka 120 mahali paitwapo Srinagar katika Kashmir na kwamba kaburi lake linapatikana katika mtaa wa Khan Yar katika mji ule. Ili kutoa maelezo kwa uwazi zaidi nimeugawa uchunguzi huu katika sura kumi; na neno la mwisho ambalo linajumuisha ushahidi wa Biblia, ushahidi wa Qur'an Tukufu na Hadithi, ushahidi wa vitabu vya tiba, ushahidi wa kumbukumbu za historia, ushahidi wa mapokeo ya mdomo ambayo yamerithiwa toka kizazi hadi kizazi, ushahidi wa ziada wa kimazingira, ushahidi wa hoja za kiakili na ushahidi wa ufunuo mpya kutoka kwa Mwenyezi Mungu kuhusu kuja kwangu. Hizi zinajumuika kuwa sura kumi. Katika sura ya 9 kutakuwa na malinganisho mafupi kati ya Ukristo na Uislam na zitapangwa hoja zenye kuthibitisha ukweli wa Islam. Katika sura ya 10 kutakuwa na maelezo marefu kidogo kuhusu malengo ya kutekelezwa ambayo kwa ajili ya hayo mimi kuwa ndiye Masihi Aliyahidiwa na kuwa mimi nimekuja kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Na mwishowe, kutakuwa na neno la mwisho ambamo yataratibiwa maagizo fulani fulani.

Natumaini wasomaji wa kitabu hiki watakisoma kwa bidii. Sitazamii kwamba watautupilia mbali ukweli uliomo humu kutokana na chuki isiyokuwa na sababu. Ningependa

kuwakumbusha kwamba huu sio uchunguzi wa juu juu tu; bali uthibitisho uliomo ndani ya kitabu hiki umepatikana baada ya utafiti wa ndani na wa kina.

Namwomba Mwenyezi Mungu anisaidie katika jukumu hili na aniongoze kwa njia ya ufunuo na mwongozo Wake maalum na kwa njia ya Nuru kamili ya ukweli - kwani elimu ya kweli na utambuzi halisi hushuka kutoka Kwake, na kwa njia ya idhini kutoka Kwake Yeye tu, niweze kuiongoza mioyo ya watu kwenye ukweli. Amin! Amin!

MIRZA GHULAM AHMAD

Qadian, Tarehe 25 Aprili, 1899.

Kwa Jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu,

SURA YA KWANZA

Ifahamike kwamba ingawa Wakristo wanaamini kwamba Yesu (amani juu yake) baada ya kukamatwa kwa sababu ya usaliti wa Yuda Iscariot na kusulubiwa na kufufuka alikwenda mbinguni, hata hivyo, kulingana na Biblia Takatifu inaelekea kwamba imani yao hii ni yenye makosa moja kwa moja. Mathayo (sura ya 12 aya ya 40) anasema kwamba kama vile Yona alivyokaa michana mitatu na mausiku matatu katika tumbo la samaki, vivyo hivyo Mwana wa Adamu nae atakaa michana mitatu na mausiku matatu ndani ya tumbo la ardhi; Sasa ni dhahiri kwamba Yona hakufa ndani ya tumbo la samaki; sana sana kilichotokea ni kwamba alikuwa katika hali ya kuzirai au kuzimia. Vitabu vitakatifu vyta Mwenyezi Mungu vinashuhudia kwamba kwa msaada wa Mwenyezi Mungu Yona alibakia hai katika tumbo la samaki na alitoka humo akiwa hai; na hatimae watu wake wakampokea. Iwapo basi Yesu (amani juu yake) alifia ndani ya tumbo la "ardhi", pangekuwapo na kufanana gani kati ya mtu mfu na aliye hai, na ingewezekanaje kulinganisha mtu aliyekufa na aliye hai? Bali ukweli ni kwamba Yesu alikuwa nabii wa kweli na kwa kuwa alijua kwamba Mwenyezi Mungu Ambaye ye ye aliwa mpendwa wake Atamwokoa na kifo cha laana, alitoa utabiri kwa njia ya methali iliyofunuliwa kwake na Mwenyezi Mungu ambamo alidokeza hatakufa juu ya msalaba wala hatakata roho juu ya ubao uliolaaniwa; kinyume cha hayo, kama vile ilivyokuwa kwa nabii Yona, ye ye atapitia katika hali ya kuzimia tu. Katika methali hiyo amedokeza pia kwamba atatoka nje ya tumbo la ardhi na kisha ataungana na watu, na kama vile ilivyokuwa kwa Yona, ataheshimiwa na watu hao. Kwa hiyo, utabiri huu pia ultimia; kwani Yesu, akiwa ametoka katika tumbo la ardhi, aliyaeenda makabila yake yaliyoishi nchi za Kashimir, Tibet na kadhalika, yaani yale makabila kumi ya Waisraeli ambao miaka 721⁽¹⁾

(1) Licha ya hawa, Wayahudi wengi zaidi walilazimishwa kuishi ugenini katika nchi za mashariki kutokana na unyama wa Wababilonia.

kabla ya Yesu yalitekwa nyara kutoka Samaria na Shalmaneser, mfalme wa Assur na akaondoka nayo. Hatimaye makabila haya yalikuja India na yakajifanya maskani katika sehemu mbalimbali za nchi hii. Na kwa vyo vyote vile ni lazima Yesu awe aliifanya safari hii, kwani shabaha ya kimbingu ya kuja kwake ilikuwa ni lazima akutane na Wayahudi waliopotea ambao walikuwa wakiishi katika sehemu mbalimbali za India; sababu yake ilikuwa kwamba kwa hakika hawa ndio waliokuwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli ambao hata ile imani ya mababu zao walikuwa wameiacha wakiwa katika nchi hizi na wengi wao wakawa wameingia katika dini ya Kibuddha na kurejea polepole kwenye ibada ya masanamu. Dakta Bernier, kwa kuwanukuu watu kadha walio wasomi, anasema katika kitabu chake kitiwacho *Travels* kwamba Wakashmiri kwa hakika ni Wayahudi ambao wakati wa mtawanyiko uliotokea wakati wa zama za yule mfalme wa Assur, walihamia katika nchi hii.⁽¹⁾

Ilmuradi ilikuwa ni lazima kwa Yesu (amani juu yake) kutafuta mahali walikokuwa hawa kondoo waliopotea ambao, baada ya kuja katika nchi hii ya India, wakachangnyika na watu wengine. Hivi punde nitatoa ushahidi kwamba kwa hakika Yesu (amani juu yake) alikuja India, na kisha, hatua kwa hatua akaenda Kashmir na kuwagundua kondoo waliopotea wa Israeli wakiwa miongoni mwa watu walioungama imani ya Kibuddha na kwamba hatimae watu hawa walimpokea kama vile watu wa nabii Yona walivyompokea Yona. Na hili lilikuwa ni jambo la lazima, kwani Yesu alisema mara chungu nzima kwamba ametumwa kwa ajili ya kondoo waliopotea wa Israeli.

Licha ya hayo, ilikuwa lazima aepukane na kifo juu ya msalaba kwani ilikwisha semwa katika kitabu kitakatifu kwamba ye yote mwenye kutundikwa juu ya mti amelaaniwa. Na ni kufuru ya kikatili na isiyokuwa ya haki kumnasibisha na laana mtu mashuhuri kama Masihi Yesu, kwani kulingana na maoni ya wote wale wanaoijua lugha hii, neno *La`nat* au laana lina marejeo kwenye hali ya moyo wa mtu.

(1) Dr. Bernier, *Travels* Vol. II. Appendix I

Mtu atasemekana kuwa amelaaniwa wakati moyo wake, baada ya kutenganishwa na Mwenyezi Mungu unakuwa mweusi kweli kweli; unapokuwa umenyimwa amani ya kimbingu na mapenzi ya kimbingu; ukiwa hauna kabisa elimu Yake; akiwa amepofushwa kama shetani, anakuwa amejazwa sumu ya ukafiri; wakati ambapo hapabaki hata chembe moja ya mapenzi na elimu ya kimbingu katika nafsi yake; wakati fungamano la utii linapokuwa limevunjika, na kati yake ye ye na Mwenyezi Mungu panazuka chuki, dharau, kinyongo na uadui, kwa kiasi hiki kwamba Mwenyezi Mungu na ye ye wanakuwa maadui wao kwa wao; na wakati Mwenyezi Mungu Anapochoshwa na ye ye; na ye ye kuwa amechoshwa na Mwenyezi Mungu; kwa kifupi wakati anapokuwa mrithi wa sifa zote za Shetani - na hii ndiyo sababu Shetani mwenyewe anaitwa mlaaniwa ⁽¹⁾. Ni dhahiri kwamba maana ya neno *Mal'un* yaani mlaaniwa ni chafu sana hivi kwamba haiwezi kunasibishwa kwa mtu ye yote aliye mchamungu ambaye hukaribisha mapenzi ya Mwenyezi Mungu katika moyo wake. Laahaula! Wakristo hawakutafakari sana kuhusu maana ya laana walipobuni imani hii; vinginevyo wasingaliweza kutumia neno baya kama hilo kwa mtu mchamungu kama Yesu. Je, tunaweza kusema kwamba moyo wa Yesu uliwhali kutengana na Mwenyezi Mungu, kwamba alimkana Mungu, kwamba alimchukia Mungu na akawa adui Yake? Je, tunaweza kudiriki kudhania kwamba Yesu aliwhali kuhisi katika moyo wake kwamba alikuwa ametengwa na Mwenyezi Mungu, kwamba alikuwa adui wa Mwenyezi Mungu na kwamba alikuwa amezama katika giza la ukafiri na ukaini? Iwapo basi Yesu kamwe hakuwa katika hali ya moyo ya namna hiyo, kwamba moyo wake ulikuwa kila mara umejawa na mapenzi na nuru ya elimu ya kimbingu, je ipo haja kwenu watu wenyewe hekima kutafakari iwapo tunaweza kusema kwamba si moja tu bali maelfu ya laana kutoka kwa Mwenyezi Mungu yalishuka katika moyo wa Yesu pamoja na maana mbaya yote ya laana hizo?

(1) Tazama makamusi: Lisanul - Arab, Sihah Jauhar, Quamus, Muhit, Tajul-Arus na kadhalika.

Hasha. Tunawezaje basi kusema kwamba (Mungu apishe mbali), alikuwa amelaaniwa? Ni jambo la kusikitisha kwamba mtu anapotoa matamshi kuhusu jambo fulani baada ya kuwa na msimamo kuhusu imani fulani si rahisi kuiachilia imani hiyo hata kama upuuzi wa imani hiyo utabainishwa kwa kila hali.

Tamaa ya kupata uokovu, kama imejengwa katika misingi ya ukweli ni jambo la maana, lakini kuna faida gani kuwa na tamaa ya uokuvu ambayo inaua ukweli na inaipendelea imani inayosema, kumhusu nabii mtukufu na binadamu aliyekamilika kwamba alipitia katika hali ambapo alitenganishwa na Mwenyezi Mungu na ambamo badala ya kuwa na moyo mmoja na msimamo mmoja pakatokea hali ya kukaa mbali na kujitenga, uadui na chuki, na badala ya nuru giza likauzunguka moyo wake?

Ifahamike vilevile kwamba hali hii siyo tu haiendani na unabii na utume wa Yesu (amani juu yake) bali ni kinyume na madai yake ya kuwa na umashuhuri wa mambo ya kiroho, utakatifu, upendo na elimu kumhusu Mungu ambayo ameyaeleza kwa kuyakariri katika Injili. Wewe angalia katika Biblia tu; humo Yesu anadai waziwazi kwamba yeze ndiye Nuru ya ulimwengu, kwamba yeze ndiye Njia, na kwamba yeze anao uhusiano mkubwa sana wa upendo kwa Mwenyezi Mungu; kwamba yeze ameheshimika kwa kuzaliwa uzazi ulio safi na kwamba yeze yu Mwana mpandwa wa Mwenyezi Mungu. Inawezekanaje sasa, pamoja na husiano zote hizi zilizo safi na takatifu, laana yenye maana zote mbaya iweze kunasibishwa na Yesu? Kamwe haiwezekani. Kwa hiyo hapana shaka kwamba Yesu hakusulubiwa, yaani hakufia msalabani, kwa sababu haiba yake haikustahili na matokea ya kifo juu ya msalaba. Na kwa kuwa hakusulubiwa aliepukana na kunasibishwa na sifa mbaya za laana, na bila shaka hii inathibitisha pia hakupaa mbinguni, kwa sababu kupaa mbinguni ni sehemu tu ya mpango wote huu na ni matokeo ya hili wazo kwamba yeze alisulubiwa. Kwa hiyo ikithibitishwa kwamba hakulaaniwa wala hakukaa Jahanamu kwa muda wa siku tatu, wala hakufa, hii sehemu nyingine ya mpango huu, yaani kwamba alipaa mbinguni, itathibitika kuwa ni ya

uwongo. Kuhusu jambo hili Biblia inazo hoja zingine zaidi ambazo nitaendelea kuzitaja hapa chini. Moja ya hoja hizo ni kauli ya Yesu: "Lakini baada ya kufufuka kwangu, nitawatangulieni kwenda Galilaya". (Mathayo Sura ya 26 aya ya 32). Aya hii inaonyesha waziwazi kwamba baada ya kutoka kaburini Yesu alikwenda Galilaya na siyo mbinguni. Na maneno ya Yesu "baada ya kufufuka kwangu" hayana maana ya kufufuka kwake baada ya kufa; bali, kwa kuwa machoni pa Wayahudi na watu wa kawaida "alifia msalabani," aliyatumia mapema yale maneno ambayo yatakubaliana na vile watakavyo mfikiria hapo baadaye. Na kwa kweli mtu ambaye aliwekwa msalabani na ambaye mikono yake na miguu yake ilipigiliwa misumari mpaka akazimia kutokana na uchungu, ni kana kwamba alikuwa amekufa; iwapo mtu huyo aliokolewa kutoka katika baa hilo na kama akaweza kupata fahamu tena, haitakuwa kutia chumvi kuhusiana na mtu kama huyo kusema kwamba amepata uhai tena. Na hapana shaka kwamba, baada ya mateso yote hayo, kuepushwa kwake Yesu na kifo ilikuwa ni mwujiza; halikuwa jambo la kawaida. Lakini kudhania kwamba alikuwa ni makosa. Ni kweli kwamba ndani ya vitabu vya Agano Jipyä maneno ya namna hii yanapatikana, lakini hili ni kosa la waandishi wa vitabu hivyo, kama walivyoweza kufanya makosa ya kurikodi matukio kadhaa ya kihistoria. Wafasirina waliovifanyia utafiti vitabu hivi wanakubali kwamba vitabu vya Agano Jipyä vina sehemu mbili: (1) maagizo ya kiroho yaliyopokelewa na wanafunzi kutoka kwa Yesu (amani juu yake) ambayo ndiyo kiini cha mafundisho ya Injili; (2) matukio ya kihistoria - kama vile ukoo wa Yesu; kutiwa kwake mbaroni na kupigwa; kuwepo kwa kidimbwi cha miujiza wakati wa zama zake na kadhalika. Haya yaliandikwa na waandishi wenywewe; hayakufunuliwa; bali yaliwekwa humo kulingana na mawazo ya waandishi. Katika baadhi ya sehemu kuna kutiwa chumvi kulikozidi kiasi, kama pale mahali panaposema kwamba kama miujiza na kazi zote za Yesu zingehifadhiwa katika vitabu dunia hii isingalikuwa na uwezo wa kuvihifadhi vitabu hivyo. Huku ni kutia chumvi kulioje!

Licha ya hayo, si kinyume cha matumizi ya misemo

kulielezea balaa kubwa lililompata Yesu kuwa ni kifo. Iwapo mtu, baada ya kupita katika hali ya kufa na kupona, hatimaye anaokolewa, msemo wa kawaida wa watu wote huielezea hali hiyo kwa njia ya methali - "amepewa uhai mpya", na hakuna watu hata kama watoke nchi gani, watasita kulielezea jambo hili kwa njia hii.

Baada ya yote hayo kusemwa, ni lazima izingatiwe kwamba katika Injili ya Barnabas, ambayo ni lazima inapatikana katika Jumba la Makumbusho la Uingereza, imetamkwa kwamba Yesu hakusulubiwa wala hakufia msalabani. Sasa tunaweza kusema vizuri sana kwamba ingawa kitabu hiki si mionganoni mwa vitabu vilivyomo katika Injili na kimekataliwa moja kwa moja, lakini hapana shaka kwamba ni kitabu cha kale na ni cha zama zile zile ambapo Injili zingine ziliandikwa. Je, hatuna fursa ya kukihesabu kitabu hiki cha kale kuwa ni kitabu cha historia ya zama za kale na kukitumia kama kitabu cha historia? Je, si dhahiri kutokana na kitabu hiki kwamba kwa uchache wakati wa tukio la msalaba watu hawakukubaliana kwa kauli moja kuhusu Yesu kufa juu ya msalaba? Tena, licha ya hayo, wakati ambapo katika Injili nne zenyewe kuna methali kama vile ya mtu aliyefariki kusemwa kwamba, hakufa bali amelala, si jambo lisiloingia akilini kuwaza kwamba hali ya kuzimia inaweza kuelezewa kama hali ya kifo. Nimekwisha sema kwamba nabii hawezo kusema uwongo. Yesu alizilinganisha siku zake tatu za kukaa kaburini na zile siku tatu za Yona za kukaa ndani ya nyangumi. Hii inaonyesha tu kwamba kama vile Yona alivyobakia hai kwa siku tatu katika tumbo la nyangumi, ndivyo hivyo Yesu alivyobakia hai kwa siku tatu akiwa kaburini. Makaburi ya Mayahudi ya siku zile hayakuwa kama makaburi yetu ya siku hizi; yalikuwa na nafasi kubwa na yalikuwa na mlango upande mmoja ambao ulifunika kwa jiwe kubwa. Na hivi punde nitathibitisha nitakapofika mahali panapostahili kwamba kaburi la Yesu ambalo limegunduliwa hivi karibuni mjini Srinagar katika Kashmir ni la namna ile ile kama alimowekwa Yesu wakati akiwa katika hali ya kuzimia.

Kwa kifupi, aya niliyokwisha inukuu hivi karibuni inaonyesha

kwamba baada ya kutoka kaburini Yesu alikwenda Galilaya. Na Injili ya Mtakatifu Marko inasema kwamba baada ya kutoka kaburini alionekana katika barabara inayokwenda Galilaya, na hatimaye akakutana na wale wanafunzi kumi na mmoja walipokuwa wakila chakula; aliwaonyesha mikono na miguu yake ambayo ilikuwa na majeraha na wakadhania pengine yeye alikuwa kiumbe cha kiroho. Ndipo akawaambia: " Tazameni mikono yangu na miguu yangu, ni mimi yule yule; nishikeni muone, kwani kiumbe cha kiroho hakina nyama na mifupa kama hii mnayoniona nayo" (Luka 24:39). " Akatwaa kutoka kwao samaki aliyechemshwa na kipande cha sega la asali akala mbele yao. (Luka 24:42-43).

Aya hizi zinaonyesha kwamba ni jambo la yakini kabisa kwamba Yesu kamwe hakwenda mbinguni; baada ya kutoka kaburini alikwenda Galilaya; - akiwa kama watu wa kawaida, akivaa nguo za kawaida na akiwa na mwili wa kibinadamu. Kama alifufuliwa baada ya kufa, ilikuwaje mwili huo wa kiroho ulikuwa bado una vidonda alivyovipata msalabani? Alikuwa na haja gani ya kula? Na kama alilhitaji chakula wakati ule, ni lazima awe anahitaji chakula hata sasa.

Wasomaji kwa vyo vyote vile wasibabaishwe na jambo hili: msalaba wa Wayahudi haukuwa kama kitanzi kinachotumika kumnyongea mtu siku hizi, ambacho mtu akitiwa, takriban ni jambo lisilowezekana kutoka humo akiwa hai, kwani msalaba wa siku zile haukuwa na kamba ya kuvishwa shingoni mwa mhusika, wala hakudondoshwa kutoka kwenye ubao kisha ndipo aning'inizwe; bali aliwekwa tu msalabani na mikono yake na miguu ikapigiliwa misumari kwenye msalaba huo; na iliwezekana sana kwamba iwapo baada ya kumsulubisha mtu na kumpigilia misumari iliamuliwa baada ya siku moja au mbili - kumsamehe mtu yule na kuokoa maisha yake, aliteremshwa chini akiwa hai kabla mifupa yake hajavunjwa, ikihesabiwa kwamba adhabu aliyokwisha pata ilikuwa inatosha. Na kama iliamuliwa kumuua, alibakizwa msalabani kwa akali kwa siku tatu; maji au mkate havikuruhusiwa kuletwa karibu naye, na aliachwa katika hali hii akiwa juani kwa siku tatu au zaidi, ndipo mifupa yake ikavunjwa

na hatimaye kutokana na mateso hayo akafa. Lakini rehema ya Mwenyezi Mungu Mwenye nguvu ilimwokoa Yesu katika mateso haya ambayo yangemaliza maisha yake. Usomaji wa Injili hizi kwa uangalifu utaonyesha kwamba Yesu (amani juu yake) hakubakia msalabani kwa siku tatu; hakulazimika kuumwa na njaa au kiu kwa siku tatu; wala mifupa yake haikuvujwa. Bali alibakia juu ya msalaba kwa saa mbili tu, na rehema na huruma ya Mwenyezi Mungu viliweza kuufanya usulubishaji huo ufanyike jioni ya siku ile, ambayo ilikuwa Ijumaa, na muda mfupi tu ulisalia kabla ya jua kuzama, na siku iliyofuata ikiwa ni Sabato ambayo ilikuwa sikukuu ya Fasah ya Mayahudi. Na kulingana na desturi za Kiyahudi ilikuwa hairuhuswi na lilituwa kosa la jinai ambalo kwalo mtu aliadhibiwa, kumfanya mtu ye yote abakie juu ya msalaba katika siku ya Sabato au usiku wa kuamkia siku hiyo; na Mayahudi, kama walivyokuwa Waislamu, walitumia kalenda ya mwezi ambapo usiku huhesabiwa kuwa upande mmoja, kulikuwa na haya mazingira ambayo yalisababishwa na sababu za kidunia, na kwa upande mwengine, Mwenyezi Mungu, Mwenye nguvu Alisababisha kuwepo kwa haya mazingira ya kimbingu, yaani ilipotimia saa ya sita kukatokea dhoruba ya vumbi ambayo ilisababisha kuwepo giza ardhini kwa muda wa saa tatu (Marko Sura 15: aya ya 33). Saa hii ya sita ilikuwa baada ya saa sita mchana, yaani ilipokaribia magharibi. Sasa basi, Mayahudi walishikwa na wasiwasi kutokana na giza hili nene, isije usiku wa Sabato ukawapita na isije kwa kunajisi utakatifu wa Sabato, wakastahili adhabu. Kwa hiyo, kwa haraka wakamwondoa Yesu msalabani pamoja na wale wezi wawili. Zaidi ya hayo yote, kulikuwa na sababu nyngine ya kimbingu, kwamba Pilato alipokuwa akiendesha mahakama yake, mkewe alimpelekea neno kwamba asimfanye lo lote mtu yule mchamungu (yaani asijaribu kumpa adhabu ya kifo), kwa sababu alisema, alipata ndoto usiku ule, ambayo ilimsumbuwa sana. (Mathayo Sura 2 aya ya 19). Kwa hiyo, huyu malaika ambaye mkewe Pilato alimwona katika ndoto yake - atatuthibitishia sisi na watu wote wenye akili timamu, kwa yakini, kwamba Mwenyezi Mungu hakukusudia kuwa

Yesu afe msalabani. Tangu ile siku ya kuumbwa kwa ulimwengu huu, haijatokea kwamba Mwenyezi Mungu apenyeze habari katika moyo wa mtu kwa njia ya ndoto kwamba jambo fulani litatokea kwa njia fulani, kisha jambo hilo lisitokee. Kwa mfano, Injili ya Mathayo inasema kwamba malaika wa bwana alimjia Yusufu katika ndoto na kusema, "Ondoka na umchukue mtoto pamoja na mama yake na mkimbilie Misri, na mkae huko mpaka nikuambie." Kwani Herod anamtafuta huyo mtoto ili amwue." Mathayo 2:13). Sasa, kuna mtu ye yote awezaye kusema kwamba Yesu angeweza kuuawa nchini Misri? Kadhalika ile ndoto ambayo mkewe Pilato aliiota ilikuwa ni sehemu ya mipango ya Mwenyezi Mungu, na kamwe haiwezi kuwa kwamba mpango huu ushindwe kufikia shabaha yake; na kama vile ambavyo uwezekano wa Yesu kufa akiwa safarini nchini Misri ungekuwa kinyume na ahadi maalum ya Mwanyezi Mungu, kwa hiyo hapo napo, ni jambo lisiloingia akilini kwamba malaika wa Mwenyezi Mungu Mwenye nguvu amtokee mkewe Pilato na kumwelekeza aseme kwamba iwapo Yesu atakufa juu ya msalaba halitakuwa jambo zuri kwake, lakini kutokea huku kwa malaika kuwe hakuna maana na kwamba Yesu aachiliwe kufa juu ya MSALABA. Je, kuna mfano wo wote wa namna hiyo ulimwenguni? Hakuna. Dhamiri safi ya watu wote wema, itakapojulishwa kuhusu ndoto ya mkewe Pilato, bila shaka itashuhudia kwamba ni jambo la kweli kwamba shabaha ya ndoto ile ilikuwa kuweka misingi ya kumwokoa Yesu. Naam, ni hiyari ya mtu kuukana hata ukweli ulio wazi kutokana na husuda itokanayo na imani ya mtu; anaweza kuukataa, lakini uadilifu utatulazimisha kuamini ndoto ya mkewe Pilato kuwa ni sehemu ya ushahidi mzito wa Yesu kuepukana na msalaba. Na Injili ya kwanza kwa daraja mionganoni mwa hizi, yaani Injili ya Mathayo imeuhifadhi ushahidi huu. Kwa hiyo, ingawa ushahidi madhubuti nitakaouratibu katika kitabu hiki unafutilia mbali uungu wa Yesu na itikadi ya kafara, hata hivyo uaminifu na kupenda haki vinatutaka tusiwe wenye kupendelea imani ya kijamii au ya kijadi katika suala la ukweli. Toka siku ya kuumbwa kwa binadamu hadi leo akili fupi ya binadamu imewekeza maelfu ya vitu katika

uungu na Umungu, kwa kiasi hiki kwamba hata paka na nyoka wameabudiwa; hata hivyo watu wenye hekima, kwa msaada wa kimbingu wameendelea kuokolewa na imani za kishirikina kama hizo.

Na mionganoni mwa ushahidi wa Biblia wenye kuunga mkono kuepushwa kwa Yesu na kifo juu ya msalaba ni safari yake ya kwenda mahali pa mbali ambayo alianza baada ya kutoka nje ya kaburi.

Mnamo asubuhi ya Jumapili kwanza alikutana na Maria Magdalena ambaye mara moja aliwajulisha wale wanafunzi kwamba Yesu alikuwa hai, lakini hawakuamini. Kisha alionekana kwa wawili mionganoni mwa wale wanafunzi walipokuwa wanakwenda nje ya mji, na mwishoni akajitokeza kwa wale kumi na mmoja waliokuwa wakila chakula na akawalaumu kwa ugumu wao na utovu wa imani (Mathayo 16:9 - 14), na wanafunzi wa Yesu walipokuwa wanakwenda kuelekea kwenye makazi yaitwayo Emmau ambayo yalikuwa umbali wa maili $3\frac{3}{4}$ kutoka Yerusalem Yesu akakutana nao: na walipoyakaribia makazi yale, Yesu akatangulia ili kutengana nao, lakini hawakumruhusu kwenda zake, wakisema kwamba usiku ule watakuwa pamoja. Kisha akala nao chakula, na wote hao pamoja na Yesu walilala kwenye kijiji kiitwacho Emmau (Luka 24:13-31). Sasa, kusema kwamba Yesu alifanya yote hayo akiwa na mwili wa kiroho (ambayo ndiyo hali inayotakiwa kuwa ya mwili baada ya kifo), ambayo yaliwezekana kufanywa na mwili wa kidunia tu, - kama kwa mfano kula, kunywa na kulala na kutembea safari ndefu ya kwenda Galilaya ambao ulikuwa kwenye umbali wa maili sabini kutoka Yerusalem ni kusema jambo lisilowezekana na lililo kinyume cha akili. Na, licha ya ukweli kwamba kutokana na upendeleo wa kibinaksi taarifa za Injili zimehitilafiana, hata hivyo, karina zake kama zilivyo zinaonyesha waziwazi kwamba Yesu alikutana na wanafunzi wake akiwa na mwili wa kawaida wa kibinadamu uwezao kufa, na kusafiri safari ndefu ya kwenda Galilaya kwa miguu; alionyesha vidonda vyake kwa wale wanafunzi, alikula nao chakula cha usiku na akalala pamoja nao. Hivi punde nitathibitisha

kwamba alitumia marhamu kwa ajili ya vidonda vyake.

Sasa, hapa mtu anatakiwa afikirie iwapo, baada ya kujipatia mwili wa kiroho wenyewe kudumu milele, yaani, baada ya kupata ule mwili usiokufa ambao ulimwepusha na ulazima wa kula na kunywa, kukaa mkono wa kulia wa Mwenyezi Mungu na kuepukana na vidonda vya aina yo yote, na maumivu, na udhaifu wa kila aina, bado ulikuwa na kasoro moja, ingawa ulikuwa na sifa za utukufu wa Mwenyezi Mungu wa Milele na wa Tangu na Tangu; - na udhaifu huo ni huu ya kwamba mwili wake ulikuwa na vidonda vipyta vya msalaba na misumari, ambavyo vilikuwa vikitoa damu na vilikuwa vichungu sana na ambavyo vilitayarishiwa marhamu, na hata baada ya kupata mwili wenyewe utukufu na usiokufa, mzima wa milele, usio kasoro, mkamilifu, na usiobadilika, mwili huo huo ukaendelea kupatikana na kasoro za aina nyingi; Yesu mwenyewe aliwaonyesha wanafunzi wake nyama na mifupa ya mwili wake, na tena si hilo tu, bali yalikuwako pia mapigo ya njaa na kiu - vitu vya lazima vya mwili wenyewe kufa, vinginevyo palikuwa na haja gani kwake wakati wa safari ya kwenda Galilaya, kufanya vitu visivyokuwa na faida kama vile kula na kunywa maji, kupumzika na kulala? Hapana shaka, katika ulimwengu huu, njaa na kiu ni vitu vyenye kuutia uchungu mwili wenyewe kufa ambapo huweza kuleta kifo iwapo njaa na kiu hiyo ni kali. Kwa hiyo hakuna shaka kwamba Yesu hakufa juu ya msalaba, wala hakupata mwili mpya wa kiroho; bali alikuwa katika hali ya kuzimia inayofanana na kifo. Na, kwa rehema ya Mwenyezi Mungu ikatokea kwamba lile kaburi alimowekwa halikuwa kama makaburi ya nchi hii; kilikuwa chumba chenye kuingiza hewa. Na katika siku zile ilikuwa desturi ya Wayahudi kulifanya kaburi liwe na hewa kama nyumba yenye nafasi kwa kuliwekea mlango. Makaburi ya namna hiyo yalitayarishwa mapema; na maiti ziliingizwa humo kulingana na hali iliyosababishwa na tukio. Injili zinatoa ushahidi ulio wazi kuhusu jambo hili: Luka anasema; "Hata ilipoingia siku ya kwanza ya wiki, mapema sana asubuhi, (yaani ilipokuwa bado kuna giza - giza) hao (yaani wale wanawake) walikwenda kaburini wakipeleka viungo vya manukato pamoja na vitu vingine

walivyokuwa wametayarisha. Na wakakuta lile jiwe limebirgingishwa kando ya kaburi (hebu fikiria jambo hili!) na wakaingia ndani lakini hawakuukuta mwili wa Bwana Yesu. (Luka 24:13-31) Hebu yatafakari kwa muda maneno haya; "wakaingia ndani." Ni dhahiri kwamba mtu anaweza tu kuliingia kaburi ambalo linafana na chumba na lina mlango. Nitaeleza ndani ya kitabu hiki, patakapofikia mahali pake maalumu, kwamba kaburi la Yesu (amani juu yake) lililogunduliwa hivi karibuni mjini Srinigar, Kashmir, lina mlango na dirisha kama kaburi hili. Hii ni dalili yetu ambayo

kama itafikiriwa kwa makini itawaongoza wachunguzi wa jambo hili kwenye uamuzi mkubwa na wa muhimu sana.

Na mionganoni mwa ushahidi wa Injili ni maneno ya Pilato yaliyorkodiwa na Mtakatifu Marko: "Hata ilipokwisha fikia kuwa jioni, kwa sababu ni maandalio, ndiyo siku iliyokabura ya Sabato, akaenda Yusufu, mtu wa Arimathaya, Mstahiki, mtu wa baraza ya mashauri, naye mwenyewe anautazamia ufalme wa Mungu, akafanya ujasiri, akaingia mbele ya Pilato, akauomba mwili wake Yesu. Lakini Pilato akastaajabu iwapo tayari alikuwa amekwisha kufa. (Marko 15:42 - 44). Hii inaonyesha kwamba katika kile kipindi cha wakati wa kusulubiwa wenyewe kulikuwa na shaka iwapo Yesu alikuwa amekufa kweli, na shaka hiyo haikutoka kwa mtu mwingine isipokuwa yule aliyejua kutokana na uzoefu, kuwa ni muda gani ilimchukua mtu kufa juu ya msalaba.

Na mionganoni mwa ushahidi wa Injili ni hii aya, "Basi Wayahudi kwa sababu ni Maandalio, miili isikae juu ya misalaba siku ya sabato, (maana ile Sabato ilikuwa siku kubwa) walimwomba Pilato miguu yao ivunjwe wakaondolewe. Basi askari wakaenda, wakamvunja miguu wa kwanza, na wa pili aliyesulubiwa pamoja naye. Lakini walipomjia Yesu na kuona ya kuwa amekwisha kufa, hawakumvunja miguu; lakini askari mmojawapo alimchoma mkuki ubavuni; na mara ikatoka damu na maji." (Marko 15:42-44). Aya hizi zinaonyesha wazi wazi kwamba ili kuutoa kabisa uhai wa mtu aliyesulubiwa ilikuwa ni desturi katika siku zile kumweka mtu huyo juu ya msalaba kwa siku chache, halafu kuivunja miguu

yake, lakini miguu ya Yesu haikuvunjwa kwa makusudi, na aliteremshwa msalabani akiwa hai kama wale wezi wawili. Hiyo ndio sababu damu ilitoka wakati ubavu wake ulipochomwa. Lakini damu huganda baada ya kifo. Na hapa, inaelekea pia kwamba yote hayo yalikuwa matokeo ya mpango maalumu. Pilato alikuwa mtu mwenye kumwogopa Mwenyezi Mungu na alikuwa mtu mwenye roho nzuri; asingeweza kuonyesha upendeleo bayana kwa kumuogopa Kaisari; kwani Mayahudi walikwisha mtangaza Yesu kuwa ni mwasi. Haidhuru Pilato alikuwa na bahati ya kumwona Yesu lakini Kaisari hakuwa na bahati hiyo.

Huyu Pilato si tu alimwona Yesu bali pia alimfanyia upendeleo mkubwa - hakutaka Yesu asulubiwe. Injili zinaonyesha waziwazi kwamba mara kadhaa Pilato alitaka kumwachia huru, lakini Mayahudi walisema kwamba kama angemwachia huru hangkuwa mtiifu kwa Kaisari; walisema pia kwamba Yesu alikuwa mwasi aliyetaka kuwa mfalme. (Yohana 19:31-34). Na ile ndoto ambayo mkewe Pilato aliona ilitia msukumo zaidi wa kumwachia huru Yesu; vinginevyo Pilato na mkewe wangejitia katika maangamizo. Lakini kwa kuwa Mayahudi walikuwa watu wakorofii waliokuwa tayari hata kumjulisha Kaisari kwa siri kuhusu kitendo cha Pilato, hivyo Pilato alitumia hekima ya kumwokoa Yesu: Kwanza aliiipanga Ijumaa kuwa siku ya kumsulubisha, masaa machache tu kabla ya kuzama kwa jua, na usiku wa sabato iliyo kubwa ulikuwa unakaribia kuingia. Na Pilato alijua vizuri sana kwamba kulingana na amri za sheria zao Mayahudi wangeweza kumbakiza Yesu msalabani hadi jioni tu, na baada ya hapo ilikuwa kinyume cha sheria kumbakiza mtu ye yote juu ya msalaba. Basi ikatokea vivyo hivyo; na Yesu akateremshwa msalabani kabla ya magharibi. Na haiyumkiniki kwamba wale wezi waliosulubiwa wakati mmoja na Yesu wawe wamebakia hai, lakini Yesu awe amekufa katika kipindi cha masaa mawili tu. Hicho kilikuwa kisingizio kilichobuniwa ili kumwokoa Yesu na utaratibu wa kuvunja miguu. Huu ukweli kwamba wezi wote wawili waliteremshwa msalabani wakiwa hai ni ushahidi wa kutosha kwa mtu mwenye akili; na kuwateremsha msalabani wahusika

wakiwa hai ndio iliyokuwa desturi ya kawaida ya wakati ule; walikufa pale tu mifupa yao ilipovunjwa au walipofanywa kubakia juu ya msalaba bila chakula au maji kwa siku kadhaa. Lakini Yesu hakukabiliwa na tajriba zo zote za namna hii - yeye hakubakia msalabani kwa siku kadhaa wala mifupa yake haikuvunjwa; na kwa kufanya ioneokane kana kwamba alikwisha kufa, Mayahudi walifanywa walisahau jambo lote. Lakini mifupa ya wale wezi ilivunjwa na waliuawa mara moja. Lingalikuwa jambo tofauti kama ingesemwa kumhusu mmoja wa wale wezi kwamba naye pia alikuwa amekufa na kwamba hapakuwa na haja ya kuvunja mifupa yake. Na mtu mmoja aitwae Yusufu rafiki mheshimiwa wa Pilato na mtu mashuhuri katika kitongoji kile na mwanafunzi wa kisirisi wa Yesu - alijitokeza katika wakati unaofaa. Ninahisi kwamba yeye pia aliitwa kutokana na ushauri wa Pilato. Yesu kwa kudhaniwa kwamba alikuwa amekufa, mwili wake ulikabidhiwa kwake, kwa kuwa alikuwa mtu mkubwa ambaye Mayahudi wasingeweza kugombana naye. Alipofika mahali pa tukio alimchukua Yesu aliyekuwa katika hali ya kuzimia tu, kana kwamba alikuwa maiti. Na jirani ya mahali pa tukio palikuwa na nyumba yenye nafasi kubwa ilijoengwa kama kaburi kulingana na desturi za wakati ule, yenye mlango na ambayo ilijengwa mahali ambapo Mayahudi hawakuwa na shughuli napo. Yesu aliwekwa kwenye nyumba hii kwa ushauri wa Pilato. Matukio haya yalitokea katika karne ya kumi na nne baada ya kifo cha Musa; na Yesu alikuwa Mujaddid (Mhuishaji) wa sheria ya Kiisraeli katika karne ya kumi na nne. Na ingawa Mayahudi walikuwa wakimtazamia Masihi Aliyahidiwa katika karne hii hii ya kumi na nne, na tabiri za manabii waliopita pia ziliashiria kwenye wakati huu-huu kwa kutokea kwake, lakini loo! Makuhani wa Kiyahudi wasiokuwa na maana hawakuutambua wakati huu na msimu huu, na wakamkamata Masihi Aliyahidiwa kwa kumdhania kuwa ni muongo. Si hivyo tu bali walimtangaza kuwa ni kafir, wakamwita si muumini, wakatamka hukumu ya kifo dhidi yake na wakamkokota hadi mahakamani.

Hii inaonyesha kwamba katika karne ya kumi na nne

Mwenyezi Mungu alizikusanya zile tashwishi zote zilizofanya mioyo ya watu kuwa migumu, makuhani kuwa watu wa kidunia, vipofu na maadui wa haki. Hata hivyo, malinganisho kati ya karne ya kumi na nne baada ya Musa na karne ya kumi na nne baada ya "mfano" wa Musa - Mtume wetu Mtukufu s.a.w. yataonyesha, awali ya yote, kwamba katika kila mojawapo ya karne hizi kulikuwako na na mtu aliyedai kuwa Masihi Aliyahidiwa; dai la kweli likiwa linategemea mamlaka ya Mwenyezi Mungu. Kisha, inaonekana pia kwamba makuhani wa watu waliwatangaza wote hao wawili kuwa ni makafiri, na kuwaita wasioamini na Madajjali, na kutoa fatwa ya kifo dhidi yao, na kuwakokotea mahakamani - mahakama ya Kirumi kwa kesi moja na ya Kiingereza kwa kesi nyingine. Hatimae, wote waliokolewa; na hao makuhani - Mayahudi na Waislamu - walishindwa katika hila zao. Mwenyezi Mungu alikuwa Amekusudia kuanzilisha jumuiya zilizo kubwa kwa Masihi wote wawili na kuzishinda hila za maadui zao. Kwa kifupi, karne ya kumi na nne baada ya Musa na karne ya kumi na nne baada ya Mtume wetu mtukufu Muhammad s.a.w. ni za majaribu makubwa kwa Masihi wake wahusika - na pia ni zenye baraka nyingi kadiri muda unavyopita.

Na mionganoni mwa ushahidi unaoonyesha kwamba Yesu a.s. aliokolewa Msalabani ni ule uliosimuliwa na Mathayo katika sura ya 26 aya ya 36 hadi 46 ambazo zinaeleza kwamba baada ya kupewa habari kwa njia ya ufunuo kuhusu kutiwa mbaroni kulikokuwa kunamsubiri, Yesu alimwomba Mwenyezi Mungu usiku kucha, akisujudu na kutokwa na machozi, na maombi yaliyofanywa kwa unyenyekevu wa namna hiyo, na ambayo Yesu alikuwa na muda wa kutosha wa kuyaomba, hayawezi kuwa yalipita bila kupokelewa; kwani kilio cha mteule wa Mwenyezi Mungu kinachotolewa wakati wa dhiki kamwe hakikataliwi. Ilikuwaje sasa, kwamba maombi ya Yesu aliyoomba usiku kucha akiwa na moyo uliojawa na uchungu na akiwa katika hali ya dhiki yakataliwe? Iliali Yesu alisema; Baba aliye mbinguni ananisikiliza. Kwa hiyo, iwapo maombi yake aliyoomba katika hali ya dhiki kama ile hayakuweza kusikilizwa, inawezaje kusemwa

kwamba Mwenyezi Mungu Anasikiliza maombi? Injili zinaonyesha pia kwamba Yesu a.s. alikuwa na yakini ya kutoka moyoni kwamba maombi yake yalikubaliwa; alikuwa na matumaini makubwa katika maombi yale. Hii ndiyo sababu alipokamatwa na kuwekwa msalabani, na alipoona kwamba mazingira yale hayakuwa sawa na matarajio yake, akashindwa kujuzuia kulia kwa kusema "Eloi, Eloi lama sabachtani", ikimaanisha, "Mungu wangu, Mungu wangu, mbona Umeniacha?" Yaani hakutazamia kwamba angekuja kuwa namna hii - kwamba angekuja juu ya Msalaba. Aliamini kwamba maombi yake yangesikilizwa. Kwa hiyo, rejea zote hizi mbili za Injili zinaonyesha kwamba Yesu aliamini kwa dhati kuwa maombi yake yangesikilizwa na kukubaliwa, kwamba maombi yake aliyoyaomba usiku kucha kwa kutokwa na machozi yasingepotea bure, wakati yeye mwenyewe aliwafundisha wanafunzi kwa maelezo kutoka mbinguni: "Mtakapoomba, maombi yenu yatapokelewa." Isitoshe, alisimulia pia fumbo la hakimu ambaye hakumwogopa mtu wala Mungu. Na shabaha ya fumbo hili ilikuwa kwamba wale wanafunzi watambue kuwa bila shaka Mwenyezi Mungu Hypokea maombi. Na ingawa Yesu alijua kutoka kwa Mungu kwamba kulikuwako na mateso makubwa yaliyokuwa yakimsibiri, hata hivyo, kama walivyo watu wote walio wacha-Mungu, alimwomba Mwenyezi Mungu akiamini kwamba hapakuwepo na jambo lisilowezekana kwa Mwenyezi Mungu na kwamba Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye kukadiria iwapo tukio fulani litokee au la. Kwa hiyo, kukataliwa kwa maombi ya Yesu mwenyewe kungeitikisa imani ya wale wanafunzi. Je ingewezekana kuweka mbele ya wanafunzi mfano wenye kubomoa imani zao? Kama wangeliona kwa macho yao wenyewe kwamba maombi ya nabii mkubwa kama Yesu, yaliyoombwa usiku kucha kwa bidii kubwa ya moyo, hayakukubaliwa, mfano huo wenye bahati mbaya ungeleta majoribu makubwa katika imani zao. Kwa hiyo, Mwenyezi Mungu aliye mwangi wa rehema Asingeefanya jambo lingine isipokuwa kuyakubali maombi haya. Ni jambo la yakini kwamba yale maombi yaliyoombwa mahali paitwapo Gethsemane yalipokelewa.

Kuna kitu kingine kuhusiana na jambo hili. Kama vile ilivyokuwepo njama ya kumwua Yesu, na kwa ajili hiyo makuhani na waandishi waliitisha mkuano wa pamoja nyumbani kwa kuhani mkuu aitwae Caiaphas ili kutengeneza mpango wa kumwua Yesu, kadhalika iliwahi kuwepo njama ya kumwua Musa, na vivyo hivyo, kulikuwa na ushauri wa kisiri-siri mjini Makka mahali paitwapo Daarun-Nadwa ili kumwua Mtume wetu Mtukufu s.a.w. Lakini Mwenyezi Mungu Mwenye nguvu aliwaokoa Mitume hawa wakubwa na hila hizo mbaya. Kiwakati, njama dhidi ya Yesu ilikuwa katikati ya hawa wengine wawili. Sasa kwa nini Yesu hakuokolewa ilhali ye ye aliomba kwa nguvu zaidi kuliko ye yote mionganoni mwa hao wawili? Kwa nini maombi ya Yesu yaliachwa kusikilizwa ilhali Mwenyezi Mungu husikiliza maombi ya watumishi wake wapendwa na kuharibu hila za waovu? Watu wote walio wacha-Mungu wanajua kutokana na uzoefu kwamba maombi ya wenye dhiki na wenye kuteswa hypokelewa; la, bali saa ya mateso kwa mtu aliye mcha-Mungu ni saa ya ishara. Mimi mwenyewe nimewahi kuwa na uzoefu wa jambo hili. Shitaka la uwongo la jaribio la kuuwa lilifunguliwa dhidi yangu miaka miwili iliypita na mtu mmoja aitwae Dakta Martin Clark, Mkristo aishiye mjini Amritsar katika Punjab mbele ya mahakama katika Wilaya ya Gurdaspur akidai kwamba nilimtuma mtu mmoja itwaye Abdul Hamid, ili kumwua daktari huyo. Ikatokea kwamba katika kesi hii nilipangiwa na watu wachache wenye hila waliotokana na Jumuiya tatu, yaani Wakristo, Wahindu na Waislamu; waliungana na walijaribu kadiri walivyoweza ili kuthibitisha shitaka la jaribio la kuuwa dhidi yangu. Wakristo walikuwa na manung'uniko dhidi yangu kwamba nilikuwa najaribu - na naendelea kujaribu hata sasa - kuwaokoa watu kutoka katika fikara potofu ambazo Wakristo wanazikaribisha kumhusu Yesu; na huu ndio ulikuwa muonjo wa kwanza wa kile nilichotendewa na watu hao. Wahindu walikasirishwa nami kwa sababu nilitoa utabiri kuhusu kifo cha mtu mmoja aitwaye Lekh Ram, Mwanazuoni wa Kihindu, kwa ruhusa yake mwenyewe, na utabiri huo ukatimia katika kipindi cha wakati uliopangwa - Ishara ya kutisha kutoka kwa Mwenyezi

Mungu. Kadhalika Masheikh wa Kiislamu walikasirika kwa sababu nilipinga wazo la kuwepo kwa Masihi mwenye kumwaga damu na ile itikadi ya Jihadi kama inavyoelweka na hao. Kwa hiyo, baadhi ya watu mashuhuri wa jumuiya hizi tatu walishauriana kwa pamoja kwa nia ya kuthibitisha lile shitaka la mauaji dhidi yangu ili imma ninyongwe au nitiwe gerezani. Kwa hiyo hao walikuwa watu wadhalimu mbele ya Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu Alinijulisha mimi kuhusu jambo hili kabla ya ile saa ya mashauriano yao ya siri. Alinipa habari njema za kuachiliwa kwangu hapo mwishowe. Funuo hizi safi kutoka kwa Mwenyezi Mungu zilitangazwa mapema kwa maelfu ya watu; na wakati baada ya ufunuo huu nilipoomba: Mola! niokoe mimi na mateso haya, ikafunuliwa kwangu kwamba Mwenyezi Mungu Ataniokoa na Ataniondolea mashitaka yaliyofunguliwa dhidi yangu. Ufunuo huu ulielezwa kwa njia ya mdomo kwa zaidi ya watu mia tatu ambao wengi wao bado wangali hai. Na ikatokea kwamba maadui zangu walileta mashahidi wa uwongo mahakamani, na ilibakia kidogo tu wathibitishe shitaka hilo - mashahidi wa hizo Jumuiya tatu zilizotajwa hapo kabla wakiwa wanatoa ushahidi dhidi yangu. Kisha, ikatokea kwamba habari za kweli kuhusu kesi ile zikabainishwa kwa njia mbalimbali na Mwenyezi Mungu kwa yule hakimu aliyekuwa akiisikiliza kesi ile ambaye jina lake lilikuwa Kapteni W. Douglas, Naibu Kamishna wa Gurdaspur. Aliridhika kwamba kesi ile ilikuwa ya uwongo. Kisha, bila kumjali huyo dakta ambaye pia alikuwa m-misionari, muono wake wa haki ulimshawishi kuifutilia mbali ile kesi, na hivyo basi yote yale ambayo niliyatangaza kuhusu kuachiliwa kwangu, kwa maelekezo ya ufunuo kutoka kwa Mwenyezi Mungu, kwa mamia ya watu, na kwenye mikutano ya hadhara, yakatokea kuwa kweli ambayo ilisaidia kuimarisha imani ya watu wengi, ijapokuwa mazingira yaliyokuwapo kabla yaliashiria welekeea wa hatari. Si haya tu, tuhuma nyangi za namna hii na mashitaka yenye sura ya jinai yalipendekezwa dhidi yangu kutokana na sababu zilizotajwa hapo juu, na kesi zikapelekwa mahakamani, lakini kabla sijaitwa mahakamani Mwenyezi Mungu alinijulisha mwanzo na mwisho

wa jambo lote na katika kila kesi ya hatari nilipewa habari njema za kuachiliwa.

Suala la msingi hapa ni kwamba bila shaka Mwenyezi Mungu Mwenye nguvu Huyapokea maombi hususan wakati watumishi Wake waaminifu wanapokwenda mlangoni pake wakiwa wameonewa; Hushughulikia utetezi wao na huwasaidia kwa njia za ajabu. Kuhusu hili mimi mwenyewe ni shahidi. Kwa nini basi yale maombi ya Yesu aliyyoatoa akiwa katika hali ya uchungu mkuu kama ule yawe hayakupokelewa? Hapani, yalipokelewa, na Mwenyezi Mungu Alimwokoa. Mwenyezi Mungu Alitengeneza mazingira ardhini na mbinguni ili kumwokoa. Yohana, yaani nabii Yahya hakuwahi kupata muda wa kuomba kwa sababu mwisho wake ulikuwa umekwisha wadia, lakini Yesu alikuwa na usiku mzima wa kufanya maombi, na akautumia usiku wote huo kwa kufanya maombi akiwa amesimama na kusujudu mbele ya Mwenyezi Mungu, kwani Mwenyezi Mungu Alikusudia kwamba Yesu aonyeshe dhiki aliyokuwa nayo na aombe kuachiliwa kwake kwa Mwenyezi Mungu Ambaye kwake hakuna lisilowezekana. Kwa hiyo Mola, kulingana na desturi Yake ya tangu na tangu, Aliyapokea maombi yake. Mayahudi walisema uwongo pale ambapo walipokuwa wakimsulubu Yesu walimsuta kwamba yeze alimtegemea Mwenyezi Mungu; kwa nini Mwenyezi Mungu Hakumwokoa? Kwa hiyo Mwenyezi Mungu Alibatilisha hila zote za Mayahudi na kumwokoa Masihii Wake mpendwa kutokana na msalaba na laana inayoambatana na msalaba huo. Mayahudi walishindwa.

Na mionganoni mwa ushahidi wa Injili uliotufikia ni aya kutoka Mathayo: "Kwamba ije juu yenu damu yote ya haki iliyomwagika juu ya nchi, tangu damu ya Habili, yule mwenye haki, hata damu ya Zakaria bin Barakia, mliyemwua kati ya patakatifu na madhabahu. Amin, nawaambieni, mambo hayo yote yatakuja juu ya kizazi hiki (Mathayo 23:35-36). Sasa, iwapo mtazitafakari aya hizi mtagundua kwamba Yesu a.s. anasema waziwazi kwamba kuuawa kwa manabii kulikokuwa kunafanywa na Mayahudi kuliishia kwa nabii Zakaria, na kwamba baada ya hapo Mayahudi

wasingekuwa na uwezo wa kumwua nabii ye yote. Huu ni utabiri mkubwa ambao unaonyesha kwamba Yesu a.s. hakuuawa kutokana na kuwekwa msalabani; bali aliokolewa kutoka msalabani, na hatimae akafa kifo cha kawaida. Kwani kama Yesu a.s. angepata kifo cha kuuawa na Mayahudi kama Zakaria, angeashiria hivyo katika aya hizi kuhusu kifo chake yeye mwenyewe. Na kama itadaiwa kwamba Yesu a.s. pia aliuawa na Mayahudi lakini kuuawa kwake hakukuwapatia dhambi Mayahudi kwani kifo cha Yesu kilikuwa katika hali ya kafara, dai hilo ni vigumu kulithibitisha kwani katika Yohana sura 19 aya ya 11 Yesu anasema wazi wazi kwamba Mayahudi walitenda dhambi kubwa kwa kukusudia kumwua Yesu; na kadhalika, katika sehemu zingine nyingi kuna kidokezo kilicho wazi kwamba walistahili adhabu mbele ya Mwenyezi Mungu kama malipo ya uovu waliomtendea Yesu (Mathayo 23:35 - 36).

Na mionganoni mwa ushahidi wa Injili uliotufikia ni aya ya Mathayo, yaani "Amin, nawaambieni, pana watu katika hawa wasimamao hapa, ambao hawataonja mauti kabisa, hata watakapomwona mwana wa Adamu akija katika ufalme wake." (Mathayo 26:24). Kadhalika ile aya katika Yohana: "Yesu akamwambia: Ikiwa nataka huyu (yaani mwanafunzi, Yohana) abakie (yaani mjini Yerusalem) hata nijapo." (Mathayo 16:28). Hii ina maana: Kama nikitaka, Yohana hatakuwa mpaka nije tena. Aya hizi zinaonyesha kwa uwazi mkubwa kwamba Yesu a.s. alitoa ahadi kwamba baadhi ya watu wataendelea kuishi mpaka atakaporudi. Mionganoni mwa hao alimtaja Yohana. Kwa hiyo ilikuwa lazima ahadi hii itimie. Hivyo basi, hata Wakristo wamekiri kwamba ili utabiri huo uhesabiwe kuwa umetimilizwa ni lazima kuja kwa Yesu kutokee katika wakati ambapo baadhi ya watu wa zama zile watakuwa bado hai, ili utabiri huo utimilizwe kulingana na ahadi. Huu ndio msingi wa tangazo la viongozi wa kanisa kwamba kulingana na ahadi yake Yesu alikuja Yerusalem wakati wa kuteketezwa kwake na kwamba Yohana alimwona, kwa vile aikuwa hai wakati ule. Lakini ni lazima itambuliwe kwamba Wakristo hawasemi kwamba Yesu aliteremka kidhahiri kutoka

mbinguni akifuatana na Ishara zilizoahidiwa; bali wanasesma kwamba alijitokeza kwa Yohana kama katika kashfu ili aweze kutimiliza utabbiri wake uliomo katika aya ya 38 ya sura ya 16 ya Mathayo. Lakini mimi nasema kwamba kuja kwa namna hii hakutimilizi utabiri ule. Hiyo ni tafsiri dhaifu sana ambayo inakwepa kwa taabu lawama zitolewazo dhidi ya msimamo huu. Na tafsiri hii ni dhahiri kabisa kwamba haiwezi kuthibitishwa na ni ya makosa, kwa kiasi hiki kwamba hakuna haja ya kuikanusha, kwani kama Yesu ilikuwa atokee kwa mtu ye yote kwa njia ya ndoto au kashfu utabiri wa namna hiyo ungekuwa kichekesho (Mathayo 26:24)¹. Yesu alijitokeza kwa Paulo pia kwa namna hiyo hiyo muda mrefu kabla ya tukio hili. Inaelekea kwamba utabiri uliomo katika aya ya 38 ya sura ya 16 ya Mathayo umewatia kiwewe mapadri na wamekuwa bado hawajaweza kupata maana inayokubalika akilini kulingana na imani zao wenyewe, kwani ni vigumu kwao kusema kwamba Yesu wakati wa kutekwa kwa Yerusalem alishuka kutoka mbinguni akiwa katika hali ya utukufu, na kwamba kama vile radi inavyolimulika anga lote na inaonekana na kila mtu, wote walimwona yeye; na pia haikuwa rahisi kwao kuipuuza ile kauli, yaani: Baadhi ya wale waliokuwa wamesimama hapa hawataonja kifo mpaka wamwone mwana wa Adamu katika Ufalme wake. Kwa hiyo, kutokana na tafsiri iliyotiwa chumvi waliamini kutimilizwa kwa utabiri ule kwa njia ya kashfu. Lakini hii siyo kweli; watumishi wacha-Mungu wa Mwenyezi Mungu hujitokeza kila mara kwa wateule kwa njia ya kashfu, na kwa kupata kashfu si lazima ya kwamba zitokee wakati wa ndoto tu; sivyo, zinaweza kuonekana hata katika hali ya kuwa macho; mimi

1. Nimeona katika vitabu fulani fulani tafsiri za aya ya 24 ya sura 26 (aya ya 38 ya sura 16 - Mfasiri) ya Mathayo zilizotolewa na Masheikh ambazo zimetiwa chumvi zaidi hata kuliko zile za Wakristo: wanasesma kwamba wakati Yesu alipoitangza kuwa ishara ya kuja kwake kwamba baadhi ya watu wa kizazi kile watakuwa bado hai na kwamba mwanafunzi mmoja pia atakuwa bado yu hai wakati wa Masihi atakapotokea, ni lazima kwamba yule mwanafunzi awe ameendelea kuishi hadi sasa kwani Masihi bado hajaja; na wanafikiri kwamba yule mwanafunzi amejificha mahali fulani katika baadhi ya milima akimsubiri Masihi!

mwenyewe nimekwishapata tajriba ya shani kama hizo.

Nimewona Yesu a.s. mara nyingi katika kashfu (ndoto katika hali ya kuwa macho), na nimekutana na baadhi ya mitume nikiwa macho kabisa; pia nimewona Mkuu wetu, Bwana wetu na Kiongozi wetu, Mtume Muhammad s.a.w. mara nyingi katika hali ya kuwa macho na nimeongea naye - katika hali ya kuwa macho wazi wazi kwa kiasi hiki kwamba usingizi au kusinzia havikuhusiana kabisa na hali hiyo. Pia nimekutana na baadhi ya wafu kwenye makaburi yao au sehemu zingine nikiwa macho; na nimeongea nao. Najua vizuri sana kwamba kukutana kwa namna hiyo na wafu katika hali ya kuwa macho ni jambo linalowezekana, siyo tu tunaweza kukutana, tunaweza kuongea pia, na hata kushikana mikono. Hakuna tofauti ya tajriba kati ya hali hii ya kashfu na ile hali ya kuwa macho ya kawaida; mtu anajiona ya kwamba yuko katika ulimwengu huu huu, ana masikio yale yale, macho yale yale na ulimi ule ule, lakini kutafakari kwa kina kutabainisha ulimwengu ulio tofauti. Ulimwengu wetu huu hauna utambuzi kuhusu tajriba ya namna hii, kwani ulimwengu huu unaishi maisha ya kutojali. Tajriba hii ni zawadi kutoka mbinguni; ni ya wale waliopewa vipawa vipyta vyatofauti. Hili ni jambo la hakika - halisi na kweli. Kwa hiyo, wakati Yesu alipojitezea kwa Yohana baada ya kuteketezwa Yerusalem, ingawa alionwa na Yohana katika hali ya kuwa macho, na ingawa yawezekana kulikuwako na mazungumzo kidogo na kushikana mikono, hata hivyo tukio hilo halihusiani kabisa na utabiri ule. Shani za namna hiyo hutokea mara nyingi ulimwenguni; na hata sasa, iwapo nitafunga nia kidogo kuhusu jambo hili, ninaweza kwa rehema ya Mwenyezi Mungu kumwona Yesu au baadhi ya Mitume watakatifu nikiwa katika hali ya kuwa macho. Lakini kukutana kwa namna hiyo hakutimilizi ule utabiri uliomo katika Mathayo:16:38).

Kwa hiyo, kilichotokea hasa ni hiki ya kwamba Yesu alijua kwamba ataokolewa Msalabani na atahamia nchi nyingine na kwamba Mwenyezi Mungu Hatamwachilia afe wala kumwondoa katika ulimwengu huu iwapo atakuwa bado hajaona kuteketezwa

kwa Mayahudi kwa macho yake mwenyewe na kwamba hangekufa wakati ambapo bado yale matunda ya ufalme ambayo watu mashuhuri wa kiroho wamepewa na mbingu hayajapati kana. Yesu alitoa utabiri huu ili awahakikishie wanafunzi kwamba hivi punde wangeona ishara kwamba wale walioinua upanga dhidi yake wangeuawa kwa upanga wakati wa uhai wake na mbele ya macho yake. Kwa hiyo, iwapo ushahidi una thamani yo yote hakuna ushahidi mkubwa kwa Wakristo kuliko huu: kwamba Yesu kwa ulimi wake mwenyewe anatoa utabiri kwamba baadhi yao watakuwa bado wangali hai atakapokuja tena.

Ni lazima itambulike kwamba Injili zina aina mbili ya utabiri kuhusu kuja kwa Yesu: (1) Ahadi ya kuja kwake siku za baadaye; kuja kwake ni kwa sura ya kiroho, na kunafanana na kuja kwa nabii Eliya katika zama za Yesu. Kwa hiyo, kama vile alivyokuwa Eliya, amesha jitokeza tayari katika zama hizi; na ni mimi mwandishi; mtumishi wa watu wote, ambaye nimekuja kama Masihi Aliyahidiwa, kwa jina la Yesu a.s. na Yesu alitoa habari za kuja kwangu katika Injili. Amebarikiwa yule ambaye, kwa ajili ya kumheshimu Yesu anatafakari kwa uaminifu na ukweli kuhusu kuja kwangu, na hivyo kujiepusha na kujikwaa. (2) Aina zingine za utabiri kuhusu kuja mara ya pili kwa Yesu zilizotajwa katika Injili kwa hakika zimetajwa kama ushahidi wa uhai ambao kwa rehema ya Mwenyezi Mungu ulibakia pasipo upungufu wakati wa tajriba ya msalaba. Mwenyezi Mungu Alimwokoa mtumishi Wake mashuhuri na kifo cha Msalaba; kama unavyoashiria utabiri uliotajwa hivi punde - Wakristo wamo katika makosa wanapozichanganya karina hizi mbili: Kwa sababu hii wamechanganyikiwa na wanalazimika kukabiliana na shida nyngi. Kwa kifupi, ile aya katika sura ya 16 ya Mathayo ni kipande muhimu sana cha ushahidi unaounga mkono kuepukana kwa Yesu na kifo cha Msalaba.

Na mionganoni mwa ushahidi wa Injili uliotufikia ni aya ifuatayo ya Mathayo: "Ndipo itakapoonekana ishara ya Mwana wa Adamu mbinguni; ndio mataifa yote ya ulimwengu yatakapoomboleza, nao watamwona mwana wa Adamu akija juu ya mawingu ya

mbinguni pamoja na nguvu na utukufu mwingi. (Tazama Mathayo, sura ya 24 aya ya 30). Maana ya aya hii ni: Yesu (amani juu yake) anasema kwamba wakati utafika ambapo kutoka mbinguni, yaani kutokana na uwezo wa kimbingu wa kuingilia kati zitazuka elimu, hoja na ushahidi ambaao utabatilisha imani za uungu wa Yesu, kifo chake juu ya msalaba na kupaa kwake mbinguni na kuja tena; na kwamba mbingu itashuhudia dhidi ya uwongo wa wale waliomkana yeye kuwa nabii wa kweli, kwa mfano Mayahudi; na wale wa upande mwingine waliomhesabu yeye kuwa mtu aliyelaaniwa kwa sababu ya kusulubiwa kwake, kwani ukweli wa kutopatikana kwake na kifo juu ya Msalaba na kwa hiyo kutokuwa mlaaniwa kungebainishwa wazi wazi; kwamba kisha mataifa yote ya dunia ambaao walitia chumvi na kupunguza sehemu ya hadhi ya kweli wangeaibishwa sana na kosa lao; kwamba, katika zama zile zile ambapo ukweli huu ungebainishwa watu wangeona kuteremka kwa Yesu duniani kimethali, yaani katika siku zile zile Masihi Aliyahidiwa angekuja katika uwezo wa sifa za Yesu, angejitokeza kwa ishara zote za kung'ara na msaada wa kimbingu na kwa uwezo na utukufu ambaao ungetambulika. Aya hii - kwa kuelezwa zaidi - ina maana kwamba kudra ya Mwenyezi Mungu imeitengeza nafsi ya Yesu na kuyapanga matukio ya maisha yake ili kuwafanya baadhi ya watu kutia chumvi, na wengine kupunguza hadhi yake, yaani wako watu ambaao wanamtoa katika jamii ya binadamu kwa kiasi hiki kwamba wanasema kuwa bado hajafa na amekaa mbinguni akiwa hai. Na watu ambaao wamewapita hawa ni wale wasemao kwamba, baada ya kufa Msalabani na kufufuka amekwenda juu mbinguni na amepewa uwezo wote wa kiungu, la bali yeye ndiye mungu mwenyewe. Na watu wengine ni Mayahudi ambaao wanasema kwamba aliuawa msalabani na kwa hiyo (najikinga kwa Mwenyezi Mungu kwa kusema hivyo) amelaaniwa milele; amehukumiwa kuwa mlengwa wa hasira ya kudumu; Mwenyezi Mungu Hapendezwi naye na Anamwona kama adui mwenye kuchukiwa; kwamba ni mwongo na mdanganyifu - na Mungu apishe mbali - ni kaafir, msikuamini mkubwa; kwamba hakutoka kwa Mwenyezi Mungu. Kutia chumvi

huku na kupunguza kulikuwa kwa dhuluma kubwa kiasi hiki kwamba isinge kuwa isipokuwa kwamba Mwenyezi Mungu Amsafishe Mtume Wake wa kweli na tuhuma hizi. Aya ya Injili iliyotajwa hapo kabla inaashiria kwenye ukweli huu. Ile kauli kwamba mataifa yote ya dunia yataomboleza inaleta fikra kwamba mataifa yote yale ambayo ainisho la neno "taifa" linahusika nayo, yataomboleza katika siku ile; watapiga vifua vyao na kulia, na kuomboleza kwao kutakuwa kukubwa. Hapa Wakristo ni lazima waifuate aya inayohusika kwa uzingativu; ni lazima wafikirie kwamba wakati ambapo aya hii inao utabiri kwamba mataifa yote yatapiga vifua vyao, imekuwaje wao wasihusike na maombolezo haya? Je hao sio taifa? Wakati, kulingana na aya hii hao wamejumuishwa mionganoni mwa wale amba ni wapigaji wa vifua, kwa nini hawashughulikii uwokovu wao? Aya hii inasema wazi wazi kwamba ishara ya Yesu itakapotokea mbinguni mataifa yote yakaayo ardhini yataomboleza. Kwa hiyo yule mtu anayesema kwamba taifa lake halitaomboleza anamkana Yesu. Lakini wale watu, amba idadi yao bado ni ndogo hawawezi kuwa watu waliodokezwa katika utabiri huu; hawajafikia sifa ya kuainishwa kama "taifa", na watu au taifa lile ndio sisi; la, bali yetu ndiyo Jumuiya pekee ambayo iko nje ya maana na upeo wa utabiri huu, kwani Jumuiya hii bado inao wafuasi wachache tu amba kwao neno "taifa" na "kabila" haliwezi kutumika. Yesu kwa mamlaka ya ufunuo wa kimbingu anasema kwamba ishara itakapotokea mbinguni watu wote wa ulimwenguni amba, kutokana na idadi yao watastahili kuainishwa kwa "kabila" au "taifa" watapiga vifua vyao; hapatakuwa na asiyehusika isipokuwa watu wenye idadi ndogo amba kwao neno "taifa" haliwezi kutumika. Si Wakristo wala Waislamu, wala Mayahudi na wala Mkanushaji ye yote auezaye kuwa nje ya utabiri huu.

Jumuiya yetu peke yake ndiyo iko nje ya upeo wa utabiri huu kwani wamepandwa kama mbegu na Mwenyezi Mungu hivi punde. Neno la nabii haliwezi kuwa la uwongo. Wakati maneno haya yana kidokezo cha wazi wazi kwamba kila taifa likaalo ulimwenguni litaomboleza, ni wepi mionganoni mwa watu hawa

wawezao kudai kwamba wako nje ya upeo wa maneno haya? Yesu hajakiri kutokuhusika kwa ye yote katika aya hii. Lakini lile kundi ambalo bado halijafikia ukubwa wa "kabila" au "taifa" kwa vyo vyote vile halihusiki yaani Jumuiya yetu. Na utabiri huu umetimilizwa waziwazi katika zama hizi, kwani ule ukweli kuhusu Yesu ambaao umegunduliwa hivi sasa bila shaka ndio chanzo cha maombolezo ya makabila haya, kwani umefichua makosa yao wote. Makelele yote ya Wakristo kuhusu uungu wa Yesu yanageuka na kuwa mipumuo ya huzuni; kung'ang'ania kwa Waislamu - usiku na mchana - kwamba Yesu amepaa mbinguni akiwa hai, kunageuka na kuwa kilio cha maombolezo; na Mayahudi hao ndio wanaopoteza kila kitu.

Na hapa ni lazima kutaja kwamba katika kauli iliyomo katika aya hiyo, yaani, kwamba wakati ule mataifa yote ya dunia yatapiga vifua vyao, "dunia" ina maana ya Baladish-Sham (Falastin na Syria - Mfasiri) ambazo zina uhusiano na watu hawa wa aina tatu - Mayahudi kwa sababu hapo ndipo mahala pao pa asili na mahala pao pa ibada; Wakristo kwa sababu Yesu alitokea mahali hapo na jumuiya ya kwanza ya dini ya Kikrsto iliinukia kutoka katika nchi ile; Waislamu, kwa sababu watakuwa warithi wa nchi hii hadi siku ya kiyama. Na kama neno "dunia" litachukuliwa kuwa na maana ya kuzikusanya nchi zote, hata hivyo hakuna tatizo, kwani ukweli utakapodhihirishwa wakanushaji wote wataaibika.

Na mionganoni mwa ushahidi uliotufikia kupitia Injili ni kauli inayoandikwa hapa chini kutoka katika Injili ya Mathayo: "Na makaburi yakafunguliwa, na miili mingi ya watakatifu iliyolala ikaamka na kutoka nje ya makaburi baada ya kufufuka kwake (yaani Yesu) na wakauingia mji na wakajitokeza kwa watu wengi" (Mathayo 27:52).

Hapana shaka hata ile ndogo kwamba kisa hiki kilichotajwa katika Injili, yaani, kwamba baada ya kufufuka kwa Yesu watakatifu walitoka nje ya makaburi na kujitokeza wakiwa hai kwa watu wengi, hakitokani na uhakika wa kihistoria; kwani kama ingekuwa hivyo, siku ya kiyama ingekuwa imetendeka katika ulimwengu huu huu, na kile ambacho kilikuwa kimewekwa siri

kwa maana ya kuwa kipimo cha imani na uaminifu kingebainishwa kwa wote; imani isingekuwa imani, na, machoni pa kila mumini na mkanushaji, hali ya ulimwengu ujao ingekuwa jambo la dhahiri na bayana kama vile kuwako kwa mwezi, jua na kuhitilafiana kwa usiku na mchana kulivyokuwa jambo la wazi. Katika hali kama hiyo imani isingalikuwa kitu chenye kuthaminiwa na isingalikuwa kitu cha thamani ambacho kingeweza kuleta thawabu yo yote.

Kama watu na Manabii wa zamani wa Israeli ambao idadi yao ni mamilioni, walifufuliwa kweli wakati wa kusulubishwa kwa Yesu na wakaja mjini wakiwa hai, na kama muujiza - kwamba mamia ya manabii na mamia mengi ya maelfu ya watakatifu yalifufuliwa kwa wakati mmoja - kwa hakika ulionyeshwa kama uthibitisho wa ukweli wa uungu wa Yesu, Mayahudi walikuwa na fursa nzuri sana ya kuwauliza hawa manabii waliofufuliwa, iwapo Yesu aliyedai kuwa yeye ni Mungu ni Mungu kweli au alidanganya. Na huenda hawakuipoteza fursa hii. Ni lazima waliuliza kuhusu Yesu, kwani walikuwa na shauku ya kuwauliza wafu kama wangaliweza kufufuliwa. Kwa hiyo, wakati mamia ya maelfu ya watu walifufuliwa na kuja mjini na maelfu ya hao yalirudi kwenye nyumba zao, Mayahudi wangewezaje kuiachilia fursa kama hii? Ni lazima wawe wameulizia, siyo kutoka kwa mtu mmoja au wawili, bali kutoka kwa maelfu; na wale wafu kila mmoja alipoingia katika nyumba yake ni lazima kulikuwa na msisimko katika kila nyumba, kwani mamia ya maelfu ya hao yalirudishwa ulimwenguni. Katika kila nyumba lazima kulikuwa na mazungumzo mengi na kila mtu ni lazima alikuwa akiwauliza wafu iwapo walijua kwamba yule mtu aliyejiita Yesu Masihi alikuwa ni Mungu kweli. Lakini, kwa kuwa Mayahudi hawakumwamini Yesu kama ilivyotazamiwa, wala nyoyo zao hazikulainika, bali waliimarika katika ugumu wa miyo, inaelekeea yumkini wafu hao hawakuzungumza neno jema kumhusu yeye. Ni lazima walitoa majibu bila kusita kwamba mtu huyu alikuwa anatoa madai potofu ya Uungu na alikuwa akisema uwongo dhidi ya Mwenyezi Mungu. Hiyo ndiyo sababu Mayahudi hawakuacha utundu, ingawa mamia ya maelfu ya manabii yalifufuliwa. Baada ya "kumwua" Yesu

wakajaribu kuwaua watu wengine. Mtu awezaje kuamini kwamba mamia ya maelfu ya watakatifu waliokuwa wamelala makaburini mwao katika ardhi ile iliyobarikiwa, tangu zama za Adamu hadi zama za Yohana Mbatizaji, wote hao wawe wamefufuliwa? - kwamba wote hao waje mjini kuhubiri, na kila mmoja wao asimame na kutoa ushahidi mbele ya maelfu ya watu kwamba Yesu, Masihi hakika alikuwa mwana wa Mungu - la, bali Mungu mwenyewe; kwamba yeye tuaabudiwe; kwamba watu lazima waache imani zao za zamani vinginevyo watakwenda motoni ambako watakatifu hao wamekushuhudia wao wenyewe! na bado pamoja na kuwepo kwa ushahidi mzuri wa namna hiyo na taarifa za watu walioshuhudia kwa macho yao zilizotoka vinywani mwa mamia ya maelfu ya watakatifu waliokufa, Mayahudi wasiache kukataa kwao! Mimi binafsi siko tayari kuamini hivyo. Kwa hiyo, iwapo mamia ya maelfu ya watakatifu na manabii na mitume kadhalika, waliokuwa wamekufa, walifufuka kweli na kuja mjini kutoa ushahidi, bila shaka walitoa ushahidi usiofaa; kamwe hawakutoa ushahidi wenyewe kuunga mkono uungu wa Yesu. Hii yaelekeea kuwa ndiyo iliyokuwa sababu kwa nini Mayahudi baada ya kuusikiliza ushahidi wa wafu, wakaimarika katika kutoamini kwao. Yesu alitaka kuwafanya waamini uungu wake, lakini hao, kutokana na ushahidi huu, walikanusha kwamba wala hakuwa nabii. Kwa kifupi, imani za namna hiyo zina matokeo mabaya na yenye kuleta madhara sana - imani hizi, yaani kwamba mtu aseme kuwa haya mamia ya maelfu ya watu waliokufa au mtu ye yote aliye kufa kabla ya zama zile alifufuliwa na Yesu; kwani, kurejeshewa uhai kwa wale waliokufa hakukuleta jambo lo lote la maana. Mtu aliyetembelea nchi ya mbali na ambaye anarudi mjini kwake baada ya miaka michache ya kutokuwapo kwa kawaida huwa na shauku ya kuwaambia watu kuhusu mambo ya ajabu aliyo yaona na kuwasimulia hadithi za ajabu za nchi aliyetembelea; hatanyamaza au kuwa na ulimi uliofungwa akutanapo na watu wake baada ya kipindi kirefu cha kutengana. Hasha, wakati kama huo watu wengine pia huwa na shauku ya kumkimbia na kumkuliza kuhusu nchi ile; na iwapo kwa bahati watu hawa wanafikiwa na

mtu fulani aliye dhalili, mpole kwa umbile na ambaye hata hivyo anadai kuwa mfalme wa nchi ambayo mji wake mkuu umekwisha onwa na watu hawa na ambaye anasema kwamba yeye ni mkubwa zaidi katika cheo cha ufalme kuliko mfalme mwininge huyu au yule, kwa kawaida watu huhoji kuhusu wasafiri kama hao, iwapo mtu fulani anayepitapita wakati ule katika nchi yao ni mfalme kweli wa nchi ile; na kisha, wale wasafiri, kulingana na yale waliyoweza kuyaona, huyajibu maswali ya namna hiyo. kwa kuwa hivi ndivyo ilivyo, kama nilivyokwisha sema hapo kabla, kufufuliwa kwa wafu na Yesu kulikuwa kunastahili kuaminiwa iwapo ule ushahidi walioulizwa wafu - kuuliza ambako kulikuwa hapana budi kufanywe - ulileta matokeo mema. Lakini hapa sivyo ilivyokuwa. Kwa hiyo, pamoja na hiyo dhana kwamba wafu walifufuliwa, mtu analazimika kudhani pia kwamba hao wafu hawakutoa ushahidi unaofaa kwa Yesu, ambao ungemfanya mtu auamini ukweli wake; bali walitoa ushahidi ambao ulizidisha mtafaruku. Laiti kama mnyama fulani angetangazwa kuwa amefufuliwa badala ya binadamu wa kweli! Hiyo ingalitatta matatizo mengi. Kwa mfano, kama ingalisemwa kwamba Yesu alifufua elfu chache za madume ya ng'ombe - hayakuwa na ulimi wa kutolea ushahidi unaofaa au usiofaa! Lakini wafu ambao Yesu aliwafufua walikuwa binadamu. Kama baadhi ya Wahindu wataulizwa hivi leo iwapo kama mababu zao wa zamani kumi au ishirini wangefufuliwa na kurudishwa ulimwenguni, na kama wangesema kwamba dini kadhaa na kadhaa ndiyo dini ya kweli, bado tu wangekuwa na shaka kuhusu ukweli wa dini ile. Kamwe wasingesema kuwa ni ya kweli.

Kwa hiyo, lichukulieni kuwa jambo la yakini kabisa kwamba hakuna mtu ulimwenguni kote awezaye kuendelea kutoamini kwake na pia ukushaji wake baada ya ubainishaji wa namna hii. Nasikitika kwamba katika kubuni hekaya za namna hii Masingasinga wa nchi yetu wamefanya vizuri zaidi kuliko Wakristo. Hawa Masingasinga wametoa uthibitisho wa werevu wao katika sanaa ya kutunga hekaya; kwani wanasesma kwamba Guru wao, Bawa Nanak, mara moja alimfufua tembo. Sasa huu

ni "muujiza" ambao haukabiliwi na upinzani uliotajwa hapo juu. Kwani Masingasinga wanaweza kusema: Huyo tembo hakuwa na ulimi wa kuongelea, kwamba angaliweza kutoa ushahidi wa kumwunga mkono au wa kumkanusha Bawa Nanak. Kwa kifupi, watu wa kawaida wenyewe akili ndogo, wanafurahishwa na "miujiza" kama hiyo lakini wenyewe hekima wanakuwa walengwa wa upinzani wa watu wengine na hivyo wanakerwa na upinzani huo. Wanafedheheshwa mbele ya wale wanaohusishwa na hekaya hizo za kipuuzi. Hivyo, kwa kuwa mimi ninazo hisia zile zile za upendo na ukweli kwa Yesu kama walizonazo Wakristo, la bali mimi nina fungamano la nguvu zaidi kwake, kwani Wakristo hawamjui mtu huyu wanayemsifu lakini mimi namjua ninayemsifu, kwani nimemwona; kwa hiyo, naendelea kufichua hali halisi ya taarifa zilizotolewa katika Injili - kama vile ile taarifa kwamba wakati wa tukio la msalaba watakatifu wote waliokufa walifufuliwa na wakaja mjini.

Kwa hiyo, naieleweke wazi wazi kwamba taarifa kama hizi zinakuwa katika hali ya Kashf, kama lile ono lililoonwa na baadhi ya watu watakatifu wakati wa tukio la msalaba - kwamba watakatifu waliokufa walifufuliwa na wakaja mjini ambako waliwatemebelea watu. Na kama vile ndoto zilivyo na uaguzi wake ambao umetajwa hata katika kitabu kitakatifu cha Mungu - kwa mfano ndoto ya Yusufu ilikuwa na uaguzi - ono hili pia lilitakiwa liwe na uaguzi wake; na uaguzi huu ulikuwa kwamba Yesu hakufa juu ya Msalaba; kwamba Mwenyezi Mungu Alimwokoa na kifo juu ya msalaba. Na kama swalii liliizwe kwamba nimeupata wapi uaguzi huu, jibu lake ni kwamba watu maarufu wenyewe maarifa yawezayo kupokewa bila shaka kuhusu sanaa ya uaguzi wanasema hivyo, na waaguzi wote wameshuhudia hivyo kutokana na uzoefu wao. Hapa nanukuu kutoka katika uaguzi wa mtu wa kale aliyekuwa maarufu na mwenye maarifa kuhusu sanaa ya uaguzi, yaani mtunzi wa Ta'tirul - Anam: (Tazama Kitaab Ta'tirul - Anam fi Ta'birul - Manam, kilichotungwa na Qutubuz-Zaman Shaikh Abdul Ghani An-Nablisi, ukurasa 289) ambao ukitafsiriwa ni kwamba kama mtu ye yote anaona katika ndoto au ono lililo

katika hali ya kashf, kwamba wafu wametoka makaburini na wamekwenda majumbani kwao, uaguzi wake ni kwamba mfungwa ataachiwa huru kutoka kifungoni, na kwamba ataokolewa kutoka katika mikono ya watesi wake. Karina hii inaonyesha kwamba mfungwa huyu atakuwa mtu mkubwa na mashuhuri. Hivyo itaonekana jinsi uaguzi huu kiakili unavyohusikana na Yesu. Mtu anaweza kuelewa mara moja kwamba baada ya kufufuka, watakatifu waliokuwa wamefufuka walionekana wakienda mjini ili kuonyesha ukweli huu, ili wenye hekima wajue kwamba Yesu ameokolewa na kifo cha Msalabani.

Kadhalika, rejea nyingi zaidi katika Injili zinaonyesha wazi wazi kwamba Yesu hakufa Msalabani; aliokolewa nacho, na akahamia nchi nyingine. Lakini, nafikiri yale niliyoyaeleza yanatosha kwa mtu asiyé na upendeleo usio na sababu za kiakili.

Yawezekana baadhi wanaweza kukaribisha miyoni mwao ule upinzani kwamba mbona Injili zinasema mara kwa mara kwamba Yesu alikufa msalabani, au kisha baada ya kufufuliwa alipaa mbinguni. Upinzani wa namna hii nimekwisha ujibu kwa kifupi, lakini ningeweza kusema tena kwamba kukutana kwa Yesu (amani juu yake) na wanafunzi baada ya tukio la Msalaba; kusafiri kwake hadi Galilaya; kula mkate na nyama; kuonyesha vidonda vya mwilini mwake; kukaa usiku mzima na wanafunzi pale Emmau; kukimbia kisirisiri kutoka kwenye mamlaka ya Pilato; kuhama kutoka mahali pale kama ilivyokuwa desturi ya manabii; na kusafiri chini ya kivuli cha woga - matukio yote haya yanathibitisha kwamba hakufa msalabani; kwamba mwili wake uliendelea kuwa na sifa yake ya kufa; na kwamba haukupata mabadiliko yo yote.

Hakuna ushahidi katika Injili kwamba mtu ye yote alimwona Yesu akipaa mbinguni; na hata kama ushahidi kama huo ungelikuwapo, usingekuwa wa kuaminiwa, kwani kutengeneza milima kwa kutumia vichuguu vya fuko na kuvikuza vitu vidogo vionekane vikubwa yaonekana kuwa ni tabia ya waandishi wa Injili. Kwa mfano, kama mmoja anatokea kusema kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu, mwingine anaanza kumfanya Mungu kamili,

wa tatu anampa uwezo juu ya ulimwengu wote, na wa nne anasema bila kificho kwamba ye ye ni kila kitu, na kwamba hakuna Mungu mwingine zaidi ya ye ye. Kwa kifupi, kutia chumvi kunawafikisha mbali sana. Kama mtu atafikiria lile ono ambamo wafu walionekana wakitoka nje ya makaburi yao na kuelekea mjini, mtu huyo atagundua kwamba ono hili lilikuwa limepewa uaguzi wake wa dhahiri kiasi cha kusema, kwamba wafu kidhahiri walitoka nje ya makaburi yao na kuja katika jiji la Yerusalem ambako waliwatemebelea watu. Sasa ona, jinsi "Unyoya" mmoja wa kunguru ulivyofanywa kuwa "kunguru"; na si kunguru mmoja tena, bali mamilioni mengi! Wakati mambo yanatiwa chumvi kiasi hicho, hatuna jinsi ya kuutafuta ukweli. Vile vile yafaa kufikiria - kwamba hizi Injili, zinazoitwa vitabu vy a Mungu, zina madai yasiyosadikika - kama vile, kama kazi zote za Yesu zingewekwa katika maandishi, maandishi hayo yasingepata nafasi ya kuyahifadhia ulimwenguni kote! Je kutia chumvi kwa namna hiyo ndiyo njia ya uaminifu na ukweli? Iwapo kazi za Yesu zilikuwa hazina kikomo kama hivyo, na iwapo hazingeweza kuandikwa, ilikuwaje kwamba kazi hizo zilifanyika katika kipindi cha miaka mitatu tu? Tatizo jingine kuhusu hizi Injili ni kwamba zinatoa rejea za kimakosa kuhusu baadhi ya vitabu vy a kale; hazisemi kwa usahihi hata kuhusu ukoo wa Yesu. Kutokana na Injili yaelekeea kwamba watu hawa walikuwa wazito wa kuelewa kwa kiasi hiki kwamba baadhi yao walimchukulia Yesu kuwa ni kiumbe wa kiroho.

Na hizi Injili tangu hapo mwanzoni zilikuwa zinakabiliwa na tuhuma kwamba hazikuhifadhi usafi wa maandiko yake, na kwa kuwa viko vitabu vingine vinavyoitwa Injili, hakuna sababu madhubuti kwa nini taarifa zote za hivi vitabu vingine zikataliwe, na kwa nini zote zilizomo katika hizi zinazoitwa na wengi kuwa Injili zikubaliwe kuwa za kweli. Hakuna mtu awezaye kusema kwamba hizo Injili zingine zina utiwaji chumvi kama huu unaopatikana katika hizi injili nne. Inashangaza kwamba wakati kwa upande mmoja zinasema kwamba Yesu alikuwa mtu mchamungu na kwamba tabia yake haikuwa na lawama, kwa

upande mwengine zinaletwa dhidi yake tuhuma zisizomstahili mtu ye yote aliye mchamungu. Kwa mfano, pasipo shaka kulingana na mafundisho ya Taurati, manabii wa Kiisraeli walikuwa na mamia ya wanawake kwa wakati mmoja, ili kwa kufanya hivyo waweze kuongeza kizazi cha wachamungu, lakini hungesikia kamwe kwamba nabii ye yote aliwahi kuonyesha mfano wa uhuru kama huu kwamba amruhusu mwanamke mchafu na mzinifu, malaya maarufu wa jiji, aguse mwili wake kwa mikono yake, kumruhusu ampakaze mafuta kichwani mwake - ustadi wa mafanikio ya uasherati wake - na kumpangusa miguu kwa nywele zake; kwamba aruhusu yote haya kufanywa na mwanamwali mzinifu, na asimwambie "Acha". Mtu ataoolewa na lawama ya kushuku ambako kunajileta kwenyewe mtu aonapo jambo la namna hii - kwa kuamini wema wa Yesu. Hata hivyo, mfano huu si mzuri kwa watu wengine. Kwa kifupi, Injili hizi zinayo mambo mengi yanayoonyesha kwamba hazikuhifadhi hali yao ya asili, au kwamba waandishi wake walikuwa watu wengine - sio wale wanafunzi. Kwa mfano, je inaweza, ile taarifa ya Injili ya Mathayo: "Na hili linajulikana vema mionganoni mwa Mayahudi hadi leo", kunasibishwa na Mathayo? Alikuwa mtu mwengine ambaye aliishi katika wakati ambapo Mathayo alikuwa tayari amekwisha fariki? Kisha, Injili hiyo hiyo ya Mathayo inasema: "Na wakakusanyika pamoja na wazee, wakafanya shauri, wakawapa askari fedha nyingi, wakisema, semeni ya kwamba wanafunzi wake walikuja usiku na wakamwiba sisi tulipokuwa tumelala" (Mathayo 28:12-13). Yaweza kuonekana jinsi taarifa kama hizo zisivyosadikika na zisivoingia akilini. Kwa maana ya kauli hii ni kwamba Mayahudi walitaka kuficha kufufuaka kwa Yesu kutoka katika wafu, na kwamba waliyahonga maaskari ili kwamba mwujiza huu mkubwa usijulikane kwa watu wengi, kwa nini basi Yesu ambaye wajibu wake ulikuwa kuutangaza mwujiza huu mionganoni mwa Mayahudi, aliufanya kuwa siri; la bali aliwakataza watu wengine kuutangaza? Kama ikidaiwa kwamba aliogopa kukamatwa, ningesema kwamba, wakati amri ya Mwenyezi Mungu ilipomshukia, na baada ya kufariki akaufufuka akiwa na mwili wa kiroho na mtukufu, hofu

gani aliyokuwa nayo sasa kuhusu Mayahudi? - Bila shaka Mayahudi sasa hawakuwa na uwezo wo wote juu yake; sasa alikuwa mbele na juu ya maisha yawezayo kufa. Mtu anaona kwa masikitiko kwamba, wakati kwa upande mmoja inasemekana kwamba alikutana na wale wanafunzi na akaenda Galilaya na kutoka hapo akapaa mbinguni, hata hivyo anawaogopa Mayahudi kwa mambo madogo madogo tu, na pamoja na kuwa na mwili wenye utukufu, anakimbia kisiri siri kutoka katika nchi ile, isije Mayahudi wakamgundua; anakwenda safari ya maili sabiini hadi Galilaya ili kuokoa maisha yake na mara kwa mara anawaomba watu wasiwaambie watu wengine kuhusu jambo hili. Je hizi ndizo dalili na ishara za mwili wenye utukufu? Hapani! Ukweli ni kwamba haukuwa mpya wala haukuwa mwili wenye utukufu - ulikuwa mwili ule ule, wenye vidonda, ambaeo uliokolewa katika kifo; na, kwa vile kulikuwako bado na ile hofu ya Mayahudi, Yesu aliihama nchi ile kwa kutumia njia zote za uangalifu. Mazungumzo ya jambo lo lote yaliyo kinyume na maelezo haya ni upuuzi mtupu; - kama lile linalohusu Mayahudi kuwashonga maaskari ili kuwafanya waseme kwamba wanafunzi waliiiba maiti wakati hao maaskari walipokuwa wamelala. Iwapo hao maaskari walikuwa wamelala wanaweza kuulizwa vizuri sana jinsi walivyoweza kujua wakati wakiwa usingizini kwamba maiti ya Yesu iliibiwa. Na kutokana na huo uhakika peke yake wa Yesu kutokuwemo ndani ya kaburi, je mtu mwenye akili timamu anaweza kuamini kuwa amepaa mbinguni? Je hapawezi kuwako na sababu zingine ambazo kwazo makaburi yanaweza kubakia tupu? Wakati wa kupaa mbinguni ilikuwa ni wajibu wake Yesu kukutana na mamia machache ya Mayahudi, na pia Pilato. Alikuwa akimwogopa nani akiwa na mwili wake wenye utukufu? Hakujali kuwapatia wapinzani wake hata uthibitisho mdogo tu. Bali alishikwa na hofu na akakimbilia Galilaya. Hii ndiyo sababu tunaamini kwa uhakika kwamba ingawa ni kweli kwamba aliliacha lile kaburi, lililokuwa kama nyumba na lenye mlango, na ingawa ni kweli kwamba alikutana kwa siri na wale wanafunzi, hata hivyo siyo kweli kwamba alipewa mwili wo wote mpya na wenye utukufu; ulikuwa mwili ule ule, na vidonda

vile vile na hofu ile ile moyoni mwake isije walaaniwa Mayahudi wakamkamata tena. Wewe soma kwa utulivu tu Mathayo, sura ya 28 aya ya 7 hadi ya 10. Aya hizi zinasema wazi wazi kwamba wale wanawake walioambiwa na mtu fulani kwamba Yesu alikuwa hai na alikuwa anakwenda Galilaya, na ambao pia walinong'onezwa kwamba wawajulishe wanafunzi, bila shaka walifurahi kusikia habari hizi, lakini walikwenda wakiwa na moyo wenye hofu, - walikuwa bado wanaogopa isije Yesu akashikwa tena na Mayahudi waovu. Na aya ya tisa inasema kwamba wakati wanawake hawa walipokuwa njiani kwenda kuwajulisha wanafunzi, Yesu alikutana nao na akawasalimu. Na aya ya kumi inasema kwamba Yesu aliwaomba wasiwe na hofu, yaani, ya kukamatwa kwake; akawaomba wawajulishe nduguze kwamba wote waende Galilaya¹; kwamba wataonana naye huko, yaani, hakuweza kukaa pale kwa kuwaogopa maadui. Kwa kifupi, kama Yesu alifufuka kweli kutoka katika kifo na akapata mwili wenye utukufu, ulikuwa wajibu wake kuwapatia Mayahudi uthibitisho wa maisha kama hayo. Lakini tunajua kwamba hakufanya hivyo. Kwa hiyo, ni upuuzi kuwalamu Mayahudi kwa kujaribu kufanya uthibitisho wa kufufuka kwa Yesu ukarushike. Hapana, Yesu mwenyewe hakutoa walau uthibitisho mdogo tu wa kufufuka kwake; bali kwa kukimbia kwake kisirisiri, na kwa uhakika wa yeye kuwa amekula chakula, na kulala na kuonyesha vidonda vyake, yeye mwenyewe alithibitisha kwamba hakufa Msalabani.

1. Hapa, Yesu hakuwaliwaza wale wanawake kwa maneno kwamba amefufuka akiwa na mwili mpya na wenye utukufu, kwamba sasa hakuna awezaye kumkamata. Hapana, kwa kuona hali yao ya udhaifu aliwaliwaza kwa njia ambayo kwa kawaida wanaume huitumia kuwaliwaza wanawake. Kwa kifupi hakutoa uthibitisho wa mwili wenye utukufu; bali alionyesha nyama na mifupa yake na hivyo kuthibitisha kwamba ulikuwa mwili wa kawaida wenye kufa.

SURA YA PILI

Kuhusu ushahidi wa Qur'an Tukufu na mapokeo sahihi yanayothibitisha kuokoka kwa Yesu

Hoja ambazo sasa nitaziratibu zaweza kuonekana kuwa hazina maana kwa vile zimekusudiwa kuwaongoza Wakristo, kwani watu hawa hawalazimiki kukubali kile kinachosemwa na Qur'an Tukufu au Hadithi kuhusu suala hili; lakini ninazisema tu kwa sababu ninataka Wakristo waujue muujiza wa Qur'an yetu na Mtume Mtukufu s.a.w.; kuwaambia kwamba ule ukweli ambaa umegundulika baada ya mamia ya miaka tayari umekwisha tangazwa na Mtume wetu Mtukufu na Qur'an. Hivyo basi, naratibu baadhi ya ukweli huo hapa chini:-

Mwenyezi Mungu Mwenye nguvu Anasema katika Qur'an: "Na kusema kwao: Hakika tumemwua Masihi Isa mwana wa Mariamu, Mtume wa Mungu; hali hawakumwua wala hawakumfisha msalabani, bali alifananishwa kwao (kama maiti). Na kwa hakika wale waliohitilafiana kwalo, yakini wana shaka nalo, wao hawalijui hakika yake isipokuwa wanafuata dhana. Na kwa yakini wao hawakumwua- Bali Mwenyezi Mungu Alimnyanya Kwake, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye hekima." Yaani Mayahudi hawakumwua Yesu wala hawakumfisha juu ya msalaba, hapana, walishuku tu kwamba Yesu alikufa Msalabani; hawakuwa na hoja ambazo zingeweza kuwashawishi na kuwaridhisha kwamba Yesu (amani juu yake) alikufa kweli msalabani.

Katika aya hizi Mwenyezi Mungu Mwenye nguvu Anasema kwamba ingawa ni kweli kwamba kidhahiri Yesu aliwekwa msalabani, na kwamba walikuwa wamedhamiria kumwua, hata hivyo ni makosa kwa Mayahudi na Wakristo kudhania kwamba Yesu alikufa kweli juu ya msalaba. Hapana, Mwenyezi Mungu Alitengeneza mazingira ambayo yalimwokoa Yesu na kifo cha msalabani.

Hivyo basi, kama mtu ni mwadilifu atalazimika kusema kwamba kilichosemwa na Qur'an dhidi ya Mayahudi na Wakristo hatimaye kikatokea kuwa kweli. Na uchunguzi wa hali ya juu sana hivi leo umethibitisha kwamba kwa kweli Yesu aliokolewa na kifo cha Msalabani. Usomaji kwa bidii wa kumbukumbu unonyesha kwamba Mayahudi hawakuweza kamwe kulijibu hili swalii: Ilikuwaje kwamba Yesu alikuwa katika kipindi cha masaa mawili au matatu ilhali mifupa yake haikuvunjwa?

Hili likawafanya Mayahudi walete utetezi mwingine - kwamba walimwua Yesu kwa upanga, ilhali historia ya kale haionyeshi kwamba Yesu aliuawa kwa upanga. Utukufu na uwezo wa dhati Tukufu ya Mwenyezi Mungu ulifanya pawepo na giza ili Yesu aweze kuokolewa. Palikuwapo na tetemeko la ardhi. Mkewe Pilato aliona ndoto. Usiku wa sabato ulikaribia kuingia ambapo haikujuzu kuruhusu mwili uliosulubiwa ubakie msalabani. Na yule hakimu kutokana na ndoto ile ya kutisha, akawa amepata shinikizo la kumwachilia Yesu. Yote haya yaliletwa sawia na Mwenyezi Mungu ili kumwokoa Yesu. Yesu mwenyewe alifanywa azimie ili achukuliwe kuwa amekufa. Kwa njia ya ishara za kutisha kama ile ya tetemeko la ardhi, na kadhalika, ukalazimika katika nafsi za Mayahudi woga na hofu, na pia hofu ya adhabu ya kimbingu. Pia kuliwako na hofu isije ile miili ikabakia misalabani wakati wa usiku wa Sabato. Tena, Mayahudi walipomwona Yesu akiwa katika hali ya kuzimia walidhani kuwa amekwisha kufa. Ilikuwa giza. Na kulikuwako na tetemeko la ardhi na wasiwasi mkubwa. Pia walikuwa na wasiwasi kuhusu majumbani kwao - watoto wao walikuwa wakijisikiae katika hali ile ya giza na tetemeko la ardhi? Pia kulikuwako na hofu kubwa katika mioyo yao kwamba kama mtu huyo alikuwa mwongo na Kaafir kama walivyomdhania, kwa nini ishara zenyenuguu zimeonyeshwa wakati wa kuteswa kwake - ishara ambazo hazikuonyeshwa hapo kabla? Walikuwa wamefadhaika sana kiasi kwamba hawakuwa tena katika hali ya kujiridhisha wenyewe iwapo Yesu alikuwa amekufa kweli au kwa hakika alikuwa katika hali ya namna gani.

Lakini kile kilichotokea ulikuwa mpango wa kimbingu wa

kumuokoa Yesu. Hii inadokezwa katika ile aya . . . yaani, Mayahudi hawakumwua Yesu - Mwenyezi Mungu Aliwafanya waamini kwamba walikwisha mwua. Mazingira haya yanawatia moyo wacha-Mungu kumtegemea Mwenyezi Mungu, kwamba Mwenyezi Mungu Anaweza kuwaokoa watumishi wake jinsi Atakavyo.

Na Qur'an Tukufu inayo aya hii: "Jina lake litakuwa Mashihi Isa mwana wa Mariamu, mwenye heshima katika dunia na Akhera, na yu mionganoni mwa wale waliopewa ukaribu na Mwenyezi Mungu".

Hii ina maana kwamba, siyo tu hapa, ambapo Yesu atakuwa na heshima na umashuhuri na kuwa na ukuu machoni pa watu wa kawaida, bali hata akhera pia. Hivyo, ni dhahiri kwamba Yesu hakuheshimiwa katika nchi ya Herod na Pilato. Kinyume cha hayo, yeye alifedheheshwa. Na kuleta rai kwamba ataheshimiwa wakati wa kuja kwake mara ya pili duniani ni jambo lisilokuwa na msingi. Ni kinyume na vitabu vitakatifu na kinyume na sheria ya milele ya hali ya asili. Isitoshe hakuna uthhibitisho wa jambo hilo. Lakini ukweli ni kwamba baada ya kuachiliwa kutoka mikononi mwa watu wale walaaniwa, Yesu alikuja katika ardhi ya Punjab na akaifanya iheshimike kutokana na ziara yake; Mwenyezi Mungu alimpa umashuhuri mkubwa - hapa akayakuta makabila kumi yaliyopotea ya Israeli. Yaonekana takriban wote mionganoni mwa Waisraeli hawa walikuwa wameangukia kwenye ibada ya masanamu ilio duni sana. Lakini kutokana na kuja kwa Yesu mahali hapa, takriban wote walirejea kwenye njia ilio sawa; na kwa kuwa katika mafundisho ya Yesu mlikuwemo mawaidha ya kumwamini Mtume atakayekuja, yale makabila kumi ambayo yalikuja kujulikana katika nchi hii kama Waafghani na Wakashmiri hatimae yote yakawa Waislamu. Kwa hiyo Yesu alikuja na heshima kubwa katika nchi hii. Hivi karibuni imegunduliwa sarafu katika nchi hii ya Punjab, ambamo limeandikwa jina la Yesu (amanji juu yake) kwa herufi za Kipali.

Sarafu hii ni ya zama za Yesu. Hii inaonyesha kwamba Yesu alikuja katika nchi hii na alipokewa kwa heshima ya kifalme; sarafu

hii ni lazima iwe imetolewa na mfalme ambaye alikuwa mfuasi wa Yesu. Sarafu nyingine imepatikana ikiwa na sanamu ya Muisraeli. Yaonekana kwamba hii pia ni sanamu ya Yesu.

Qur'an tukufu pia inayo aya isemayo kwamba Yesu alibarikiwa na Mwenyezi Mungu kila alipokwenda . . . kwa hiyo, sarafu hizi zinaonyesha kwamba alipokea heshima kubwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu, na kwamba hakufa hadi alipopata heshima ya kifalme. Kadhalika Qur'an Tukufu inayo aya hii: "(Kumbukeni) Mwenyezi Mungu Aliposema: Ewe Isa kwa yakini Mimi Nitakufisha na Nitakuinua Kwangu, na nitakutakasa na (masingizio ya) wale waliokufuru

Yaani Ewe Isa! Mimi Nitakusafisha kutokana na tuhuma hizi; Nitathibitisha hali yako ya kutokuwa na hatia na Nitaziondoa lawama zilizoletwa dhidi yako na hawa Mayahudi na Wakristo. Huu ni utabiri mkubwa, ambao una maana kwamba Mayahudi walidai kuwa baada ya kusulubiwa Yesu akawa (Mungu apishe mbali) mlaaniwa, na hivyo akapoteza mapenzi ya Mungu, kwamba moyo wa Yesu, kama neno "laana" linavyolazimisha, ulimpa kisogo Mwenyezi Mungu; yaani akatokea kumchukia. Moyo wake ukawa umefunikwa na utando mnene wa giza. Akatokea kuyapenda maovu na kujitenga na mema. Ukajitenga na Mwenyezi Mungu na ukawa chini ya ushawishi wa shetani. Kukawa na uadui kati yake na Mwenyezi Mungu! Lawama hiyo hiyo - kwamba alikuwa mlaaniwa - ililetwa na Wakristo, lakini zaidi ya hiyo Wakristo kutokana na ujinga wanaunganisha hali mbili zinazopinzana na zilizo mbalimbali kabisa; wanasema kwamba Yesu alikuwa mwana wa Mungu, lakini pia wanamwita mlaaniwa, na baya zaidi wanakiri kwamba mtu aliyelaaniwa ni Mwana wa Giza na Shetani au ni shetani mwenyewe. Kwa hiyo, hizi ndizo tuhuma chafu zilizoletwa dhidi ya Yesu; lakini utabiri uliomo katika neno unaonyesha kwamba ulikuwa utokee wakati ambapo Mwenyezi Mungu Angemwondolea Yesu tuhuma zote hizi. Na huu ndio wakati ule. Bila shaka kutokuwa na hatia kwa Yesu kumethibitika machoni pa watu wenye kutafakari kutokana na ushahidi wa Mtukufu Mtume s.a.w., kwani ye ye na pia Qur'an

Tukufu imethibitisha kwamba tuhuma zilizoletwa dhidi ya Yesu (amani juu yake) zote hazina msingi. Lakini ushahidi huu kidogo ulikuwa wa kiakili na wa hali ya hoja zaidi kuweza kuwashawishi watu wa kawaida. Kwa hiyo, haki ya kimbingu ilitaka kwamba kama vile kusulubiwa kwa Yesu kulivyokuwa tukio la kuonekana wazi na la kujulikana sana, vivyo hivyo usafi wake ni lazima uonyeshwe kwa vitendo kwa namna ambayo itawafanya watu wote wauone. Na hilo likatimia. Kutokuwa na hatia kwa Yesu kumo katika misingi siyo tu ya hoja bali kumeonyeshwa kwa vitendo kwa njia iliyo bayana kuliko zote. Kwani, mamia ya maelfu ya watu kwa macho yao wenyewe wameona kwamba kaburi la Yesu a.s. linapatikana njimi Srinagar, Kashmir. Na kama vile alivyosulubiwa mahala paitwapo Golgotha, yaani mahali pa "Sri", vivyo hivyo na kaburi lake lake limekutwa mahali pa "Sri", yaani, Srinagar. Neno "Sri" linalopatikana katika majina ya mahali pote pawili ni jambo la kustaajabisha sana. Mahali ambapo Yesu alisulubiwa paliitwa Gilgit au "Sri", na mahali ambapo katika sehemu ya mwisho ya karne ya kumi na tisa kaburi la Yesu liligunduliwa pia panaitwa Gilgit, au "Sri". Na yaelekeea kwamba mahali panapoitwa Gilgit nchini Kashmir, panaashiria neno hilo hilo "Sri". Mji huu huenda ulianzishwa katika zama za Yesu, na ikiwa kama kumbukumbu ya tukio la Msalaba kwa ajili ya mahali pale, ukaitwa Gilgit, yaani "Sri"; kama vile Lhasa, ambayo ina maana ya "Mji wa anayestahili kuabudiwa"; neno hili ni la asili ya Kiebrania na linaashiria kwamba mji huu pia ulianzishwa katika zama za Yesu.

Na taarifa za kuaminika katika hadithi zinaonyesha kwamba Mtukufu Mtume s.a.w. alisema kuwa Yesu alikuwa na umri wa miaka 125. Isitoshe, firqa zote za Kiislamu zinaamini kwamba Yesu alikuwa na sifa mbili za pekee - sifa ambazo hazipatikani kwa nabii mwingine ye yote, nazo ni:

(1) Aliishi hadi kufikia umri kamili wa uzee, yaani hadi miaka 125; (2) Alitembea katika sehemu nyingi za ulimwengu na kwa hiyo akaitwa "nabii mtembeaji". Ni dhahiri kwamba kama alipaishwa mbinguni akiwa na umri wa miaka 33 tu taarifa ya

"miaka 125" isingalikuwa kweli, wala asingalikuwa ametembea kwa kiasi kikubwa kama hicho ilhali alikuwa na umri wa miaka 33 tu. Na siyo tu taarifa hizi zinapatikana katika vitabu vya Hadithi vyenye kuaminika. Zimekuwa zikijulikana sana mionganoni mwa firqa za Kiislamu hivi kwamba ni vigumu kufikiria jambo lingine lo lote ambalo limepata kujulikana kwa wingi zaidi mionganoni mwao. Kanzul - Ummal (Jalada la 2) ambacho ni kitabu cha Hadithi chenye habari nyingi kinayo Hadithi kwenye ukurasa wa 34 kutoka kwa Abu Huraira. Yaani, Mwenyezi Mungu Alimfunulia Yesu a.s., Ewe Isa! Tembea kutoka mahali pamoja kwenda mahali pengine". Yaani, nenda kutoka nchi moja hadi nyingine isije ukabainika na kuteswa. Tena, kwenye kitabu hicho hicho kama ilivyoripotiwa na Jabar, ipo Hadithi Isemayo:

¹Kila mara Yesu alikuwa akisafiri; alikwenda toka nchi moja hadi nyingine, na usiku ulipoingia alikuwa akila majani ya porini na kunywa maji safi po pote alipokuwa. Tena kwenye kitabu hicho hicho ipo taarifa kutoka kwa Abdullah bin Umar:

²Mtukufu Mtume alitangaza kwamba wenyewe kupendwa sana mbele ya Mwenyezi Mungu ni wale walio maskini. Aliulizwa neno maskini linamaanisha nini? je ni wale watu ambao kama Yesu Masihi walizikimbia nchi zao wakiwa na Imani zao?

-
1. Jalada la 2 ukurasa 71
 2. Jalada la 2 ukurasa 51

SURA YA 3

Kuhusu Ushahidi unaotokana na Vitabu vyatiba

Kipande cha ushahidi wenyewe thamani kubwa kuhusiana na Yesu kuepukana na Msalaba ambao mtu hawesi kujizua kuukubali ni changanyiko la dawa lijulikanalo kama Marham-i-Isa au "Marhamu ya Yesu" lililotajwa katika mamia ya vitabu vyatiba. Baadhi ya vitabu hivi vilitungwa na Wakristo, baadhi na Majusi na Mayahudi, baadhi na Waislamu. Vingi vyao ni vyatiba zamani sana. Uchunguzi unaonyesha kwamba mwanzoni changanyiko hilo lilipata kujulikana kama jambo la jadi miongoni mwa mamia ya maelfu ya watu. Kisha wakaliweka katika maandishi. Kwanza, wakati wa zama zile zile za Yesu, muda kidogo tu baada ya tukio la Msalaba, kitabu cha kifamasia kilitungwa kwa lugha ya Kilatini ambamo kulikuwa na kutajwa kwa changanyiko hili pamoja na taarifa kwamba changanyiko hilo lilitayarishwa kwa ajili ya vidonda vyatiba Yesu. Kisha, kitabu hiki kikatafsiriwa katika lugha kadhaa, hadi katika zama za Mamun-al-Rashid ambapo kilitafsiriwa katika lugha ya Kiarabu. Aidha ni kutokana na uingiliaji kati wa kimbingu wa ajabu kwamba matabibu mashuhuri wa dini zote - Wakristo, Mayahudi, Majusi na Waislamu - wote wamelitaja changanyiko hili katika vitabu vyao, na wanasema kwamba lilitayarishwa na wanafunzi kwa ajili ya Yesu. Usomaji sana wa vitabu vyatiba elimu ya utengenezaji madawa unaonyesha kwamba changanyiko hili ni la manufaa sana katika ajali ziletazo majeraha kutokana na mapigo au mianguko, kwa kuzuia mara moja mtiririko wa damu, na kwa vile linayo "manemane" pia ndani yake, kidonda hubakia bila usaha. Marhamu haya pia yanafaa sana katika kutibu ugonjwa wa tauni; ni mazuri kwa ajili ya majipu na vidonda vyatiba tumboni vyatiba aina zote. Lakini bado haiko wazi iwapo marhamu haya yalitayarishwa kutokana na ufunuo wa kimbingu alioupokea Yesu mwenyewe baada ya kupata mateso ya Msalaba, au kwamba yalitayarishwa baada ya mashauriano na baadhi ya matabibu.

Baadhi ya vichanganyizio vyake ni kama dawa halisi ya ugonjwa

mmoja: hususan "manemane" ambayo pia inatajwa katika Taurati. Kwa vyo vyote vile vidonda vya Yesu vilipona kwa muda wa siku chache tu kwa kutumia marhamu haya. Ndani ya kipindi cha siku tatu alipona vya kutosha na kupata uwezo wa kutembea maili sabini kwa mguu kutoka Yerusalem hadi Galilaya. Hivyo basi, kuhusu nguvu ya changanyiko hili inatosha tu kusema kwamba wakati Yesu aliwaponya watu wengine, changanyiko hili lilimponya yeye! Vitabu vilivyoweka kumbukumbu ya ukweli huu vinafikia idadi ya zaidi ya elfu moja. Kuvitaja vyote itakuwa orodha ndefu sana. Isitoshe, kwa vile matumizi ya dawa hii yanajulikana sana mionganoni mwa matabibu wa Kiyunani (yaani wale waliobobea katika madawa ya kale ya Kigiriki), sioni haja ya kutaja majina ya vitabu vyote hivi; naorodhesha hapa chini majina ya vichache tu ambavyo vinapatikana hapa.:-

**Orodha ya Vitabu vyenye mtajo wa Marham-i-Isa, na taarifa
kwamba Marham hayo yalitayarishwa kwa ajili ya Yesu,
yaani kwa ajili ya vidonda vya mwilini mwake**

Qanun; kilichotungwa ba Shaikur - Rais Bu Ali Sina, Jalada la 3, Ukurasa 133;

Sharah Qanun; kilichotungwa na Allama Qutbud-Din Shirazi, Jalada la 3;

Kamil-us-Sanaat; kilichotungwa na Ali Bin-al-Abbas Al-Majuusi, jalada la 3, ukurasa 602;

Kitab Majmua-i-Baqai; Mahmud Muhammad Ismail, Mukhatif az Khaqan, kilichotungwa na Khitab pidar Muhammad Baqa Khan, Jalada la 2 ukurasa 497;

Kitab Tazkara-i-Ul-ul-Albab; kilichotungwa na Shaikh Daud-ul-Zariirul - Antaki, ukurasa 303;

Qarabadin-i-Rumi; kilichotungwa karibuni wakati ule ule wa zama za Yesu na kutafsiriwa kwa Kiarabu wakati wa utawala wa Mamun al-Rashid, tazama Maradhi ya Ngozi;

Umdat-Ul-Muhtaj; kilichotungwa na Ahmd Bin Hasan al-Rashid al-Hakim. Katika kitabu hiki, *Marham-i-Isa* na machanganyiko

mengine yameandikwa kutoka katika vitabu mia moja, pengine zaidi ya mia moja, vitabu vyote hivi vikiwa katika lugha ya Kifaransa. *Qarabadin*, kwa lugha ya Kiajemi, kilichotungwa na Hakim Muhammad Akbar Arzani-Maradhi ya Ngozi; *Shifaaul-Asqaam*, Jalada la 2 ukurasa 230; *Miratush - Shafaa*, kilichotungwa na Hakim Hatho Shah (muswada) Maradhi ya Ngozi; *Zakhira-i-Khawarazm Shahi*, Maradhi wa Ngozi; *Sharah Qanun Gilani*, Jalada la 3; *Sharha Qanun Qarshi*, Jalada la 3; *Qarabadin*, kilichotungwa na Ulwi Khan Maradhi ya Ngozi; *Ilajul-Amraz*, cha Hakim Muhammad Sharif Khan Sahib, ukurasa 893; *Qarabadin, Unani* - Maradhi ya Ngozi; *Tuhfatul Mu'miniin*, kwenye nafasi ya pemberi ya Makhzanul-Adwiya, ukurasa 713; *Muhit Fi-Tibb*, ukurasa 367. *Aksir-i-Azam*, jalada la 4, kilichotungwa na Hakim Muhammad Azam Khan Sahib, Al Mukhatab ba Nazim-i-Jahan, ukurasa 331; *Qarabadin*, kilichotungwa na Masumi-ul-Masumi bin Karamu-Din Al-Shustri Shirazi; *Ijala-i-Nafiah*, Muhammad Sharif Dehlavi, ukurasa 410; *Tibb-i-Shibri*, kwa jina jingine kijulikanacho kama Lawami Shibriyya. Syed Hussain Shibri Kazimi, ukurasa 471; *Makhzan-i-Sulaimani*, tafsiri ya Aksir Arabi, ukurasa 599, kilichotungwa na Muhammad Shamsud-Din Sahib wa Bahawalpur. *Shifaaul-Amraz*, kilichotafsiriwa na Maulana Al-Hakim Muhammad Nuur Karim, 282; *Kitab Al-Tibb Dara Shakohi*, kilichotungwa na Nurud-Din Muhammad Abdul Hakim, Ainul-Mulki Al-Shirazi, ukurasa 360; *Minhajud-Dukan ba Dastuurul-Aayan fi Aamal wa Tarkib al-Nafiah Lil-Abdan*, kilichotungwa na Aflatuun-i-Zamana wa Rais-i-Awana Abdul-Mina Ibn Abi Nasrul-Atta Al Israili Al-Haruuni (Yaani Myahudi), ukurasa 86,

Zubdatut-Tibba, kilichotungwa na Syedul-Imam Abu Ibrahim Ismail bin Husaini Al-Jarjani, ukurasa 182;

Tibb-i-Akbar, kilichotungwa na Muhammad Akbar Arzani, ukurasa 242.

Mizan-ul-Tibb; kilichotungwa na Muhammad Akbar Arzani, ukurasa 152;

Sadidi, kilichotungwa na Raisul-Mutakaalimin Imamul-Muhaqqiqiin *As-Sadidul-Kazruuni*, Jalada la 2 ukurasa 283;

Hadi Kabir, kilichotungwa na Ibni Zakariya, Maradhi ya Ngozi;

Qarabadin, kilichotungwa na Ibni - Talmiz, Maradhi ya Ngozi;

Qarabadin, kilichotungwa na Ibni - Abi, Sadiq, Maradhi ya Ngozi.

Vitabu hivi vimetajwa hapa kwa njia ya kielelezo. Watu walio wasomi, hususan matabibu, wanajua kwamba vingi mionganini mwa vitabu hivi, katika zama za kale vilifundishwa katika sehemu muhimu za mafunzo chini ya utawala wa Kiislamu; hata wanafunzi kutoka Ulaya walijifunza vitabu hivyo. Ni jambo la uhakika, na hakuna kutia chumvi walau kidogo tu, kwamba katika kila karne kumekuwako na mamilioni ya watu ambao walikuwa wanavijua vitabu hivi; mamia ya maelfu ya watu hao wamekuwa wakivisoma vitabu hivyo kwa mfululizo. Naweza kudai kwamba hakuna mtu walau mmoja tu mionganini mwa wasomi wa Ulaya na Asia ambaye alikuwa hajajua walau baadhi ya majina ya vitabu vilivyomo katika orodha iliyojajwa hapo juu. Wakati Hispania na Qastmonia na Shantrin zilipopata vyuo vikuu, Qanun kuu ya Bu Ali Sina, kitabu maarufu cha tiba ambamo yamepangwa vizuri matumizi ya Marham-i-Isa, na vitabu vingine kama vile Shifaa na Isharat na Basharat kuhusu sayansi, elimu ya nyota na falsafa, vilisomwa kwa hamu na kufunzwa na Wazungu. Kadhalika, vitabu vya Abu Nasr Farabi, Abu Raihan, Israil, Thabit bin Qurrah, Hunain bin Ishaq na kadhalika - vitabu vyote maarufu vya mafunzo - tafsiri zilizofanywa na watu hao kutoka Kigiriki pia zilifundishwa.

Tafsiri za vitabu vyao bila shaka zitakuwa bado zinapatikana huko Ulaya hadi leo. Kwa vile watawala wa Kiislamu walikuwa wafadhili hodari wa mambo ya tiba, walitayarisha tafsiri za vitabu vizuri

vya Kigiriki.

Ukhalifa ambao ndio mamlaka ya juu, kwa muda mrefu ulibaki mikononi mwa wafalme ambao walitamani kuipanua elimu kuliko kuendeleza tawala zao. Hii ndiyo sababu siyo tu vitabu vya Kigiriki vilitafsiriwa kwa lugha ya Kiarabu bali pia waliwaalika makuhani wa Kihindu kutoka India, na wakawafanyisha kazi ya kutafsiri vitabu vya tiba na vinginevyo, wakiwalipa marupurupu makubwa. Kwa hiyo moja ya madeni makubwa ambayo watafutaji elimu ya kweli wanadaiwa na watu hao, ni hili ya kwamba walitayarisha tafsiri za Kilatini na Kigiriki za vitabu vya tiba ambavyo vilikuwa na mtajo wa "Marhamu ya Yesu", na ambavyo, takriban kama mchoro, vimeurikodi ukweli huu kwamba marhamu yale yalitayarishwa kwa ajili ya vidonda vya Yesu. Wakati wasomi wa zama za Kiislamu kama vile Thabit bin Qurrah na Hunain bin Ishaq ambao licha ya kuwa na elimu ya tiba, walibobea katika Sayansi na falsafa, waliitafsiri Qarabadin ambamo mlikuwa na mtajo wa Marham-i-Isa, walilihadhi kwa busara neno *Shailikha* kwa herufi za Kiarabu ili kuendeleza ule muashirio kwamba kitabu kile kilitafsiriwa kutoka katika maandiko ya kifamasia ya Kigiriki. Hii ndiyo sababu takriban katika kila kitabu linatokea neno *Shailikha*.

Isitoshe, ni jambo la kuzingatia kwamba ingawa sarafu za zamani zina thamani kubwa, kama itokeavyo kwamba zinafumbua mafumbo ya kihistoria, hata hivyo, vitabu vya kale ambavyo kwa nyakati zote vimeduwa vikijulikana kwa mamilioni ya watu na ambavyo vimeduwa vikifundishwa kama vitabu vya mafunzo kwenye vituo vikubwa vya elimu na bado vinaendelea kutekeleza kusudio hilo, ni vyenye thamani mara elfu moja zaidi kuliko sarafu na michoro. Kwani, kwa upande wa sarafu na michoro upo uwezekano wa udanyanyifu pia. Vitabu vya elimu ambavyo tangu wakati wa kutungwa kwao vimeduwa vikijulikana na mamilioni ya watu na vimehifadhiwa na kulindwa na mataifa yote na vinaendelea kulindwa hadi leo, ni ushahidi ulio na thamani kiasi hiki kwamba sarafu na michoro havina cho chote cha kulinganishia na hivyo. Naataje mtu ye yote kama anaweza, sarafu au mchoro

ambao umepata kujulikana na watu wengi kama Qanun ya Bu Ali Sina.

Kwa kifupi, "Marham ya Yesu" yanajemga kipande cha ushahidi muhimu sana kwa ajili ya watafutaji ukweli. Kama ushahidi huu usiaminike, ushahidi wote wa kihistoria ni lazima ukataliwe, kwani, licha ya idadi ya vitabu vya namna hiyo ambavyo vina mtajo wa Marham-i-Isa kuwa elfu moja au zaidi hivyo na watunzi wa hivyo wanajulikana na mamaillioni ya watu. Yule ambaye hataukubali uthibitisho huu ulio bayana na ulio wazi na wenye nguvu ni lazima auchukie uthibitisho wote utokanao na historia. Je anaweza kuthubutu kupuuza kipande cha ushahidi wenye nguvu kama huu? Je tunaweza sisi kutilia shaka ushuhuda huu mzito ambao umesambaa Ulaya na Asia na ambao ni matokeo ya kauli za wanafalsafa maarufu - Mayahudi, Wakristo, Majusi na Waislamu?

Hivyo basi, enyi wachunguzi waadilifu uangalieni ushuhuda huu: Ukimbilieni uthibitisho huu adhimu na kuutafakari. Je ushahidi kama huu wenye kung'ara unastahili kupuuzwa? Je hatupendi "Uhai" kutoka katika "Jua" hili la ukweli? Ile rai kwamba Yesu aweza kuwa ameyapata baadhi ya majeraha kabla ya wakati wa kuitwa kwake au kwamba yaweza kuwa majeraha yaliyopatikana kipindi fulani wakati wa mahubiri yake lakini si kutokana na kusulubishwa; kwamba mikono na miguu yake yaweza kuwa iliumizwa kutokana na sababu zingine; kwamba aweza kuwa alianguka kutoka kwenye paa na marham yaweza kuwa yalitayarishwa kwa ajili ya majeraha aliyoyapata katika mwanguko huu, ni ya kipuuzi. Ni ya kipuuzi kwa sababu kabla ya kuchaguliwa kwake kuwa Mtume hakuwa na wanafunzi, ambapo sambamba na kutajwa kwa marham hayo wametajwa pia wanafunzi. Neno *Shailikha*, ambalo ni neno la Kigiriki bado linapatikana katika vitabu hivi. Zaidi ya hayo, kabla ya kutangaza utume wake Yesu hakuhesabiwa kuwa mtu muhimu wa kiasi hiki kwamba matukio ya maisha yake yawe yanarikodiwa. Kazi yake ya mahubiri ilidumu kwa kipindi cha miaka mitatu na nusu tu, na wakati wa kipindi hiki hakuna ajali au jeraha lililoripotiwa katika kumbukumbu kumhusu yeeye isipokuwa tukio

la Msalaba.

Lakini kama mtu ye yote ana maoni kwamba Yesu aliyapata majeraha haya kutokana na sababu zingine, ni juu yake kuleta uthibitisho kwani tukio ambalo tumelirejea linathabitika na kukubalika kwa kiasi hiki kwamba si Myahudi wala Mkristo wawezao kulikana hilo tukio, yaani, la Msalaba. Lakini, wazo la Yesu kuwa alijeruhija kutokana na sababu zingine halijashuhudiwa na kumbukumbu yo yote ya kihistoria. Kwa hiyo, kukaribisha wazo kama hilo ni kuiacha njia ya ukweli kwa kujua. Uthibitisho ambao umekwisha tolewa si ule ambao unaweza kukataliwa kwa kutegemea rai ya kipuuzi kama hiyo.

Ipo miswada ambayo inapatikana hata leo; mimi pia ninayo nakala ya zamani ya Qanun Bu Ali Sina ya zama zile, iliyoandikwa kwa mkono. Kwa hiyo, litakuwa jambo la dhuluma kubwa - itakuwa ni kuuchinja ukweli moja kwa moja - kutupilia mbali uthibitisho ulio wazi kama huu. Ufikirieni tena na tena - tafakarini kwa kina kuuhusu huo - Vitabu hivi bado viko mikononi mwa Mayahudi, Majusi, Wakristo, Waarabu, Waajemi, Wagiriki, Warumi, Wajerumani na Wafaransa, na vile vile katika maktaba za kale za nchi nyingine za Ulaya na Asia. Je ni sawa kuuacha uthibitisho kama huu ambao nuru yake hulitia kiwi jicho la ukanaji? Kama vitabu hivi vingekuwa vimetungwa na Waislamu tu, na kama vingekuwa mikononi mwa wafuasi wa Islam, kungeweza kuwa na watu ambao wangeamua kwa pupa kwamba Waislamu walighushi taarifa hii na kuirikodi kwenye vitabu vyao ili kuifanya iwe shambulio dhidi ya imani ya Kikristo. Lakini hii, licha ya sababu nitakazotaja hivi punde, ni fikra isiyokuwa na msingi pia kutokana na ukweli kwamba Waislamu kamwe wasingekuwa na hatia ya kughushi kwa namna hii; kwani, kama walivyo Wakristo, Waislamu pia wanaamini kwamba baada ya tukio la Msalaba Yesu ghafla akapaa mbinguni. Zaidi ya hayo Waislamu hawaamini kwamba Yesu aliwekwa Msalabani kwa vyo vyote vile au kwamba alipata majeraha yo yote kutokana na kusulubiwa. Yawezekanaje sasa watengeneze kwa makusudi taarifa ya kughushi ambayo iko kinyume na imani yao? Isitoshe, Islam haikuwapo ulimwenguni

wakati vitabu hivi vya tiba, kwa lugha ya Kilatini na Kigiriki, vilipokuwa vinatungwa na kusambazwa mionganoni mwa mamia ya maelfu ya watu; vitabu ambavyo vilikuwa na maelekezo ya matumizi ya "marhamu ya Yesu" na pia maelezo kwamba marhamu haya yalitayarishwa na wanafunzi wa Yesu (amani juu yake). Na wale watu, yaani, Mayahudi, Wakristo, Waislamu na Majusi walikuwa wakipingana wao kwa wao katika mambo ya dini. Kwa hiyo, ule ukweli kwamba warneyataja marhamu haya katika vitabu vyao, au tuseme, ule ukweli kwamba hawajiali hata dini zao mbalimbali, ni uthibitisho ulio wazi kwamba utayarishaji wa marhamu hayo ulikuwa ni ukweli unaojulikana kwa kiasi hiki kwamba haukukanwa na jumuiya au taifa lo lote. Lakini ni kweli, kwamba hadi kufikia wakati wa kutokea kwa Masihi Aliyahidiwa, haikutokea kwa ye yote mionganoni mwa watu hawa kufaidika na dawa hii ambayo imetajwa katika mamia ya vitabu na ilijulikana kwa mamilioni ya watu wa mataifa mbalimbali. Kwa hiyo hatuna njia nyingine isipokuwa kukubali kuhusiana na jambo hili kwamba Mwenyezi Mungu Alitaka - ilikadirwa na Yeye - kwamba silaha hii yenye kung'ara na hoja hii yenye kufichua ukweli ambayo inateketeza ile imani kuhusu msalaba iechezwe ulimwenguni na Masihi Aliyahidiwa; kwani Mtukufu Mtume s.a.w. alitabiri kwamba Imani ya Msalaba haitapungua wala maendeleo yake hayatasimamishwa hadi Masihi Aliyahidiwa atakaptokea ulimwenguni. Ilikuwa ni Masihi Aliyahidiwa ambaye mikononi mwake ulikuwa usababishwe "Uvunjaji wa Msalaba". Kidokezo katika utabiri huu kilikuwa kwamba katika zama za Masihi Aliyahidiwa Mwenyezi Mungu Angeleta mazingira ambayo yangeweka wazi ukweli kuhusu tukio la msalaba. Kisha mwisho ungekuja, na Imani ya msalaba ingekamilisha kipindi cha uhai wake, siyo lakini, kwa njia ya vita na vurugu, bali kwa njia ya wakala za kimbingu tu, ambazo zingejidhihirisha ulimwenguni kwa sura ya hoja na ugunduzi. Hii ndiyo maana ya Hadithi iliyotajwa na Bukhari na wengineo. Kwa hiyo ilikuwa lazima kwamba zisizifichue thibitisho hizi na vipande hivi vya ushahidi usio na shaka mpaka zama za kutokea kwa Masihi Aliyahidiwa. Na hivyo

macho yatafunguka na watu wenye kufikiri watadadisi kuhusu swali hili. Kwani Masihi wa Mwenyezi Mungu ameshatokea.

Akili ni lazima sasa zinolewe; nyoyo ni lazima ziwe zingativu; kalamu zishikwe kwa nguvu, na wote ni lazima wajifunge vibwebwe. Nyoyo za kiuchamungu hivi sasa zitapewa ufahamu, na kila mtu aliye tayari atapata akili. Kwani, kila king'aacho mbinguni huimulika dunia pia. Aliyebarikiwa na mwenye bahati nzuri ni yule ambaye anayo hisa ya nuru hii! Kama vile tunda linavyotokea kwa msimu, kadhalika Nuru nayo hushuka kwa wakati wake uliowekwa; hakuna awezaye kuiteremsha kabla haijashuka yenyewe, wala kuizua wakati inaposhuka. Hitilafu na mabishano ni lazima yawepo. Lakini, mwishowe ukweli ni lazima utashinda, kwani hii siyo kazi ya binadamu; mwana wa binadamu hana hisa humo - unatoka kwa Mwenyezi Mungu ambaye hubadilisha misimu, Huzisogeza nyakati na Huugeuza usiku kuwa mchana na mchana kuwa usiku. Ameumba giza lakini Anapenda nuru. Anaiachia Shirki (Imani ya kuwepo miungu wengi) ipatikane ulimwenguni, lakini anapenda Tauhidi au Umoja Wake Mwenyewe; Hapendi utukufu wake kutolewa kwa mtu mwingine ye yote. Tangu kuzaliwa kwa binadamu, na mpaka binadamu atakapotoweka ulimwenguni, Sheria ya kimbingu ni hii ya kwamba Mwenyezi Mungu Anadumisha Tauhidi au Umoja Wake. Lengo la Manabii wote waliioletwa na Yeye lilikuwa kufuta kuabudiwa kwa binadamu na viumbe vingine na kuanzilisha kuabudiwa kwa Mwenyezi Mungu. Huduma waliyoitoa ulimwenguni ilikuwa kuifanya hii kanuni "Hakuna apasaye kuabudiwa isipokuwa Allah" ing'are ulimwenguni kama inavyong'ara mbinguni. Kwa hiyo mbora wao ni yule ambaye alifanya kazi kubwa zaidi ya kuifanya kanuni hii ing'are kwa kumetameta; ambaye kwanza aliweka wazi udhaifu wa miungu ya uwongo na kuthibitisha kutokuwa cho chote kwa miungu hiyo, kwa misingi ya akili na uwezo, na kisha alipokwisha thibitisha kila kitu, aliacha ukumbusho na ushindi wake dhahiri kwa sura ya hii Kalima: Hakuna Mungu isipokuwa Allah, Muhammad ni Mtume wa Allah." Hakuitamka Kalima hii: "Hakuna Mungu isipokuwa Allah" ikiwa madai matupu; bali kwanza alitoa vithibitisho

na kubainisha kosa la imani za uwongo na kisha akawaita watu waje washuhudie kwamba hakuna Mungu kinyume cha yeye Ambaye Alizivunja nguvu zao zote na Ambaye Alikivunjavunja kiburi chao chote. Kwa hiyo, ikiwa kama ukumbusho wa ukweli huu uliothibitika, akafundisha kalima hii iliyobarikiwa: "Hakuna Mungu isipokuwa Allah; Muhammad ni Mtume wa Allah".

SURA YA 4

USHAHIDI KUTOKA KWENYE VITABU VYA HISTORIA


Kwa kuwa sura ifuatayo imehodhi ushahidi wa aina mbalimbali, kwa ajili ya kuweka wazi mfuatano wa mambo, imegawanywa katika sehemu chache ambazo zinapangwa hapa chini:

SEHEMU YA 1

Ushahidi kutoka katika vitabu vya Kiislamu kutaja safari ya Yesu.

Katika Rauzat-us-Safa, kitabu kijulikanacho sana cha historia kwenye ukurasa wa 130-135 panajitokeza taarifa kwa lugha ya Kiajemi ambayo ikitafsiriwa kwa muhtasari ni kama ifuatavyo:

Isa (amani juu yake) aliiwta "Masihi" kwa sababu alikuwa msafiri mkubwa. Alivaa shali ya hariri kichwani mwake, na mgolole wa hariri mwilini mwake. Alikuwa na fimbo mkononi mwake; alikuwa na tabia ya kutembea tembea kutoka nchi moja hadi nyingine na kutoka mji moja hadi mwingine. Usiku ulipoingia alitulia mahala alipokuwa. Alikula mimea ya porini, na aliendelea na safari zake kwa mguu. Katika moja ya misafara yake, Masahaba zake wakati mmoja walimnunulia farasi; siku moja akampanda huyo farasi, lakini kwa vile hakuweza kuandaa masurufu kwa ajili ya kumlisha farasi huyo, akamrudisha. Akisafiri kutoka nchini mwake aliwasili Nasibain, mji ambao ulikuwa kwenye umbali wa maili mia chache kutoka nyumbani kwake. Pamoja naye walikuwepo wachache mionganini mwa wanafunzi wake ambao aliwatuma mjini kwenda kuhubiri. Lakini huko mjini kulikuwako na uvumi mpya mpya ambao ni wa uwongo na usiokuwa na msingi kuhusu Isa (amani ya Mungu juu yake) na mama yake. Kwa hiyo gavana wa ule mji aliwakamata hao wanafunzi na kisha kumwita Yesu. Yesu aliwaponya baadhi ya watu kimiujiza na kuonyesha miujiza mingine.



Kwa hiyo mfalme wa jimbo la Nasibain pamoja na majeshi yake yote na watu wake, akawa mfuasi wake.

Kile kisa cha "kuteremka kwa chakula" kilichomo ndani ya Qur'an Tukufu ni cha zile zama za misafara yake.

Hii kwa kifupi, ndiyo taarifa ya Rauzat-us-Safa. Lakini, mtumzi wa kitabu hicho amenasibisha kwa Yesu miujiza mingi ya kipuuzi na isiyoingia akilini ambayo sitaitaja hapa, na kwa kuiachanisha na uwongo na utiaji chumvi wa kipuuzi, naligeukia suala halisi la mjadala ambalo linaongoza kwenye uamuzi kwamba Isa (amani juu yake) wakati wa safari zake aliwasili Nasibain. Hii Nasibain ni mahali kati ya Mosul na Syria ambapo katika ramani za Kiingereza pametwa Nasibus. Kama mtu anasafiri kutoka Syria kwenda Uajemi, atapita Nasibain, ambao upo kwenye umbali wa maili 450 kutoka Yerusalem: Mosul uko takriban maili 48 kutoka Nasibain na maili 500 kutoka Yerusalem. Mpaka wa Uajemi uko umbali wa maili 100 tu kutoka Mosul. Hii ina maana kwamba Nasibain uko maili 150 kutoka mpakani mwa Uajemi. Mpaka wa Mashariki wa Uajemi unaugusa mji wa Herat katika Afghanistan, yaani Herat uko katika mpaka wa Magharibi wa Afghanistan kuelekea upande wa nchi ya Uajemi na uko takriban maili 900 kutoka mpaka wa Magharibi wa Uajemi. Kutoka Herat hadi kwenye Mlangobahari wa Khayber umbali wake ni kama maili 500 hivi. Ifuatayo hapa ndiyo ramani inayonyesha ile njia aliyoifuata Isa.

Ramani hii inaonyesha njia aliyoitumia Yesu katika safari yake ya Kwenda Kashmir. Lengo la safari hii lilikuwa kwamba aweze kukutana na Waisraeli ambao mfalme Shamasenser aliwakamata mateka na kuwapelekea Media. Itaonekana kwamba kwenye ramani zilizochapishwa na Wakristo, Media unaonyshwa kuelekea Kusini kwa Bahari ya Khizar (Avoz), ambapo hivi sasa ni Uajemi. Mpaka wa Mashariki wa Uajemi unatangamana na Afghanistan; kuelekea Kusini ipo bahari na kuelekea Magharibi ipo Dola ya Kituruki. Kama taarifa iliyomo katika Rauzat-us-Safa ni sahihi inelekea kwamba, kwa kwenda Nasibain Yesu alikusudia kuja Afghanistan kupitia Uajemi, na kuwaita kwenye ukweli. Mayahudi waliopotea ambao wakaja kujulikana kama Waafghani.

Neno "Afghan" laelekea kuwa na asili ya Kiebrania; na neno lilitotokana na neno jingine ambalo maana yake ni "shujaa". Yaeleeka kwamba kwenye kilele cha ushindi wao wakajichagulia jina hili¹.

Kwa kifupi; Yesu alikuja Punjab baada ya kupitia Afghanistan akiwa na kusudio la asili la kwenda Kashmir baada ya kuiona nchi ya Punjab na Hindustan. Itaonekana kwamba Chitral na ukanda wa Punjab vinatenganisha Kashmir na Afghnistan. Kama mtu atasafiri kutoka Afghnistanwa kwenda Kashmir kupitia Punjab, mtu huyo atatembea umbali wa maili 80 au kiasi cha kilometra 135.

Lakini kwa busara, Yesu akachagua njia ya kupitia Afghanistan ili kwamba yale makabila yaliyopotea ya Israeli yajulikanayo kama Waafghani nayo yaweze kufaidika naye. Mpaka wa Mashariki wa Kashmir unagusa Tibet. Kutoka Kashmir angaliweza kwenda kwa urahisi hadi Tibet na baada ya kufika Punjab hakuwa na ugumu wa kuzizungukia sehemu muhimu za Hindustan kabla ya kwenda Kashmir na Tibet. Kwa hiyo inawezekana sana, kama baadhi ya

¹Katika Taurati kulikuwako na ahadi kwa Mayahudi, kwamba kama wangemwamini nabii wa "mwisho" wangepewa ufalme na utawala, baada ya kupitia kwenye mteso mengi. Ahadi ile ilitimilizwa kwa yale makabila kumi ya Israeli kuukubali Uislamu. Hii ndiyo sababu kumekuwako wafalme wakubwa mionganoni mwa Waafghani na pia mionganoni mwa Wakashmiri.

Ipo barua katika sehemu ya 14 ya Sura ya Kwanza ya Historia kwa Kigiriki "Imani ya Eusebio" iliyotafsiriwa na Mlondon mmoja aitwaye Heinmer mnamo mwaka 1650 kwa kalenda ya Kikristo, ambayo inaonyesha kwamba mfalme mmoja aitwaye Abgerus alimwita Yesu kutoka nchi ilio ng'ambo ya mto Euphrates, kwenye Ikulu yake. Barua iliyopelekwa na Abgerus kwa Yesu, na majibu yake, zimejawa na uwongo na utiaji chumvi mwangi sana. Lakini hili moja laonekana kuwa ni la kweli, kwamba mfalme yule, baada ya kuarifiwa kuhusu ukatili wa Mayahudi alimwita Yesu kwenye Ikulu yake ili ampe hifadhi. Yumkini mfalme huyo aliamini kwamba alikuwa nabii wa kweli.

kumbukumbu za zamani za kihistoria za nchi hii zinavyoonyesha, kwamba Yesu aweza kuwa aliona Nepal, Benares na sehemu zingine. Kisha hana budi alikwenda Kashmir kuititia Jammu na Rawalpindi. Kwa kuwa yeye alikuwa mwenyeji wa nchi ya baridi, ni jambo la yakini kwamba alikaa kwenye majimbo haya wakati wa kipupwe tu, na ilipofikia mwishoni mwa mwezi wa Machi au mwanzoni mwa Aprili hana budi alianza kuelekea Kashmir. Kwa vile Kashmir inafanana na Shamu ni lazima awe alichagua makazi yake ya kudumu katika nchi hii. Aidha yawezekana kwamba aweza kuwa alikaa kwa kipindi fulani nchini Afghanistan. Si jambo lisilowezekana kwamba aweza kuwa alioa katika nchi ile. Mojawapo mionganini mwa makabila ya Waafghani linajulikana kama "Isa Khel" - halitakuwa jambo la kushangaza iwapo hao ni wazao wa Yesu. Lakini ni jambo la kusikitisha kwamba historia ya Waafghani ipo katika hali ya vurugu; kwa hiyo ni vigumu kufikia kwenye jambo lo lote la uhakika kwa kusoma taarifa zao za kikabila. Lakini hakuna shaka, kwamba Waafghani ni Waisraeli kama walivyo Wakashmiri. Wale ambao wamechukua maoni yaliyo tofauti na haya kwenye vitabu vyao wamepotezwa kupotea kwa hali ya juu; hawakulichunguza jambo hili walau kwa dakika moja. Waafghani wanakiri kwamba wao ni wazao wa Qais; na Qais ni mtu wa Israel. Lakini si lazima kuendeleza mjadala huu hapa. Nimekwisha lishuhgulikia suala hili kikamilifu katika kimoja mionganini mwa vitabu vyangu; hapa, ninatoa taarifa ya safari ya Yesu kuititia Nasibain, Afghanistan, Punjab na kuendelea hadi Kashmir na Tibet. Aliitwa "nabii mwenye kusafiri, la bali kiongozi wa wasafiri", kutokana na safari hii iliyo ndefu sana.

Mwanachuo mmoja wa Kiislamu, yaani, Ibn-al-Walid Al-Fahri At-Tartuushi Al-Maliki, ambaye alitukuzwa kwa ajili ya kisomo chake, anasema kumhusu Yesu kwenye ukurasa wa 6 wa kitabu chake *Siraajul-Muluk*, kilichochapishwa na Matbaa Khairiya ya Misri mnamo mwaka 1306 A.H.:

"Yuko wapi Isa, aliye Ruhullah, na Kalimatullah, ambaye alikuwa kiongozi wa wachamungu na chifu wa wasafiri?" akimaanisha kwamba alikuwa amekufa, na kwamba, hata mtu mkubwa kama

yeye aliondoka katika ulimwengu huu. Ni lazima izingatiwe kwamba msomi huyu mwenye mamlaka anamwita Yesu siyo tu "Msafiri" bali "Kiongozi wa wasafiri". Kadhalika kwenye ukurasa wa 461 wa Lisaanul-Arabi imesemwa:

Yesu aliitwa "Masihi" kwa sababu alisafiri huku na huko, na kwa sababu hakukaa katika sehemu moja." Taarifa hiyo hiyo imerikodiwa katika Tajul-Urus Sharah Qamus. Humo imesemwa pia kwamba "Masihi" ni yule ambaye amepewa wema na baraka, yaani amepewa sifa hizi kwa kiwango cha namna hii kwamba hata mguso wake umebarikiwa; na kwamba jina hili lilitolewa kwa Yesu, kwani Mwenyezi Mungu Humpa jina hili ye yote Amtakaye. Kinyume na huyu, yuko "Masihi" mwininge, ambaye mguso wake ni mwovu na wenyewe laana, yaani, asili yake iliumbwa kwa laana na uovu, kwa kiasi hiki kwamba mguso wake unaleta giza la uovu na giza la laana. Jina hili lilitolewa kwa yule Masihi ambaye ni Dajjal na kwa wale wote ambao wanafanana na yeye. Aidha haya majina mawili, yaani Masihi mwenye kusafiri na Masihi Aliyebarikiwa si yenye kipingana. Moja halilibatilishi lenzie. Kwani, ni desturi ya kimbingu kwamba Mwenyezi Mungu Humwita mtu kwa zaidi ya njia moja na kwamba majina yote ya namna hiyo yanamhusu yeye. Kwa kifupi, katika hali ya kuwa msafiri, Yesu amethibitishwa vizuri sana na historia ya Kiislamu hivi kwamba kama rejea zote zitanakiliwa kutoka kwenye vitabu vile nadhani zitasababisha kupatikana wa lijitabu likubwa sana. Kwa hiyo niliyoyasema yanatosha.

SEHEMU YA 2

Ushahidi kutoka kwenye vitabu vya Kibuddha.

Naiwe wazi kwamba maandiko matakatifu ya Kibuddha yametupatia ushahidi wa aina mbalimbali ambao kwa jumla unatosha kuthibitisha kwamba Yesu (amani juu yake) lazima alikuja Punjab na Kashmir n.k. Nauratibu ushahidi huo humu ili watu waadilifu kwanza waweze kuusoma, na kisha kwa kuupanga katika akili zao kama taarifa iliyoungana, waweze wao wenyewe kufikia kwenye uamuzi uliokwisha semwa. Ushahidi huo ni huu hapa. Kwanza: majina aliyopewa Buddha yanafanana na majina aliyopewa Yesu. Kadhalika, matukio ya maisha ya Buddha yanalingana na yale ya maisha ya Yesu. Lakini rejea ya hapa inahu Dini ya Kibuddha ya sehemu zilizopo ndani ya mipaka ya Tibet, kama vile Leh, Lhasa, Gilgit na Hams n.k., ambazo ndizo sehemu zilizothibitika kuwa zilitembelewa na Yesu. Kuhusiana na kufanana majina, inatosha kuonyesha kwamba, iwapo kwa mfano Yesu (amani juu yake) anajita "Mwanga" katika mafundisho yake, vivyo hivyo Gautama ameitwa Buddha, ambalo kwa lugha ya Sanskrit lina maana ya "Mwanga"¹. Iwapo Yesu ameitwa "Bwana"² katika Injili, vivyo hivyo Buddha ameitwa *Sasta* au "Bwana". Kama Yesu ameitwa "Mbarikiwa" katika Injili, vivyo hivyo Buddha ameitwa *Sugt*, yaani, "Mbarikiwa". Kama Yesu ameitwa "Mwanamfalme" vivyo hivyo Buddha naye ameitwa "Mwanamfalme. Yesu ameelezewa pia na Injili kama mtu ambaye anatimiliza shabaha ya kuja kwake. Vivyo hivyo Buddha naye katika maandiko matakatifu ya Kibuddha ameitwa *Siddhartha*, yaani, "mtu anayetimiliza shabaha ya kuja kwake". Yesu pia ameitwa na Injili "Kimbilio la waliochoka". Vivyo hivyo katika maandiko matakatifu ya Kibuddha, Buddha ameitwa *Asar Sarn*, yaani "Kimbilio la wasiokuwa na mahali pa kukimbilia." Na Yesu ameitwa pia "Mfalme" na Injili, ingawa yeeye alilitafsiri hilo kuwa

1. Kitabu cha Sir M. M. William, Buddhism, Ukurasa wa 23
2. Kitabu cha Sir M. M. William, Buddhism, Ukurasa wa 23

na maana ya "mfalme" wa Ufalme wa Mbingu. Vivyo hivyo Buddha naye ameitwa "Mfalme". Kufanana kwa matukio kunathibitishwa na matukio kama haya: Kama vile Yesu alivyoshawishiwa na shetani kwa utajiri na ufalme wa ulimwengu ilmuradi tu amsujudie, kadhalika Buddha naye alishawishiwa na Shetani alipomwambia kwamba atampatia fahari na utukufu wa wafalme kama angeachana na maisha yake ya upweke na kurudi nyumbani. Lakini, kama vile Yesu alivyokataa kumtii shetani, vivyo hivyo imerikodiwa kwamba Buddha naye hakumtii. Tazama *Buddhism* cha T.W. Rhys Davis; na *Buddhism* cha Sir Monier Monier Williams.¹

Hii inaonyesha kwamba majina yale yale anayojinasibisha nayo Yesu katika Injili, kadhalika yamenasibishwa kwa Buddha kwenye vitabu vya Kibuddha ambavyo vilitungwa muda mrefu baade; na, kama vile Yesu alivyoshawishiwa na Shetani, vivyo hivyo vitabu hivi vinadai kwamba Buddha naye alishawishiwa na Shetani la, bali taarifa ya kushawishiwa kwa Buddha kama ilivyoandikwa katika vitabu hivi ni ndefu kuliko ile taarifa ya kushawishiwa kwa Yesu katika Injili za Kikristo.

Imerikodiwa kwamba wakati shetani alipomtangulizia kishawishi cha utajiri na heshima ya kifalme, Buddha alielekea kurudi nyumbani. Lakini hakutii tamaa hii. Lakini Shetani huyo huyo akakutana naye tena katika usiku mmoja, akiwa amewaleta wazao wake wote, na kumtisha kwa sura za kuogopesha. Kwa Buddha mashetani hawa walionekana kama nyoka waliokuwa wakitema moto kutoka kwenye midomo yao. Hawa "nyoka" walianza kumtupia sumu lakini sumu yao ikageuzwa kuwa maua na ule moto ukafanya mduara wa nuru kumzunguka Buddha.

Huyo Shetani baada ya kutofanikiwa hivyo, akawaita kumi na sita mionganoni mwa mabinti zake na akawaomba wamdhahirishie Buddha uzuri wao, lakini Buddha bado hakutikisika. Shetani akashindwa katika hila zake. Akachagua njia zingine lakini hakuweza kufanya lo lote dhidi ya usimamaji Imara wa Buddha,

¹. Pia, tazama *Chinese Buddhism* cha Edkins; *Buddha*, cha Oldenberg, kilichotafsiriwa na W. Hoey; *Life of Buddha* kilichotafsiriwa na Rickhill.

ambaye aliendelea kupanda madaraja ya utakatifu ya juu na juu zaidi, na baada ya usiku mrefu, yaani baada ya majaribu makali na ya muda mrefu, alimshinda adui yake Shetani; "Mwanga" wa Elimu ya kweli ulimchomozea, sambamba na kufika kwa "asubuhi, yaani, mara tu baada ya majaribu yake kumalizika, akatokea kuyajua yote. Siku ambapo vita hii kubwa ilimalizika ilikuwa ni siku ya kuzaliwa kwa dini ya Kibuddha. Wakati huo Gautama alikuwa na umri wa miaka 35; aliitwa Buddha au "Mwanga" na ule Mti ambao chini yake alikuwa ameketi wakati ule, ukaja kujulikana kama "mti wa Mwanga". Hivyo, kama mtafungua na kuiangalia Biblia mtaona jinsi kushawishiwa kwa Buddha kunavyofanana na kushawishiwa kwa Yesu kwa kiasi hiki kwamba umri wa Buddha kwa wakati ule ulikuwa takriban sawa na umri wa Yesu. Na, kama inavyoonekana kutoka katika maandiko ya Kibuddha, yule Shetani hakujitokeza kwa Buddha katika hali ya kimwili inayoweza kuonekana. Ilikuwa shani iliyoona na Buddha tu; yale "mazungumzo" ya Shetani ni "ushauri mbaya uliotiwa moyoni mwa Buddha", yaani, yule Shetani alipojitokeza kwake, alitia ushauri katika moyo wa Buddha kwamba yeye (Buddha) aache njia yake, kwamba ni lazima amfuate yeye (Shetani), kwamba Shetani atampa utajiri wote wa ulimwengu. Kadhalika, imani ya madaktari wa Kikristo ni kwamba Shetani aliyejitokeza kwa Yesu hakuja kwake katika hali ya kimwili - hakuja kwa Yesu kama binadamu - mbele ya macho yale yale ya Mayahudi, akipita mitaani na vichochoroni akiwa katika mwili wenye umbo la kibinadamu na akizungumza na Yesu kwa namna ambayo angeweza kusikika na wale waliokuwapo. Kinyume cha hivyo, mkutano huo ulikuwa katika hali ya Kashf iliyoona na Yesu tu; yale mazungumzo pia yalikuwa katika hali ya ushauri uliotiwa moyoni, yaani Shetani, kama desturi yake alipenyeza ushauri mbaya katka moyo wake. Lakini Yesu hakukubali - aliukataa ushauri huo wa shetani.

Hivyo inafaa kutafakari kwa nini kulikuwako na kufanana kwingi kati ya Buddha na Yesu? Kuhusiana na jambo hili Maarya wanasema kwamba Yesu alizijua habari za dini ya Kibuddha

kutokana na safari zake nchini India, na baada ya kujipatia elimu kuhusu uhakika wa maisha ya Buddha, alitengeneza Injili yake kutokana na elimu hii aliporejea kwenye nchi yake ya uzalendo; kwamba Yesu alitunga mafundisho yake kimaadili kwa kuiba mafundisho ya kimaadili ya Buddha; kwamba kama vile Buddha alivyojita "Mwanga" na "Ujuzi" na kujipangia majina mengine - vivyo hivyo Yesu naye aliyanasibisha kwake majina yote hayo, kwa kiasi hiki kwamba hata ile hadithi ndefu ya kushawishiwa kwa Buddha ikachukuliwa na yeze. Lakini huu ni uzushi wa Maarya. Si kweli hata kidogo kwamba Yesu alikuja India kabla ya tukio la Msalaba; hakuwa na haja ya kufunga safari kama hiyo wakati ule - alikuwa na haja ya kufunga safari kama hiyo wakati Mayahudi wa nchi ya Sham walipomkataa na kama walivyoamini kwamba walimwua msalabani. Lakini mpango mzuri sana wa kimbingu ulimwokoa. Hivyo baada ya kumaliza juhudzi zake zote za kutaka kuwahurumia Mayahudi na shauku yake ya kutaka kuwahubiria na kutokana na Mayahudi kuwa na moyo mgumu sana kwa sababu ya uovu wa hali yao ya asili iliowafanya wasiweze kabisa kuukubali Ukweli, Yesu, kwa kujulishwa na Mwenyezi Mungu kwamba makabila kumi ya Mayahudi yalihamia upande wa India, akashika njia kuelekea kwenye majimbo hayo. Na, kwa kuwa makundi makubwa ya Mayahudi yalikuwa yameingia katka dini ya Kibuddha, hapakuwa na njia nydingine kwa nabii huyu mkweli isipokuwa kuelekeza juhudzi zake kwa wafuasi wa dini ya Kibuddha. Makuhani wa Kibuddha wa nchi ile walikuwa wakitazamia kutokea kwa "Masihi" Buddha. Kwa hiyo, yale majina ya Yesu na pia baadhi ya mafundisho yake ya kimaadili kama vile "Mpende adui yako; usirejeshe uovu", na kama vile ilivyotabiriwa na Gautama Buddha kuhusu Yesu kuwa na ngozi yenye ung'avu, kutokana na ishara zote hizi makuhani wakamchukulia yeze kuwa ndiye Buddha. Yawezekana pia kwamba baadhi ya majina yake na mafundisho yake na mambo ya uhakika kuhusu maisha ya Yesu vyawenza kuwa vilinasibishwa kwa Buddha wakati ule kwa makusudi au bila kukusudia; kwani Wahindu kamwe hawajatoa uthibitisho wa ustadi wa kutosha katika kuiweka historia kwenye

kumbukumbu. Matukio ya maisha ya Buddha hayakuwekwa katika kumbukumbu hadi wakati wa Yesu.

Kwa hiyo, Makuhani wa Kibuddha walikuwa na fursa nzuri sana ya kulinasibisha kwa Buddha jambo lo lote walilotaka. Hivyo yaelekeea kwamba walipokuja kuujua uhakika kuhusu maisha ya Yesu na mafundisho yake kimaadili, wakayachanganya haya na mambo mengine waliyoyabuni wao wenyewe na wakayanasibisha yote hayo kwa Buddha¹. Hivi punde nitathibitisha kwamba yale mafundisho ya kimaadili ya Biblia - yale majina "Mwanga" n.k. ambayo, jinsi yalivyo kwa Yesu yanakutwa yamerikodiwa kumhusu Buddha kama pia kilivyo kisa cha kushawishiwa na Shetani - yote haya yaliandikwa kwenye vitabu vya Kibuddha wakati Yesu alipokuja humu nchini baada ya kutungikwa msalabani.

Zaidi ya hayo kupo kufanana kwингine kati ya Buddha na Yesu: Dini ya Kibuddha imeweka katika kumbukumbu zake kwamba wakati wa kushawishiwa Buddha alikuwa amefunga saumu na kwamba kufunga huko kulidumu kwa muda wa siku arobaini. Wasomaji wa Injili wanafahamu kwamba Yesu pia alifunga kwa siku arobaini.

Na, kama nilivyokwisha sema hivi punde kuwa kupo kufanana kwa ajabu kati ya mafundisho ya Kimaadili ya Buddha na yale ya Yesu kwa kiasi hiki kwamba kwa wale wanaoyafahamu yote mawili limekuwa kwao jambo lenye nguvu sana. Kwa mfano, Injili zinasema; usilipize maovu, mpende adui yako, ishi katika umaskini, jiepusha na majivuno na uwongo na uchoyo. Hayo hayo ndiyo mafundisho ya Buddha. La, bali mafundisho ya Kibuddha yanaweka mkazo zaidi kuhusu jambo hilo kwa kiasi hiki kwamba viumbe vyote vyenye uhai - hata kuua mchwa na wadudu kumetangazwa kuwa ni dhambi. Kanuni maarufu ya dini ya Kibuddha ni: Huruma kwa ajili ya ulimwengu mzima; kuwatakia hali njema binadamu wote na wanyama wote; kuchochaea moyo

1. Hatuwezi kukana kwamba tangu zama za kale Imani ya Kibuddha ilikuwa inayo mafundisho ya kimaadili ya kutosha ndani yake; lakini wakati huo huo nashikilia kwamba ile sehemu ambayo ni mafundisho matupu ya Injili - yale mafumbo na nukuu zingine kutoka katika Biblia - bila shaka iliongezwa kwenye vitabu vya Kibuddha wakati Yesu alipokuwa katika nchi hii.

wa umoja na upendo kwa kila mtu. Hayo hayo ndiyo mafundisho ya Injili.

Tena, kama vile Yesu alivyowatuma wanafunzi wake kwenda kwenye nchi mbalimbali - na yeze mwenyewe akiwa amekwenda kwenye nchi moja - vivyo hivyo ndivyo alivyofanya Buddha. *Buddhism* kilichotungwa na Sir Monier Williams kinarikodi kwamba Buddha aliwatuma wanafunzi wake kwenda kuhubiri, akiwaagiza hivi: Enendeni na zungukeni kila mahali kwa kuuhurumia ulimwengu na kwa ajili ya ustawi wa miungu na watu. Enendeni katika pande mabalimbali. Hubirini itikadi (Dharham), kwa nasaha njema (Kalayana) mwanzoni, katikati na mwishoni, kwa maana yake halisi (artha) na jinsi ilivoandikwa (vyanjana). Tangazeni maisha ya kujizua kikamilifu, maisha ya utakatifu na maisha ya kutokuo (Drahmacariyam). Mimi pia nitakwenda kuihubiri itikadi hii. (Mahavagga 1.11.1)¹. Buddha alikwenda Benares na akafanya miujiza mingi kwenye jimbo lile; alifanya karamu ya kuvutia juu ya kilima kama vile Yesu alivyofanya karamu yake mlimani. Tena, kitabu hicho hicho kinasema kwamba mara nyingi Buddha alihubiri kwa njia ya mafumbo; alielezea mambo ya kiroho kwa mfano wa vitu vyenye kuonekana kwa macho ya kawaida.

Naikumbukwe kwamba mafundisho haya ya kimaadili na njia hii ya kuhubiri, yaani, kuzungumza kwa mafumbo ilikuwa njia ya Yesu. Namna hii ya kuhubiri na mafundisho haya ya kimaadili yakichanganywa pamoja na mazingira mengine, yanaashiria mara moja kwamba huku kulikuwa ni kumuigiza Yesu. Yesu alikuwa hapa India; alikwenda kuhubiri kila mahali; wafuasi wa imani ya Kibuddha walikutana naye, na baada ya kuona kwamba yeze alikuwa mtu mtakatifu aliyefanya miujiza, wakayarikodi mambo haya kwenye vitabu vyao; la, bali wakamtangaza yeze kuwa ndiye Buddha kwani ni tabia ya hali ya asili ya binadamu kujaribu kujipatia jambo jema po pote litapokuwa, kwa kiasi hiki kwamba watu wanajaribu kurikodi na kukumbuka tamshi lo lote la kiakili lenye kufanywa na mtu ye yote machoni pao. Kwa hiyo inaelekea zaidi

1. *Buddhism*, kilitungwa na Sir Monier Williams, kilichotangazwa na John Murray, London 1889, ukurasa 45.

sana kwamba wafuasi wa imani ya Kibuddha wanaweza kuwa wameinakili picha nzima ya Injili zote kwenye vitabu vyao; kwa mfano kufunga kwa siku arobaini kwa wote wawili, Yesu na Buddha; kushawishiwa kwa wote wawili; kuzaliwa bila baba kwa wote wawili, mafundisho ya kimaadili ya wote wawili; kujiita "Bwana" na "Masahaba" zao kuitwa "wanafunzi"; kama vile Mathayo, sura ya 10 aya ya 8 na 9 zinavyosema: "Msichukue dhahabu wala fedha wala mapesa kwenye mishipi yenu", vivyo hivyo Buddha naye alitoa amri hiyo hiyo kwa wanafunzi wake; kama vile Injili inavyohimiza kuishi bila kuoa, vivyo hivyo ndivyo yafanyavyo mafundisho ya Buddha; kama vile kulivyokuwako na tetermeko la ardhi wakati Yesu alipowekwa Msalabani; vivyo hivyo imerikodiwa kwamba kulikuwako na tetermeko la ardhi wakati wa kufariki Buddha. Mambo yote haya yenye kufanana yanatokana na ukweli wa ziara ya Yesu nchini India, ambayo ilikuwa ni kipande cha bahati njema kwa wafuasi wa Imani ya Kibuddha, kutokana na ye ye kuishi mionganii mwao kwa muda mwingi kidogo na kutokana na wafuasi wa Buddha kujipatia elimu nzuri, uhakika wa maisha yake na uhakika wa mafundisho yake yaliyo bora. Kwa sababu hiyo, ilikuwa lazima kwamba sehemu kubwa ya mafundisho hayo na suna zake ziwe zimejipenyeza kwenye kumbukumbu za Kibuddha kwani Yesu aliheshimiwa na kuhesabiwa kuwa ni Buddha na wafuasi wa Buddha. Kwa hiyo, watu hawa wakazirikodi hadithi zake kwenye vitabu vyao na wakazinasibisha na Buddha.

Kwa kweli ni jambo la ajabu, kwamba Buddha, kama alivyofanya Yesu, awe amewafundisha wanafunzi wake kwa njia ya mafumbo - hususan kwa njia ya mafumbo yale yanayopatikana katika Injili. Katika moja ya mafumbo hayo Buddha anasema:

"Kama vile mkulima anavyopanda mbegu lakini hawezi kusema: Mbegu hii itavimba leo, na kesho itachipua, vivyo pia ndivyo ilivyo kwa wanafunzi; ni lazima atii maagizo, ajizoeze kutafakari na ajifunze itikadi; hawezi kusema leo au kesho nitaokolewa".¹

Hili, itakumbukwa, ndilo fumbo lile lile ambalo limekuwamo ndani ya Injili hadi leo. Buddha anasimulia tena fumbo jingine:

1. Sir. M. M. Williams, *Buddhism*, ukurasa 51

"Tena kama vile kundi la kulungu linavyoishi msituni na mtu anakuja kulifungulia njia ya udanganyifu na: kulungu hao wakaumia, na mwininge anakuja kulifungulia njia ya usalama na kulungu wakasitawi, vivyo hivyo wakati watu wanapoishi miongoni mwa mambo ya furaha mtu mwovu anakuja na kufungua njia ya uwongo yenye ncha nne. Kisha anakuja mtu mkamilifu na kufungua njia ya usalama yenye ncha nne ya imani ya kweli n.k. (P. Oldenberg 191 - 192)".

Buddha alifundidha pia:

Uchamungu ni hazina ilio salama ambayo hakuna awezaye kuiiba. Ni hazina ambayo inakwenda pamoja na watu hata baada ya kifo: Ni hazina ambayo ni chanzo cha Elimu yote na Ukamilifu wote".¹

Hivyo itaonekana kwamba mafundisho ya Injili ni yale yale. Kumbukumbu za kale za Kibuddha zenyе mafundisho haya ni za kipindi ambacho hakiko mbali na wakati wa Yesu - la, bali ni za kipindi kile kile. Tena, kwenye ukurasa wa 135 wa kitabu hicho hicho panajitokeza hadithi ambamo Buddha anazungumzia kuhusu hali yake ya kutokuwa na hatia kwa vile hakuna mtu ambaye angeweza kuonyesha doa katika tabia yake. Hili pia linao mfano na usemi wa Yesu. Buddhism, kwenye ukurasa wa 45 kinasema:

"Mafundisho ya Kimaadili ya Buddha yana mfanano wa ajabu na yale ya Kikristo."

Nakubali; ninakiri; yote yanasema, "Usiupende ulimwengu; wala mali; usiwachukie adui zako; usitende maovu; yashinde maovu kwa wema; watendee wengine kama wewe unavyotaka kutendewa" - hii inaonyesha mfanano wa ajabu kati ya Injili na mafundisho ya Buddha kwa kiasi hiki kwamba si lazima kutaja mambo mengine zaidi ya ufanuzi.

Kumbukumbu za Kibuddha zinaonyesha pia kwamba Gautama Buddha alitabiri kutokea kwa Buddha wa pili ambaye aliiwa Metteyya.

1. Sir. M. M. Williams, *Buddhism*, ukurasa 51

Utabiri huu umo katika *Laggawati Sutatta* - kumbukumbu ya Kibuddha. Imetajwa kwenye ukurasa wa 142 wa kitabu cha Oldenberg. Utabiri huo unasomeka hivi:¹

"Atakuwa kiongozi wa kundi la wanafunzi lenye kufikia idadi ya mamia ya maelfu, kama mimi nilivyo sasa kiongozi wa makundi ya wanafunzi yenye kufikia idadi ya mamia."

Itaonekana hapa kwamba neno la Kiebrania Masiha, ni sawasawa na neno la Kipali Metteyya. Ni jambo la elimu ya kawaida kwamba wakati neno linapohamishwa kutoka katika lugha moja kwenda kwenye lugha nyingine aghlabu linapata mabadiliko: neno la Kiingereza pia, linalochukuliwa na lugha nyingine, linapata mabadiliko: kwa mfano; Max Muller, kufuatia orodha iliyotolewa kwenye ukurasa wa 318 wa jalada la 2 la "Sacred Books of the East, anasema: Ile 'th'ya alfabeti ya Kiingereza inakuwa kama 's'kwenye Kiajemi au Kiarabu. Kwa kuyazingatia mabadiliko haya tunaweza kuelewa kwa urahisi kwamba neno Messiah likawa Metteyya kwa lugha ya Kipali, ambayo ina maana kwamba Metteyya atakayekuja baadaye ambaye alitabiriwa na Buddha kwa hakika ndiye Masihi - si mtu mwingine. Hili linaungwa mkono na ukweli kwamba Buddha alitabiri kwamba imani aliyoianzilisha itadumu ulimwenguni kwa zaidi ya miaka 500; kwamba wakati wa kupungua kwa kanuni na mafundisho yake, huyo Metteyya atakuja nchini humu na ataziimarisha tena ulimwenguni. Sasa tunajua kwamba Yesu alitokea miaka 500 baada ya Buddha, na kwamba kama vile Buddha alivyoweka kikomo cha muda wa kupungua kwa Imani yake, dini ya Kibuddha iliingia katika hali ya mwanguko ulipowadia wakati uliowekwa. Kisha ndipo Yesu, baada ya kuepuka Msalabani, akasafiri kuja humu nchini; na wafuasi wa dini ya Kibuddha walimtambua na wakamtendea kwa heshima kubwa. Hapana shaka kwamba mafundisho ya kimaadili na mazoezi ya kiroho yaliyofundishwa na Buddha yalifufuliwa na Yesu.

Wakristo wanakiri kwamba ile karamu ya Mlimani ya Injili na mafundisho mengine ya kimaadili ni yale yale yaliyohubiriwa na

1. Dr. Herman Oldenberg. *Buddha*.

Buddha ulimwenguni miaka mia tano kabla. Wanasema pia kwamba Buddha hakufundisha mafunzo ya kimaadili tu; alifundisha pia kweli nyingine zilizo kuu. Kwa maoni yao hii lakabu "mwanga wa Asia" inayotumika kumhusu Buddha inatumika mahali pake hasa. Hivyo kulingana na utabiri wa Buddha, Yesu alitokea miaka mia tano baadaye; na kama wanavyokiri wanazuoni wengi wa Kikristo, mafundisho yake yalikuwa sawasawa na yale mafundisho ya Buddha. . . Kwa hiyo, hapana shaka kwamba alijitokeza katika "roho" ya Buddha. Kwenye kitabu cha Oldenberg, kwa mamlaka ya *Laggawati Sutatta*, imeelezwa kwamba kwa kuangalia yajayo baadae, wafuasi wa Buddha walijiliwaza kwa mawazo kwamba, wakiwa wanafunzi wa Metteyya, watapata furaha na wokovu; yaani walikuwa na yakini kwamba Metteyya atawajia na kwamba watapata wokovu kwa njia yake, kwani yale maneno ambayo Buddha alitangaza kuhusu matumaini ya kuja kwa Metteyya yaliashiria kwamba wanafunzi wake wangekutana naye. Maelezo ya kitabu kilichotajwa hapo juu yanatilia nguvu ile dhana kwamba kwa ajili ya kuwaongoza watu hawa Mwenyezi Mungu Alitengeneza seti mbili za mazingira: kwanza, kutokana na jina Asaf lililotajwa katika Mwanzo 3, aya ya 10, ambalo lina maana ya "mtu anayewakusanya watu", Yesu hakuwa na budi isipokuwa kuizuru ile nchi ambako Mayahudi walikuja kulowea; pili, kwamba kulingana na utabiri wa Buddha, ilikuwa jambo la muhimu kwamba wafuasi wa Buddha ni lazima wamwone na wafaidike na uchamungu wake. Kwa kuzitafakari nukta hizi mbili kwa pamoja linakuwa takriban ni jambo la yakini kabisa kwamba Yesu ni lazima awe ameizuru Tibet. Na ule ukweli kwamba mafundisho na taratibu za ibada za Kikristo vimeathiri sana dini ya Kibuddha ya Tibet unafanya liwe jambo la lazima ile imani kwamba Yesu ni lazima awe aliwahi kuwatembelea watu wa Tibet. Isitoshe, ule ukweli kwamba wafuasi wakereketwa wa dini ya Kibuddha, kama inavyoelezwa kwenye kumbukumbu za Kibuddha hadi leo, walikuwa kila mara wakitazamia kukutana naye, unadhihirisha kwamba hii shauku yao kali ilitangaza mapema ziara yake nchini humu.

Kwa kuzingatia kweli hizi mbili, mtu mwadilifu hana haja ya kuziepa kumbukumbu za Kibuddha ili kupata maelezo kwamba Yesu alipata kuja Tibet. Kwani, kulingana na utabiri wa Buddha, kwa kuwa shauku ya kuja kwa Buddha mara ya pili ilikuwa kubwa, utabiri wenyewe utakuwa umemvuta Yesu kwenda Tibet.

Ni lazima itambulike kwamba hili neno "Metteyya" lilitotajwa mara kwa mara kwenye vitabu vya Kibuddha bila shaka ndilo neno "Masihi". Katika kitabu kiitwacho *Tibet, Tartary, Mongolia*, kilichotungwa na H. T. Prinsep, kwenye ukurasa wa 14, kuhusu Metteyya Buddha ambaye kwa hakika ndiye Masihi, imeelezwa kwamba baada ya kusikia na kuona kwa mara ya kwanza hali zinazopatikana nchini Tibet, wamisionari wa kwanza (Wahubiri wa Kikristo) walifika uamuzi kwamba ndani ya vitabu vya kale vya Walama ziliweza kuonekana alama za dini ya Kikristo. Tena kwenye ukurasa huo huo imeelezwa kwamba hapana shaka kuwa mamlaka hizi za kale ziliamini kwamba wanafunzi wa Yesu walikuwa bado wangali hai wakati mafundisho ya Kikristo yalipofika mahala hapa. Kwenye ukurasa wa 171 imeelezwa kwamba hapana shaka kuwa wakati ule kulikuwako na imani iliyoshikwa na wengi kwamba angetokea mkombozi mkubwa ambaye kuhusu kutokea kwake Tacitus anasema kwamba si Mayahudi tu waliohusika na Imani hiyo bali dini ya Kibuddha wenyewe ilikuwa inajenga msingi, yaani ilitabiri kuja kwa Metteyya. Mtunzi wa kitabu hiki cha Kiingereza anasema kwenye maelezo: Vitabu viitwavyo *Pitakkatayan* na *Atha Katha* vinao utabiri ulio wazi kuhusu kutokea kwa Buddha mwingine, ambao utatimia miaka 1000 baada ya wakati wa Gautama au 'Sakhiya Muni'. Gautama anaeleza kwamba yeye ni Buddha wa 25 na kwamba yule 'Bagawa Metteyya' bado hajatokea, yaani baada ya yeye kuondoka atakuja yule ambaye jina lake litakuwa Metteyya, ambaye atakuwa mng'avu. Mtunzi huyo wa Kiingereza anaendelea kusema kwamba neno Metteyya lina mfanano wa ajabu na Masihi. Kwa kifupi, Gautama Buddha anaeleza wazi wazi kwenye utabiri huu kwamba patatokea Masihi katika nchi yake, mionganoni mwa watu wake na mionganoni mwa wafuasi wake.

Huo ndio ulikuwa msingi wa imani ya kudumu kuhusu kuja kwa Masihi mionganoni mwa wafuasi wake. Kwenye utabiri wake huyu Buddha alimwita "Bagwa Metteyya" kwa sababu kwa lugha ya Sanskrit "Bagwa" ina maana ya "Mweupe" na kwa kuwa Yesu alikuwa mkazi wa jimbo la Syria, alikuwa na rangi nyeupe.

Watu wa nchi inayohusika na utabiri huu, yaani, watu wa Magadh, ambamo ndimo mlimokuwa na mahali paitwapo Bajagriha, walikuwa weusi. Na Gautama Buddha mwenyewe alikuwa mweusi. Aliwasimulia wafuasi wake ishara mbili za kuondoa shaka kuhusu Buddha atakayekuja baadaye: (1) kwamba atakuwa "Bagwa" (2) kwamba atakuwa "Metteyya", yaani "msafiri", na kwamba atakuja kutoka nchi ya kigeni. Kwa hiyo, watu hawa kila mara walikuwa wakizitafuta ishara hizi hadi walipomwona Yesu kidhahiri. Kila mfuasi wa dini ya Kibuddha ni lazima kabisa ataungama ile imani kwamba miaka mia tano baada ya Buddha, yule Bagwa (mweupe) Metteyya alitokea katika nchi yao. Kwa hiyo lisiwe jambo la kustaajabisha iwapo vitabu vyta imani ya Kibuddha vitataja kuja kwa Metteyya, yaani, Masihi nchini mwao, na kutimilizwa kwa utabiri wake. Na tuseme kwamba hakuna mtajo wa namna hiyo, hata hivyo, kwa sababu kwa msingi huu wa ufunuo wa kimbingu Buddha aliwapatia wanafunzi wake matumaini kwamba Bagwa Metteyya atakuja nchini mwao, hakuna mfuasi wa dini ya Kibuddha ambaye anautambua utabiri huu anawenza kukana ujaji nchini humu wa Bagwa Metteyya ambaye jina lake jingine ni Masihi; kwani, kutokutimilizwa kwa utabiri huo kunathibitisha uwongo wa imani hiyo. Na huu utabiri ambao kutimia kwake kuliwekewa wakati maalumu na ambao Gautama Buddha aliusimulia kwa wafuasi wake mara nyingi - kama utabiri huu usingetimia katika wakati wake uliowekwa, wafuasi wa Buddha wangetilia shaka ukweli wake na ingalielezwa kwenye vitabu kwamba utabiri huu haukutimilizwa. Hoja nyagine yenyе kuunga mkono kutimia kwa utabiri huu ni kwamba kunako karne ya saba baada ya kuzaliwa Yesu vilipatikana nchini Tibet vitabu vilivyokuwa na neno "Masihi", yaani vilitaja jina la Yesu (amani juu yake) likiwa limeandikwa kama Mi-Shi-Hu. Mtayarishaji wa hiyo orodha

iliyokuwa na hilo neno Mi-Shi-hu ni mfuasi wa dini ya Kibuddha. Tazama kitabu kiitwacho *A record of the Buddhist Religion* kilichotungwa na I. Tsing na kutafsiriwa na G. Takakusu. Huyu Takakusu ni Mjapani aliyetafsiri kitabu cha I. Tsing; na I. Tsing ni msafiri wa Kichina - ambaye pembezoni na kwenye kiambatanisho cha kitabu chake Takakusu anaeleza kwamba kwenye kitabu kimoja cha kale linapatikana hili jina Mi-Shi-Hu (Masihi). Kitabu hiki ni cha zama takriban za karne ya saba; kilitafsiriwa hivi karibuni na Mjapani aitwaye G. Takasuku na kutangazwa na Clarendon Press, Oxford¹. Kitabu hiki kwa vyo vyote vile kinalo hili neno Masihi jambo linaloonyesha kwamba hili neno halikuingizwa kutoka nje na wafuasi wa dini ya Buddha bali lilichukuliwa kutoka kwenye utabiri wa Buddha na mara nyingine liliandikwa Masihi na mara nyingine likaandikwa Bagwa Metteyya.

Na miongoni mwa ushahidi tulio nao wa kumbukumbu za Kibuddha ni kwamba kwenye kitabu kiitwacho *Buddhism* kilichotungwa na Sir Monier Williams, kwenye ukurasa wa 45 imeandikwa kwamba mwanafunzi wa sita wa Buddha atakuwa ni mtu aitwaye "Yasa". Neno hili la mwisho laelekea kuwa ni kifupisho cha neno "Yasu". Kwa vile Yesu (amani juu yake) alitokea miaka mia tano baada ya kifo cha Buddha, yaani kwenye karne ya sita, aliitwa mwanafunz wa sita. Ni lazima ifahamike kwamba ndani ya kitabu kiitwacho *The Nineteenth Century*, kwenye ukurasa wa 517 wa toleo la Oktoba 1894, Professa Max Muller anaunga mkono maelezo yaliyotolewa hapo juu kwa kusema kwamba waandishi mashuhuri wamekwishaonyesha mara nyingi kwamba Yesu aliathiriwa na kanuni za dini ya Kibuddha na kwamba majaribio yanafanywa hata leo ili kugundua baadhi wa misingi ya kihistoria ambayo kwayo kanuni za imani ya Buddha zitathibitishwa kuwa zilifika Falastin wakati wa siku za Yesu. Jambo hili linaviunga mkono vitabu vya imani ya Kibuddha ambamo imeandikwa kwamba Yasa alikuwa mwanafunzi wa Buddha, kwani, wakati Wakristo mashuhuri kama Profesa Max Muller

1. Tazama ukurasa wa 169 na 223 wa kitabu hiki.

wamekiri kwamba kanuni za dini ya Kibuddha zilikuwa na athari kwa Yesu haitakuwa kukosea sana kusema kwamba hii ilikuwa na maana ya yeye kuwa mwanafunzi wa Buddha.

Hata hivyo, mimi nachukulia utumiaji wa maneno kama hayo kumhusu Yesu (amani juu yake) kuwa ni utovu wa heshima na ni ufidhuli. Na maelezo yanayopatikana kwenye vitabu nya imani ya Kibuddha kwamba "Yasu" alikuwa mwanafunzi wa Buddha ni mfano tu wa tabia iliyothibitika ya makuhani wa watu hawa ya kutaja mtu mkubwa atakayetokea wakati ujao kana kwamba ni mwanafunzi wa yule aliyetokea kabla. Licha ya hayo, kama ilivyokwisha elezwa, kwa vile upo mfanano mkubwa kati ya mafundisho ya Yesu na Buddha haitakuwa kukosea sana kuzungumzia uhusiano wa bwana na mwanafunzi kati ya Buddha na Yesu, ingawa unaweza kuwa hauendani na hisia za heshima. Lakini mimi sikubaliani na jinsi wachunguzi wa Kizungu wanavyotaka kuthibitisha kwamba kanuni za dini ya Kibuddha zilifika Falastin wakati wa siku za Yesu. Ni jambo la bahati mbaya kweli kweli kwamba wakati jina na kutajwa kwa Yesu kumo ndani ya vitabu nya kale nya dini ya Kibuddha wachunguzi hawa bado waendelee kuchukua njia iliyopinda ya kujaribu kutafuta alama za imani ya Buddha nchini Falastin. Kwa nini wasitafute nyayo zilizobarikiwa za Yesu kwenye ardhi ya majabali ya Nepal, Tibet na Kashmir? Lakini najua kwamba wachunguzi hawa wasingeweza kutazamiwa kugundua ukweli ambaio ulikuwa umefichika chini ya matabaka elfu moja ya giza; bali ilikuwa ni kazi ya Mwenyezi Mungu - Ambaye Aliona kutoka mbinguni kwamba kuabudiwa binadamu na urukaji wa mipaka yote vimezagaa ulimwenguni kote na kwamba kuabudiwa kwa Msalaba na kinachodhaniwa kuwa ni kafara ya binadamu viliiitenganisha miyo ya mamilioni mengi ya watu na Mwenyezi Mungu wa kweli - Ambaye ghera Yake ilimleta ulimwenguni mtumishi Wake kwa jina la Yesu Mnazareti ili kuvunja imani ya Msalaba. Na kulingana na ahadi ya zamani alitokea kama Masihi Aliyahidiwa. Kisha ukaja wakati wa kuvunjwa kwa Msalaba, yaani ule wakati ambapo kosa la imani ya Msalaba likadhihirishwa kama vile kukivunja

kipande cha ubao katika sehemu mbili. Kwa hiyo sasa ndio wakati ambapo Mbingu imefungua njia kwa ajili ya uvunjwaji wa Msalaba ili mtafutaji ukweli aweze kuangaza macho na kuutafuta ukweli huo.

Lile wazo la Yesu kupaa mbinguni, ingawa lilikuwa kosa, hata hivyo lilikuwa na maana, yaani kwamba Ukweli wa Kimasihi ulikuwa umesahauliwa na ulikuwa umefutiliwa mbali kama vile maiti inavyoliwa na udongo kaburini - Ukweli huu wa Kimasihi uliaminiwa kuwako mbinguni katika hali ya kimwili ya binadamu. Kwa hiyo ilikuwa lazima kwamba Ukweli huu uteremshwe ardhini katika siku za baadaye. Na umeteremka ardhini katika zama hizi kwa sura ya binadamu aliye hai; "umeuvunja" Msalaba; na yale maovu ya uwongo na ya kuabudu mambo yasiyokuwa kweli ambayo katika Hadithi ihusuyo Msalaba Mtume wetu Mtukufu ameyalinganisha na nguruwe, yamekatwa vipande vipande sambamba na "kuvunjwa" kwa msalaba, kama vile nguruwe akatwavyo kwa upanga. Hadithi hii haimaanishi kwamba Masihi Aliyahidiwa atawauwa makafiri na kuvunja misalaba yao kidhahiri: bali, kuvunjwa kwa Msalaba kunamaanisha kwamba wakati wa zama zile Mungu wa Mbingu na Ardhi Ataufichua huu ukweli uliofichika ambao kwa ghafula utalivunja jengo lote la Msalaba. Na kuuawa kwa nguruwe hakuna maana ya kuuawa kwa watu au nguruwe bali kuna maana ya kuuawa kwa tabia za kinguruwe - kama vile kudumu katika uwongo na usisitizaji wa kuwasilisha uwongo huo kwa watu wengine, jambo ambalo ni sawasawa na kula uchafu. Kwa hiyo, kama vile nguruwe mfu asivyoweza kula uchafu, vivyo hivyo wakati utafika - la bali tayari umeshafika - ambapo silika za uovu zitazuiliwa kula uchafu wa namna hii. Maulamaa wa Kiislamu wamepotoka katika kuutafsiri utabiri huu. Maana halisi ya "Kuvunjwa kwa Msalaba" na "Kuuawa kwa nguruwe" ni hiyo niliyoieleza. Isitoshe, katika zama za Masihi Aliyahidiwa vita za kidini zitafikia ukomo; na Mbingu itazirudisha zile kweli zing'aazo kiasi cha kuleta machoni pa mtu ile tofauti iliyo ang'avu kati ya ukweli na uwongo. Kwa hiyo, msidhani kwamba nimekuja na upanga. Hasha, nimekuja kuziingiza panga zote

katika ala zake. Ulimwengu umekuwa ukipigana vikali gizani. Watu wengi wamewashambulia wale wakweli wawatakiao mema, wameijeruhi moyo ya marafiki wenye kuwahurumia na kuwaumiza wapenzi wao. Lakini sasa, giza halipo tena. Usiku umeondoka na hivi sasa ni mchana. Na amebarikiwa yule ambaye atabakia bila kupata hasara tena.

Na mionganoni mwa ushahidi uliomo kwenye kumbukumbu za Kibuddha ni ule ushahidi uliopo kwenye ukurasa wa 419 wa kitabu kiitwacho *Buddhism* kilichotungwa na Oldenberg. Ndani ya kitabu hiki, kwa mamlaka ya kitabu kiitwacho '*Mahavaga*', ukurasa wa 54 sehemu ya kwanza, imerikodiwa kwamba mrithi wa Buddha atakuwa mtu aitwaye 'Rahula' anayeelezewa pia kama mwanafunzi; la, bali mtoto wake. Sasa hapa nasema kwa nguvu kwamba lile neno 'Rahula' lililomo kwenye kumbukumbu za Kibuddha ni matamshi mabaya ya neno "Ruuhullahi" ambalo ni moja mionganoni mwa majina ya Yesu. Na kile kisa kwamba huyu 'Rahula' alikuwa mwana wa Buddha ambaye, baada ya kumtelekeza mtoto huyu akiwa yungali mchanga alikwenda uhamishoni, na ambaye akiwa na nia ya kuachana na mkewe moja kwa moja, alimwacha akiwa amelala bila kumjulisha wala kumuaga, na akakimbilia nchi nyingine, wote huo ni upuuizi, ni jambo la kijinga na lenye kuaibisha utukufu wa Buddha. Mtu katili na mwenye moyo mgumu wa namna hiyo ambaye hakuwa na huruma kwa mkewe maskini, ambaye alimwacha mkewe akiwa amelala na bila kumwambia neno la kumliwaza, akayeyuka kama mwizi; ambaye alipuuza moja kwa moja wajibu aliokuwa nao kwake kama mume - bila kumtaliki wala kumwomba ruhusa ya kwenda safari isiyokuwa na mwisho; ambaye aliupa dharuba kali moyo wake kwa kupotea ghafla, ambaye alimtia machungu na hakumpelekea walau barua hadi mtoto akakua na kuwa mtu mzima, na ambaye hakukihurumia hicho kitoto kichanga - mtu wa namna hiyo ambaye hakuyaheshimu mafundisho ya kimaadili aliyoafundisha ye ye mwenyewe kamwe hawezi kuwa mchamungu. Busara yangu inakataa kulikubali hili kama inavyokataa kukubali kile kisa kilichomo kwenye Injili kwamba siku

moja Yesu hakumstahi mama yake, kwamba hakumjali alipokuja na kumwita, bali badala yake akamtolea maneno ya matusi.

Kwa hiyo ingawaje hivi visa vihusuvyo kuumizwa kwa hisia za mke na mama vina aina fulani ya kufanana, hata hivyo hatuwezi kuvinasibisha visa vyatamna hiyo, ambavyo vinaleta maana ya mchapuko kutoka kwenye viwango vyatamna kawaida vyatamna tabia, kwa Yesu au Gautama Buddha.

Kama Buddha hakumpenda mkewe, je hakuwa vile vile na huruma juu ya mwanamke masikini na mtoto anayeteseka? Hii ina maana ya utovu mbaya sana wa tabia njema; mbaya kwa kiasi hiki kwamba nimepata uchungu kwa kuufikiria baada ya kupita kwa mamia ya miaka. Mtu anashindwa kuelewa kwa nini aliyafanya yote haya. Kutokumjali mke kunatosha kumfanya mtu awe mbaya- isipokuwa pale mwanamke mwenyewe anapokuwa hana maadili mema, si mtiifu au mtovu wa imani na adui kwa mumewe. Hivyo, hatuwezi kuvinasibisha tabia mbaya yo yote ya namna hiyo kwa Buddha; hili likiwa kinyume hata na mafundisho yake mwenyewe. Kwa hiyo mazingira haya yanaonyesha kwamba kisa hiki siyo sahihi. Kwa hakika 'Rahula' lina maana ya Yesu ambaye jina lake jingine ni "Ruuhullahi". Neno "Ruuhullahi" kwa Kiebrania linakuwa sawa na "Rahula", na huyo "Rahula", yaani "Ruuhullahi" ameitwa mwanafunzi wa Buddha kwa sababu kama nilivyokwisha eleza kuhusu Yesu kuja baada yake na kuleta mafundisho ya Buddha, na kwa sababu ya wafuasi wa imani ya Kibuddha kutangaza kwamba chanzo cha mafundisho yale ni Buddha na kwamba Yesu alikuwa mmoja wa wanafunzi wake. Na lisiwe jambo la kustaajabisha iwapo Buddha, kutokana na ufunuo kutoka kwa Mwenyezi Mungu akamtangaza Yesu kuwa 'mwana' wake.

Kipande kingine cha ushahidi wa kimazingira ni kwamba ndani ya kitabu hicho hicho imerikodiwa kwamba wakati 'Rahula' alipotenganishwa na mama yake, mwanamke aliyekuwa mfuasi wa Buddha, na ambaye jina lake lilikuwa Magdaliyana alifanya kazi ya utarishi. Itazingatiwa kwamba jina Magdaliyana ni matamshi mabaya ya Magdalena, mwanamke mfuasi wa Yesu

aliyetajwa ndani ya Injili.

Ushahidi wote huu, ambao umepangwa kwa muhtasari unawaongoza watu waadilifu kufikia kwenye uamuzi kwamba Yesu ni lazima awe alikuja nchini humu, na licha ya ushahidi wote huo bayana, hakuna mtu mwenye busara awezaye kupuuza mfanano unaopatikana hususan nchini Tibet, kati ya mafundisho na ibada ya dini ya Kibuddha na ile ya Ukristo. La, bali kuna mfanano wa kustaajabisha kati yao kwa kiasi hiki kwamba Wakristo wengi wenye kutafakari wanaamini kwamba dini ya Kibuddha ni Ukristo wa Mashariki, na Ukristo ni dini ya Kibuddha ya Magharibi.

Kwa kweli ni jambo la kustaajabisha sana ya kwamba kama vile Yesu asemavyo, "Mimi ni Mwanga na Njia", hayo hayo yamesemwa na Buddha; kama vile Injili zinavyomwita Yesu Mkombozi, Buddha pia anajiita Mkombozi (*tazama Lalta Wasattara*). Ndani ya Injili imeelezwa kwamba Yesu hakuwa na baba, na kuhusiana na Buddha imeelezwa kwamba kwa hakika alizaliwa bila baba, ingawaje kidhahiri, kama vile Yesu alivyokuwa na baba, Yusufu, vivyo hivyo Buddha alikuwa na baba. Imeelezwa pia kwamba nyota ilichomoza wakati wa kuzaliwa kwa Buddha; kipo pia kile kisa cha Solomon akitoa amri ya kukatwa mtoto katika nusu mbili na kumpa moja ya nusu hizi mbili kila mmojawapo wa wale wanawake wawili, ambacho kinapatikana ndani ya kitabu cha Buddha *kiitwacho Jataka*. Hii, licha ya kuonyesha kwamba Yesu alikuja nchini humu, inaonyesha pia, kwamba Mayahudi wa nchi ile waliokuja nchini humu, walianzisha mahusiano na dini ya Kibuddha. Na ile hadithi ya mwanzo kama ilivyoelezwa ndani ya vitabu vya imani ya Kibuddha ina mfanano mkubwa na hadithi ya namna hiyo hiyo iliyotolewa ndani ya Taurati. Kama vile kulingana na Taurati mwanamume anavyohesabiwa kuwa bora kuliko mwanamke, vivyo hivyo katika dini ya Buddha mtawa mwanamume anahezesabiwa kuwa bora kuliko mtawa mwanamke. Lakini yaweza kuonekana kwamba huyu Buddha aliamini uhamaji wa roho, lakini "uhamaji" aliouamini ye ye hauko kinyume na mafundisho ya Injili. Kulingana na Buddha uhamaji

uko wa aina tatu:

(1) Kwamba vitendo vya mtu anayekufa na juhudzi zake vinalazimisha kupatikana kwa mwili mwingine; (2) ile aina ya uhamaji ambayo Watibet wanaamini itafanya kazi mionganini mwa Walama, yaani, sehemu fulani ya roho ya Buddha au Buddha Satwa inahamia kwa Mlama kwa wakati ule; ambayo inamaanisha kwamba uwezo wake, tabia yake na sifa zake za kiroho zinahamishiwa kwa Mlama huyo na kwamba roho yake inaanza kumhuisha Mlama huyo; (3) kwamba katika maisha haya mtu anapitia katika uumbaji wa aina mbalimbali - unafika wakati ambapo anakuwa kama dume la ng'ombe; anapozidi kuwa mchoyo na mwovu, anakuwa mbwa, lile umbile lake la kwanza likiwa linatoweka na kujichomoza jingine linalooana na tabia na vitendo vyake; lakini mabadiliko yote hayo yanatokea katika maisha haya haya ya kidunia. Imani hii haipingani na mafundisho ya Injili.

Nilikwisha eleza kwamba Buddha anaamini kuwako Shetani, kwa hiyo anaamini pia kuwako kwa jahanamu na pepo na kuwako kwa malaika na siku ya Kiyama. Na ile tuhuma kwamba Buddha hamwamini Mwenyezi Mungu ni uzushi mtupu. Buddha hakumwamini Vedanta na hakuiamini miungu ya kimwili ya Wahindu. Amezikosoa vikali sana hizi Veda. Haziamini hizi Veda zilizopo. Anakihesabu kile kipindi ambapo alikuwa Mhindu mfuasi wa hizi Veda kuwa ni kipindi cha kuzaliwa kiovu. Kwa mfano anadokeza kwamba kwa kipindi fulani alikuwa nyani; tena kwa muda alikuwa tembo; kisha akawa kulungu na mbwa; mara nne akawa nyoka na kisha akawa kinega, kisha akawa chura, akawa samaki mara mbili, mara kumi chui, mara nne kuku, mara mbili nguruwe na mara moja sungura, na kwamba wakati alipokuwa sungura alikuwa akiwafundisha manyani, mbewa na mbwa - maji; tena, anasema kwamba alikuwa pepo; siku moja alikuwa mwanamke, mchezaji na shetani. Vidokezo vyote hivi vina maana ya kuonyesha awamu za maisha yaliyojaa woga, za tabia za kike, za utovu wa kuogopa adhabu na ushenzi, na za ufisadi, ulafi na imani ya mambo ya uchawi. Inaonekana kwamba kwa njia hii

anaonyesha wakati ambapo ye ye ali kuwa mfuasi wa hizo Veda, kwani, baada ya kuachana nazo hatoi kidokezo cha dalili yo yote ya maisha mabaya ambayo bado yanaendelea kumkabili. Bali kinyume cha hayo, baadae anadai madai makubwa; alisema kwamba ye ye amebadili ka na kuwa mdhihirishaji wa Mwenyezi Mungu na amefikia daraja ya *Nirwana*.

Buddha anaeleza pia kwamba mtu anayeuhama ulimwengu akiwa amebeba vitendo vya kijahanamu anatupwa ndani ya jahanamu. Walinzi wa jahanamu humkokota kuelekea kwa Mfalme wa jahanamu aitwaye Yamah, na kisha mlaaniwa huyu huulizwa iwapo hakupata kuwaona wajumbe watano amba walitumwa kwake ili kwenda kumuonya: Utoto - Uzee - Maradhi - Kuadhibiwa mtu kutokana na makosa yake katika maisha haya haya ya kidunia amba ni uthibitisho wa adhabu ya akhera - Maiti ambazo zinaashiria uwezekano wa kuteketezwa kwa ulimwengu. Na huyu mtu mlaaniwa anajibu kwamba ali kuwa mjinga kwa hiyo hakupata kilitafakari lo lote mionganoni mwa mambo haya. Kisha walinzi wa jahanamu humkokota hadi mahali pa kutolea adhabu na kumfunga kwa minyororo ya chuma ambayo iko moto kama moto wenyewe. Zaidi ya hayo Buddha anasema kwamba jahanamu ina majimbo kadhaa ambamo wenyе dhambi wa makundi mbalimbali hutupwa. Kwa kifupi, mafundisho yote haya yanabainisha wazi wazi kwamba dini ya Kibuddha ina deni inalodaiwa na ushawishi binafsi wa Yesu. Lakini sikusudii kuendelea na mjadala huu. Naifunga sehemu hii hapa, kwani wakati ambapo kuna utabiri ulio wazi, ulioelezwa ndani ya vitabu vya imani ya Kibuddha kuhusu kuja kwa Yesu nchini humu - utabiri amba hakuna mtu awezaye kuukanusha - wakati mafumbo na mafundisho ya kimaadili ya Injili yanapatikana ndani ya vitabu vya imani ya Kibuddha vilivytungwa wakati wa zama za Yesu - nadharia zote hizi mbili zikiwekwa pamoja haziachi shaka yo yote kuhusu kuja kwa Yesu katika nchi hii. Kwa hiyo, ushahidi tulio panga kuufanya utafiti kwa kutumia kumbukumbu za Kibuddha umepatikana wote - Ashukuriwe Mwenyezi Mungu Mwenye nguvu.

SEHEMU YA 3

Kuhusu ushahidi kutoka kwenye vitabu vya historia unaoonyesha kwamba kuja kwa Yesu kwenye jimbo la Punjab na maeneo jirani yake lilikuwa jambo la lazima

Swali linajitokeza katika hali ya asili kuhusu kwa nini baada ya kuepukana na Msalaba Yesu alikuja katika nchi hii. Nini kilimshawishi kufanya safari ndefu ya namna hiyo? Linakuwa ni jambo la lazima kulijibu swali hili kwa kutoa kiasi fulani cha ufanuzi. Tayari nilikwisha sema kitu kuhusu jambo hili, hata hivyo nadhani kuna ulazima wa kulijadili kikamilifu ndani ya kitabu hiki.

Kwa hiyo, naitambulikane kwamba ilikuwa ni lazima sana kwa Masihi Isa (amani juu yake), kutokana na wadhifa wake wa kuwa mjumbe wa Kimbingu, kufunga safari ya kuelekea Punjab na vitongoji vyake kwani, yale makabila kumi ya Israeli ambayo katika Injili yameitwa Kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli, yalihamia nchini humu, ukweli ambao haukanushwi na mwanahistoria ye yote. Kwa hiyo ilikuwa ni lazima kwamba Masihi Yesu (amani juu yake) afunge safari ya kuja nchini humu, na baada ya kuwaona hao kondoo waliopotea awahubirie ujumbe wake kutoka mbinguni.

Na kama asingefanya hivyo, ujumbe wake ungekuwa bado haujatimilizwa, kwani kazi aliyotumwa ilikuwa hii ya kuwahubiria kondoo waliopotea wa Israeli; kufariki kwake dunia bila kuwatafuta kondoo hawa waliopotea, na baada ya kuwaona kuwafundisha njia ya wokovu, kungekuwa sawasawa na mtu aliyetumwa na mfalme wake kuliendea kabilia fulani la porini ili kuwachimbia kisima na kuwagawia maji, badala yake anakwenda mahali pengine na kukaa huko miaka mitatu au minne lakini hachukui hatua yo yote ya kulitafuta lile kabilia. Je mtu kama huyo atakuwa ametekeleza maagizo ya mfalme? Hapana, hata kidogo; mtu huyu halijali lile kabilia; anajitafutia starehe zake tu.

Lakini, kama iulizwe ni kwa vipi na kwa nini idhaniwe kwamba yale makabila kumi ya Israeli yalikuja nchini humu, jibu lake ni

kwamba upo ushahidi ambao hata mwenye akili ndogo hawezi kuutilia shaka: kwani inajulikana vizuri sana kwamba watu kama vile Waafghan na wakazi wa kale wa Kashmir kwa hakika ni Waisraeli kwa asili. Kwa mfano, watu wa ukanda wa vilima vya Alai ambao uko umbali wa safari ya siku mbili au tatu kutoka wilaya ya Hazara, wamejita Banii Israeli tangu zama zisizokumbukwa; vivyo hivyo wakazi wa Kala Dakah, ukanda mwengine wa vilima katika jimbo hili, huona fahari ya kuwa wenye asili ya Kiisraeli. Kisha lipo kabilia katika Wilaya ya Hazara yenye ambalo linanasibisha asili yao nchini Israeli. Kadhalika, watu wa eneo la milimani baina ya Chalas na Kabul hujiiita Waisraeli. Kuhusu watu wa Kashmir, maoni yaliyolezwa na Dk. Bernier kwa mujibu wa mamlaka ya baadhi ya wanazuoni wa Kiingereza kwenye sehemu ya pili ya kitabu chake kiitwacho *Travels in the Moghul Empire*, yanaonekana kuwa sahihi: yaani, yale maoni kwamba watu wa Kashmir ni wana wa Israeli; mavazi yao, maumbile yao na baadhi ya mila zao zinaonyesha moja kwa moja kwenye ukweli kwamba wana asili ya Kiisraeli. Mwingereza mmoja, George Forster kwa jina, anaeleza katika kitabu chake kwamba wakati wa ukaaji wake nchini Kashmir alijidhania yuko mionganini mwa kabilia la Mayahudi. Ndani ya kitabu kiitwacho *The Races of Afghanistan*, kilichotungwa na H. W. Belews C.S.I., (Thacker Spink & Co., Calcutta) imetajwa kwamba Waafghan walikuja kutoka Syria. Nebuchadnezzar aliwakamata mateka na kuwalishwa nchini Uajemi na Media ambapo kutoka hapo baadae walitembea kuelekea Mashariki na kulowea katika vilima vya Ghaur, ambako walijulikana kama Banii Israeli. Katika kulithibitisha hili kuna utabiri wa nabii Idrisa (Enoch), usemao kwamba yale makabila kumi ya Israeli ambayo yalikamatwa mateka yalitoroka kutoka utumwani na yakakimbilia katika eneo liitwalo Arsartat ambalo laelekewa kuwa ndilo jina la sehemu iitwayo Hazara hivi leo, ambapo sehemu nyingine ya jimbo hilo inaitwa Ghaur. Ndani ya kitabu kiitwacho *Tabaqat-i-Nasri*, ambamo kuna taarifa ya kutekwa kwa Afghanistan na Changiz Khan, imeelezwa kwamba katika zama za ukoo wa kifalme wa Shabnisi paliishi kabilia liitwalo Banii Israeli ambao

baadhi yao walikuwa wafanya biashara hodari. Mnamo mwaka 622 baada ya kuzaliwa Yesu, karibu na ule wakati ambapo Mtume wetu Mtukufu Muhammad (amani na rehema za Mwenyezi Mungu juu yake) alitangaza mwito wake, watu hawa walikalishwa katika eneo kuelekea Mashariki mwa Herat. Chifu mmoja wa Kikuraishi, Khalid bin Walid kwa jina, aliwaletea habari njema za majilio ya Mtume kwa nia ya kuwaleta chini ya bendera ya Mjumbe huyu wa Kimbingu (amani na rehema za Mwenyezi Mungu juu yake). Machifu watano au sita walijiunga naye, ambao mionganoni mwao Qais ndiye aliyekuwa kiongozi na ambaye jina lake lingine lilikuwa Kish. Baada ya kuukubali Uislam watu hawa walipigana kishujaa kuutetea Uislam na walipata ushindi mwingi, huku Mtukufu Mtume (amani na rehema za Mwenyezi Mungu juu yake) akiwapa zawadi nyingi walipokuwa wakirejea, akiwabarikia na kutabiri kwamba watu wale wangepata nguvu kubwa za utawala. Mtukufu Mtume alisema kwamba machifu wa kabila hili daima watajulikana kama Malik. Alimpa Qais jina la Abdul Rashid na akampa cheo cha 'Pathan'. Waandishi wa Kiafghan wanasema kwamba hili ni neno la Kisyria ambalo lina maana ya 'usukani'. Kwa kuwa huyu Qais aliyejiunga upya na Islam alikuwa kiongozi wa kabila lake, kama vile ulivyo usukani wa meli akapewa cheo cha 'Pathan'.

Haiwezekani kusema ni katika wakati gani Waafghan wa Ghaur walisonga mbele na kuja kulowea katika eneo lililopo kando kando ya Kandhar, ambako ndiyo maskani yao hivi leo. Hii ilitokea yumkini katika karne ya kwanza ya Kiislam. Waafghan wanashikilia kwamba Qais alimwoa binti wa Khalid bin Walid ambaye alizaa naye watoto wa kiume watatu ambao majina yao yalikuwa Saraban, Patan na Gurgasht. Saraban alikuwa na watoto wa kiume wawili walioitwa Sacharj Yun na Karsh Yun ambao wazao wao ni Waafghan, yaani Banii Israeli. Watu wa Asia - Minor, na wanahistoria wa Kiislamu wa nchi za Magharibi wanawaita Waafghan "Wasulaimanii".

Na katika kitabu kiiwtacho *The Encyclopaedia of India, Eastern and Southern Asia* kilichotungwa na E. Balfour, jalada la 3 imeelezwa kwamba watu wa Kiyahudi wamesambaa katika

majimbo ya kati, Kusini na Mashariki ya Asia. Katika siku za mwanzo watu hawa walikalishwa kwa makundi makubwa katika nchi ya Uchina; walikuwa na hekalu mahali paitwapo Yih Chu, ambapo ndiyo makao makuu ya wilaya ya Shu. Dakta Wolf alizunguka kwa muda mrefu akiyatafuta yale makabila kumi yaliyopotea ya Yahuda na Bin Yamin. Taarifa nyininge inaonyesha kwamba Mayahudi walipewa hifadhi ya ukimbizi katika nchi ya Tartary; walikutwa katika makundi makubwa kwenye majimbo yaliyo pembezoni mwa Bukhara, Merv na Khiva. Prester John, Mfalme wa Tartary, akiandika kuhusu milki zake katika barua kwa Alexis Comninus, Mfalme wa Constantinapole anasema kwamba ng'ambo ya mto huu (AMU) yapo yale makabila kumi ya Israeli ambao ingawa wanadai kuwa chini ya mfalme wao wenyewe, kwa hakika ni raia wake na ni watumwa wake. Tafiti za Dakta Moore zinaonyesha kwamba makabila ya Tartar yanayoitwa Chosan ni ya asili ya Kiyahudi na kwamba mionganii mwao zinapatikana alama za imani ya kale ya Kiyahudi: Kwa mfano wanashikilia desturi ya kutahiri. Waafghan wanayo simulizi kwamba wao ni yale makabila kumi yaliyopotea ya Israeli. Baada ya kutekwa kwa Yerusalem mfalme Nebuchadnezzar aliwakamata mateka na kuwakalisha katika nchi ya Ghaur karibu na Bamiyar. Kabla ya kuja kwa Khalid Bin Walid waliidumisha kwa uthabiti imani ya Kiyahudi.

Kimaumbile Waafghan wanafanana na Wayahudi kwa kila hali. Kama walivyo hao, ndugu mdogo huoa mjane wa kaka yake. Msafiri wa Kifaransa aitwaye L. P. Ferrier ambaye alipitia Herat anaeleza kwamba katika eneo hili kuna Waisraeli wengi ambao wana uhuru kamili wa kutekeleza desturi za imani yao. Mnamo karne ya kumi na mbili baada ya kuzaliwa Yesu, Rabbi Bin Yamin wa Toledo (Hispania) alijitosa katika kuyatafuta haya makabila kumi yaliyopotea. Anaeleza kwamba Wayahudi hawa wamelowea katika nchi za Uchina, Iran na Tibet.

Kwenye kitabu chake cha kumi na moja katika msururu wa taarifa kuhusu Mayahudi walitoroka utumwani wakiwa na mtume Ezra, Josephus ambaye aliandika historia ya kale ya Mayahudi

mnamo mwaka 93 baada ya kuzaliwa Yesu, anaeleza kwamba hayo makabila kumi yalikalishwa ng'ambo ya Euphrates hata wakati ule, na kwamba idadi yao haikuweza kuhesabika.

Kwa kusema "ng'ambo ya Euphrates" ina maana ya Uajemi na maeneo ya Mashariki. Na Mtakatifu Jerome ambaye aliishi katika karne ya tano baada ya kuzaliwa Yesu, akiandika kuhusu Mtume Hosea kuhusiana na suala hili, anasema kwenye ukingo wa ukurasa kwamba tangu siku ile makabila kumi (ya Waisraeli) yamekuwa chini ya mflame Parthya, yaani Paras, na bado hayajatolewa utumwani. Katika jalada la kwanza la kitabu hicho hicho imeelezwa kwamba Count Juan Steram anaandika kwenye ukurasa wa 233-34 wa kitabu chake kwamba Waafghani wanakiri kwamba baada ya kuteketezwa kwa Hekalu la Yerusalem, Nebuchadnezzar aliwapeleka uhamishoni kwenye eneo la Bamiyan. (eneo hili linatangamana na Ghaur, na liko Afghanistan). Na katika kitabu kiitwacho *A Narrative of a Visit to Ghazni, Kabul and Afghanistan* kilichotungwa na G. T. Vigne, F.G.S. (1840) kwenye ukurasa wa 166 imeelezwa kwamba mtu mmoja aitwaye Mullah Khuda Dad alisoma kutoka kwenye kitabu kiitwacho Majma-ul-Ansab kwamba mwana mkuu wa Yakubu alikuwa Yahuda ambaye mwanawewe alikuwa Usrak; mwana wa Usrak alikuwa Aknur; mwana wa Aknur alikuwa Maalib; na wa Maalib alikuwa Ka-Farlai; wa Ka-Farlai alikuwa Qais, wa Qais alikuwa Talut; wa Talut alikuwa Armea na mtoto wa Armea alikuwa Afghan ambaye wazao wake ni watu wa Afghan ambao wanaitwa kwa jina la mtu huyu. Afghan alikuwa mtu wa rika moja na Nebuchadnezzar; aliiwa mzao wa Israeli na alikuwa na watoto wa kiume arbaini. Wakati wa kizazi cha 34, baada ya miaka 2000 akazaliwa Qais, aliyeishi katika zama za Muhammad (Mtukufu Mtume, amani na rehema za Mwenyezi Mungu juu yake). Wazao wake waliongezekwa na kufikia vizazi 64. Mwana mkuu wa Afghan aitwaye Salm alihama kutoka nyumbani kwake nchini Syria na kulowea katika Ghaur Mashkoh, karibu na Herat. Wazao wake wakasambaa nchini Afghanistan.

Na katika *Encyclopaedia of Geography* kilichotungwa na James

Bryce, F.G.S. (London, 1856) kwenye ukurasa wa 11 imeelezwa kwamba Waafghan wanafuatilizia uzao wao kwa Saul, Mfalme wa Kiisraeli na wanajiita kuwa ni wazao wa Israeli. Alexander Burns anasema kuwa Waafghan wanaeleza kwamba wana asili ya Kiyahudi; kwamba mfalme Babul aliwateka na kuwakalisha katika eneo la Ghaur ambalo liko Kaskazini - Magharibi ya Babul; kwamba hadi kufikia mwaka 622 baada ya kuzaliwa Yesu waliendelea na imani yao wenyewe ya Kiyahudi, lakini kwamba Khalid bin Abdullah (lilikosewa badala ya Walid) alimwoa binti wa chifu wa kabile hili na akawafanya waukubali Uislamu katika mwaka ule.

Na katika kitabu kiitwacho *History of Afghanistan* kilichotungwa na Kanali G. B. Malleson na kutangazwa mjini London (1878), kwenye ukurasa wa 39 imeelezwa kwamba Abdullah Khan wa Herat, yule msafiri wa Kifaransa Friar John na Sir William Jones (ambaye alikuwa mustashiriki mkubwa) wanatokana na Banii Israeli; wao ni wazao wa yale makabila kumi yaliyopotea. Kitabu Kiitwacho *History of the Afghan* kilichotungwa na L. P. Ferrier kilichotafsiriwa na Kapteni W. M. Jasse na kutangazwa mjini London (1858) kimerikodi kwenye ukurasa wa 1 kwamba wengi mionganoni mwa wanahistoria mustashrikina wana maoni kwamba watu wa Afghan wametokana na yale makabila kumi ya Israeli na kwamba maoni ya Waafghan wenyewe ni hayo hayo. Mwanahistoria huyo huyo anasema kwenye ukurasa wa 4 wa kitabu hiki kwamba Waafghan wanao ushahidi kuwa wakati wa kuvamiwa kwa India, Nadir Shah alipewa na machifu wa kabile la Yusuf-Zai zawadi ya Biblia iliyoandikwa kwa Kiebrania mahali paitwapo Peshawar, na pia alipewa vitu vingine kadhaa vilivyoifadhiwa na familia zao kwa ajili ya kufanya tafrija za kidini za imani yao ya zamani. Walikuwepo Mayahudi pia kwenye kambi ya Nadir Shah. Walipoviona vitu vile wakavitambua mara moja. Tena mwanahistoria huyo huyo anaeleza kwenye ukurasa wa 4 wa kitabu chake kwamba kwa maoni yake maoni ya Abdullah Khan wa Herat ni ya kuaminika.

Yakielezwa kwa muhtasari maoni hayo ni kwamba: Malik Talut

(Saut) alikuwa na watoto wa kiume wawili Afghan na Jalut. Afghan ndiye aliyekuwa mzee mheshimiwa wa watu hawa. Baada ya utawala wa Daudi na Suleiman kulikuwako na mapigano ya wenyewe kwa wenyewe baina ya makabila ya Israeli ambapo kutokana na mapigano hayo kila kabile likajitenga na mengine na hali hii ya mambo ikaendelea hadi wakati wa Nebuchadnezzar. Nebuchadnezzar akafanya uvamizi na kuua Mayahudi elfu sabiini. Akauteketeza mji na kuwachukua Mayahudi waliosalia hadi Babel wakiwa wafungwa. Baada ya maangamizi haya watoto wa Afghan walikimbia kwa hofu kutoka Judea hadi Arabia na wakaishi kule kwa muda mrefu. Lakini kwa kuwa maji na ardhi vilikuwa adimu, na watu na wanyama walikuwa wote katika dhiki kubwa, wakaamua kuhamia India. Kundi la ma-Abdali lilisalia nchini Arabia na wakati wa Ukhilifa wa Hadhrat Abu Bakar mmoja wa machifu wao alianzisha kiungo kwa ndoa kati yao na Khalid Bin Walid . . . Wakati Iran ilipotekwa na Arabia, watu hawa walihama kutoka Arabia na wakajikalisha katika majimbo ya Iran ya Faras na Kirman. Walikaa kule hadi ulipofanyika uvamizi na Changiz Khan. Hawa ma-Abdali hawakuweza kujisaidia dhidi ya ukatili wa Changiz Khan. Wakaja India kupitia Makran, Sindh na Multan. Lakini hawakuwa na amani mahali hapa. Hatimae wakaenda Koh Sulaiman na kukaa pale. Wanachama wengine wa hili kabile la ma-Abdali pia waliungana nao kule.

Wanajumuika kufanya makabila 24 - wazao wa Afghan ambaye alikuwa na wana watatu, yaani Saraband (Seraban), Arkash (Gargasht), Karlan (Batan). Kila mmoja wao alikuwa na watoto wa kiume wanane ambao walizaliana hadi kufikia makabila ishirini na manne, kila kabile likiitwa kwa jina la kila mtoto wao wa kiume mmoja. Majina yao pamoja na majina ya makabila yao yanatolewa hapa chini:

Wana wa Seraband

Jina la kabilu

Abdal
Baboor
Wazir

Abdali
Baboori
Waziri

Lohan	Lohani
Barch	Barchi
Khugiyan	Khugiyani
Sharan	Sharani

Wana wa Gargasht (Arkash) Jina la kabilia

Khijl	Khijli
Kakar	Kakari
Jamurin	Jamurini
Saturiyan	Saturiyan
Peen	Peeni
Kas	Kasi
Takan	Takani
Nasar	Nasari

Wana wa Karlan Jina la kabilia

Khatak	Khataki
Afrid	Afridi
Toor	Toori
Zaz	Zazi
Bab	Babi
Banganesh	Banganeshi
Landipoor	Landipoori

Na kitabu kiitwacho *Makhazan-i-Afghani* cha Khawaja Nimatullah wa Herat, kilichoandikwa mnamo mwaka 1018 Hijriyya katika zama za Mfalme Jahangir, na tafsiri yake kutangazwa na Professa Bernhard Doran wa Chuo Kikuu Cha Kharqui (London, 1836) kimehodhi katika kurasa zilizotajwa hapa chini kauli zifuatazo:

Katika Sura ya 1 kuna historia ya Yakubu Israel ambaye kutokana naye kinaanza kizazi cha watu hawa (Waafghan).

Katika sura ya 2 kuna historia ya Mfalme Talut, yaani uzao wa Waafghan unafuatiliwa kwa Talut.

Kwenye ukurasa wa 22 na 23 imeelezwa: Talut alikuwa na wana

wawili Barkhiya na Armiyah. Barkhiya alikuwa na mwana mmoja, Asaf, na Afghan alikuwa na wana 24 na hakuna mtu mionganii mwa Waisraeli aliyingana na wazao wa Afghan. Kwenye ukurasa wa 65 imeelezwa kwamba Nebuchadnezzar aliitwaa nchi yote ya Sham (Syria), n.k., akayatia uhamishoni makabila ya Kiisraeli na kuyapeleka kwenda kukaa Ghaur, Ghazni, Kabul na Firoz ambako ndiko hasa wazao wa Asaf na Afghan walikofanya maskani yao.

Na kwenye ukurasa wa 37 na 38 wa kitabu hiki, kwa mamlaka ya mtunzi wa *Majma-ul-Ansab*, na kwa mamlaka ya Mastaufi ambaye ndiye mtunzi wa *Taarikh Buzidah*, imeelezwa kwamba wakati wa uhai wa mtukufu Mtume (amani na rehema za Mwenyezi Mungu juu yake) Khalid Bin Walid aliwakaribisha kwenye Uislamu wale Waafghan ambaa baada ya tukio la utawala na Nebuchadnezzar walifanya makazi yao katika eneo la Ghaur. Machifu wa Kiafghan chini ya uongozi wa Qais ambaye alikuwa mzao wa Talut katika kizazi cha 37, walikuja kwa Mtukufu Mtume (amani na rehema za Mwenyezi Mungu juu yake). (Hapa Talut-Saul amepewa uzao wa Abdul Rashid Qais). Mtukufu Mtume (amani na rehema za Mwenyezi Mungu juu yake) aliwatunuku machifu wale cheo cha Pathan ambacho maana yake ni "usukani wa meli". Baada ya muda kidogo machifu wale walirudi kwenye eneo lao na wakaanza kuhubiri Uislamu.

Na katika kitabu hicho hicho *Makhzan-i-Afghan* kwenye ukurasa wa 63 imerikodiwa kwamba Farid-ud-Din Ahmad anatoa kauli ifuatayo kuhusiana na majina Banii Afghana na Banii Afghan katika kitabu chake kiiwacho *Rasalah Ansab-i-Afghaniyah*: Baada ya Nebuchadnezzar, Majusi waliwateka Waisraeli na maeneo ya Sham, na alipoiteketeza Yerusalem aliwakamata mateka Waisraeli na kuwapeleka uhamishoni wakiwa watumwa. Aliondoka na mengi mionganii mwa makabila yao ambayo yaliifuata Sheria ya Musa na kuwaamrisha waachane na imani ya mababu zao na wamwabudu yeye badala ya Mungu, jambo ambalo walikataa kulifanya. Hatimae Nebuchadnezzar aliwaua watu elfu mbili mionganii wa watu wao waliokuwa na akili na

hekima nyingi sana na kuwaamuru waliosalia wajiondoe kwenye ufalme na kwenye eneo la Sham. Baadhi yao waliondoka kwenye eneo la Nebuchadnezzar wakiwa chini ya chifu mmoja na kwenda kwenye vilima vya Ghaur. Wazao wao walikaa mahali hapa, wakazaliana, na watu wakaanza kuwaita Banii Israail, Banii Asaf na Banii Afghan.

Kwenye ukurasa wa 64 mtunzi huyo anaeleza kwamba kumbukumbu zenyе kuaminika kama vile *Taarikh-i-Afghani*, *Taarikh-i-Ghaur*, n.k. zinayo madai kwamba Waafghani takriban wote ni Banii Israail na baadhi yao wanatokana na Wamisri asilia. Zaidi ya hayo Abdul Fazl anaeleza kwamba baadhi ya Waafghan wanajihesabu kuwa wanatokana na asili ya Kimisri, sababu waitoayo ikiwa kwamba wakati wa Banii Israail waliporejea Misri kutoka Yerusalem, hili kabilia (yaani Waafghan) walihamia India. Kwenye ukurasa wa 64 Farid-ud-Din Ahmad anasema kuhusu jina 'Afghan': Kuhusu hili jina Afghan baadhi wamerikodi kwamba baada ya kupelekwa uhamishoni (nje ya Syria) walikuwa kila mara 'wakiomboleza na kulia' (*faghan*) katika kukumbuka nyumbani kwao. Kwa hiyo wakaitwa Waafghan. Sir John Malcom naye pia ana maoni hayo hayo; tazama *History of Persia*, Jalada la 1 ukurasa wa 101.

Kwenye ukurasa wa 63 imeratibiwa kauli ya Mahabat Khan: "Kwa vile wao ni wafuasi na ndugu wa Suleiman (amani juu yake), kwa hiyo wao wanaitwa na Waarabu Wasulaimani".

Kwenye ukurasa wa 65 imeandikwa kwamba takriban tafiti zote za wanahistoria mustashrikina zinaonyesha kwamba maoni ya watu walio Waafghan wenyewe ni kwamba wanatokana na asili ya Kiyahudi. Baadhi ya wanahistoria wa hivi leo wameyachagua maoni hayo hayo au yavezekana sana wameyahesabu kuwa ni ya kweli.

Ama kuhusu kutumiwa kwa majina ya Kiyahudi na Waafghani kunakosemekana kuwa kunatokana na kuukubali kwao Uislamu, hakuna jambo lo lote lenye kuunga mkono maoni ya mfasiri huyu Bernhard Doran.

Katika sehemu za Kaskazini na za Magharibi ya Punjab yako

makabila yenye asili ya Kihindu ambayo yamejiunga na Uislamu lakini majina yao hayatanguliwi na majina ya watu wa Kiyahudi, jambo linaloonyesha wazi wazi kwamba kwa kuijunga na Uislamu si lazima watu wapewe majina ya Kiyahudi.

Kwa maumbile, Waafghan wana mfanano wa ajabu na Wayahudi, ukweli ambao wanaukiri hata wale wanazuoni ambao hawachangii katika maoni kwamba Waafghani wana asili ya Kiyahudi. Na huu waweza kuwa ndio uthibitisho pekee uliopo wa kutokana kwao na Mayahudi. Kuhusiana na jambo hili maneno ya Sir John Malcom ni haya:

"Asili ya makabila ya Kiafghan yanayokaa katika ukanda wa milima baina ya Khorasan na Indus inafuatiliziwa kwa njia nyingi na wanahistoria mbalimbali. Baadhi yao wanadai kwamba wametokana moja kwa moja na makabila ya Kiyahudi yaliyotiwa utumwani na Nebuchadnezzar, na wale machifu wakuu wanasemekana kuwa wanazinasibisha familia zao kwa Daudi na Saul. Ingawa haki yao ya kukubalika kwenye uzao huu wa fahari ni yenye kutiliwa shaka, ni dhahiri kutokana na maumbile yao binafsi na desturi zao nyingi kwamba wao ni taifa lililo tofauti na Waajemi, Watartar na Wahindi na kwamba hili peke yake laelekeea kuipa itibari ndogo ile kauli ambayo inakinzwa na kweli nyingi zenye nguvu na ambayo kuihusu hiyo hakuna uthibitisho wa moja kwa moja uliokwisha tolewa."

Kama kufanana kwa maumbile kati ya watu wa aina moja na watu wa aina nyingine kunaweza kuashiria jambo lo lote, Wakashmiri wakiwa na maumbile yao ya Kiyahudi bila shaka wataonekana kuwa wenyе asili ya Kiyahudi. Hili limetajwa siyo na Bernier tu bali na Forster pia, na huenda na wanazuoni wengine.

Ingawaje Forster hakubaliani na maoni ya Bernier, anakiri kwamba alipokuwa mionganoni mwa Wakashmiri alidhani alikuwa katikati ya watu wa Kiyahudi.

Kuhusu neno "Kashmiri" yanajiteze maneno yafutayo kwenye ukurasa wa 250 wa Kamusi ya Jiografia ya A. K. Johnston:

Kwenye ukurasa wa 250, chini ya kichwa cha habari

CASHMERE: "Wazalendo wote ni watu warefu wenye mitambo ya miili yenye nguvu na maumbile ya kijanadume - wanawake ni vipande vya wanamama walio warembo wa sura na wenye pua nyembamba na nyuso nyembamba zinazofanana na zile za Mayahudi".

Katika Civil & Military Gazette (23 Novemba, 1898 ukurasa wa 4), chini ya kichwa cha habari 'Sawati and Afridi' pamenakiliwa waraka wenye thamani na wenye kuvutia sana uliowasilishwa kwenye Kitengo cha Elimu ihusuyo habari zote za binadamu cha Chama cha Kiingereza kwenye mmoja wa mikutano yake ya hivi karibuni, ambao utasomwa kwenye kikao cha majira ya baridi mbele ya Kamati ya Utafiti wa Elimu ihusuyo habari zote za binadamu. Waraka huo umeripotiwa hapa chini:

"Hapa chini hatutaweza kuandika maneno yote ya ule waraka wenye thamani kubwa sana na wenye kuvutia mno uliochangwa kwenye Kitengo cha elimu ihusuyo habari zote za binadamu kwenye mkutano wa hivi karibuni wa Chama cha Kiingereza, na ambao bado utasomwa mbele ya Taasisi ya Elimu ihusuyo habari zote za binadamu kwenye mojawapo ya mikutano yake ya majira ya baridi."

"Wakazi wa asili wa njia hizi za milimani za Magharibi mwa India wanatambulika katika historia ya mwanzoni sana, mengi ya makabila hayo yakiwa yametajwa na Herodotus na wanahistoria wa Alexander. Katika zama za baina ya mwaka 500 na mwaka 1500 pori chafu lisilolimwa na miliima waliyoikalia liliitwa Roh, na wakazi wake wakaitwa Rohilla, na kwamba mengi mionganini mwa makabila haya ya mwanzoni ya Rohilla au Pathan yalikuwa katika sehemu zao muda mrefu kabla ya haya makabila ya Afghan yaliyotanda hayajafikiriwa. Waafghan wa aina yo yote ile hivi sasa wanahesabiwa kama ni ma-Pathan kwa sababu wote wanazungumza lugha ya ki-Pathan na ki-Pushto. Lakini hawakubali kwamba wote wanatokana na ukoo mmoja, wakijidaia wenyewe kwamba wao ni Banii Israeil wazao wa yale makabila ambayo yalitekwa na Nebuchadnezzar na kupelekwa utumwani nchini Babylonia. Lakini wote mionganini mwao wamechagua kuzungumza lugha ya ki-Pushto na wote wanazitambua sheria za kimila zile zile za ki-Pathan ziitwazo Paktanwali, ambazo katika mionganini mwa vipengele vyake vinaashiria kwa njia ya ajabu kwenye zama za utume wa Musa na kwenye mila za kale za mataifa ya Rajput."

ALAMA ZA KIISRAELI

Kwa hiyo ma-Pathan ambao hivi karibuni tumekuwa tukijishughulisha nao sana, wanaweza kugawanyika katika jamii kubwa mbili, yaani makabila na koo kama vile Waziriyya Afridiyya, Orkzaiyya n.k. ambao wana asili ya Kihindi, na wale Waafghan ambao wanadai kwamba wametokana na makabila ya Sham na ambao wanawakilisha taifa lililoenea kwa wingi katika sehemu za mpaka wetu; na kwa uchache inaonekana kuwa ni jambo linalowezekana kwamba hii Paktanwali ambayo ni sheria isiyoandikwa na ambayo inakubalika sawasawa na wote hao inaweza kuwa na asili iliyochanganyika kwelikweli. Tunaweza tukakuta ndani yake sheria za Musa zikiwa zimepandikizwa katika mila za Rajput na kufanyiwa mabadiliko na desturi za Kiislamu.

Waafghan ambao wenyewe wanajiita Wadurani na ambao wamefanya hivyo tangu kuanzilishwa kwa Ufalme wa Kidurani yapata karne moja na nusu iliyopita wanasema kwamba wanafuatilitiza uzao wao kutoka kwenye makabila ya Kiisraeli kupitia kwa babu mmoja aitwaye Kish, ambaye Mtume Muhammad alimpa jina Pathan (ambalo kwa Kisiria lina maana ya usukani wa meli), kwa sababu alikuwa awaongoze watu wake kwenye mikondo ya Uislamu. Lakini tumekwisha ona kwamba utaifa wa Kipaktan au Kipathan ni mkongwe sana mno kuliko Uislam. Ni vigumu kuelezea kuenea kwa majina ya Kiisraeli mionganoni mwa Waafghani bila kukiri kuwepo kwa kiasi fulani cha uhusiano wa awali na taifa la Kiisraeli.

Ngumu zaidi ni kuelezea kwa uhakika maadhimisho kama vile kwa mfano kudumishwa kwa Sikukuu ya Pasaka (ambako kwa uchache kumeigizwa kwa namna ya ajabu na taifa la Waafghan) au mshikilio ambao kwao Waafghan wenye elimu chache wanaidumisha desturi hii, bila kuwa na aina fulani ya misingi ya ukweli ya asili kuhusu jambo hili. Bellew anafikiri kwamba uhusiano huu wa Kiisraeli waweza kuwa ni uhusiano halisi, lakini anaainisha kwamba kwa uchache moja mionganoni mwa matawi matatu makubwa ya jamii ya Kafghan ambalo kulingana na simulizi lililotokana na Kish, linaitwa kwa jina la (Sarabaur) ambalo kwa hakika ndilo jina la kale la Kipushtu lililotumika kutaja taifa la jua la Warajput ambao makoloni yao yanajulikana kuwa yalihamia nchini Afghanistan baada ya kushindwa kwao na Wachandraban - taifa la mwezi katika ushindani huu mkubwa, wale Mahabharat walio tajwa katika kumbukumbu za mwanzoni za India. Hivyo Muafghan anaweza kabisa kuwa Muisraeli

aliyechanganyika na makabila ya kale ya Warajput, na kwangu mimi huu ndio kila mara ulioonekana kuwa ufumbuzi mzuri zaidi wa lile tatizo la asili yake. Kwa vyo vyote vile, Muafghan wa kisasa anashika msimamo wake wa kuwa mmojawapo mionganini mwa lile taifa teule na mzao wa Ibrahimu kutokana na misingi ya simulizi na anatambua tu udugu wake na Mapathan wengine kwa njia ya kuzungumza lugha moja na kutumia sheria moja ya mila za kikabila".

Nukulu zote hizi kutoka katika vitabu vya waandishi mashuhuri sana, vikifikiwa kwa pamoja vitamshawishi mtu aliye muadilifu kuamini kwamba Waafghan na Wakashmiri wanaopatikana nchini India, mpakani na katika nchi za jirani, kwa hakika ni Banii Israili. Katika sehemu ya pili ya kitabu hiki Mungu Akipenda nitathibitisha kwa ufanuzi zaidi kwamba shabaha ya msingi iliyosababisha safari ndefu ya Yesu kwenda India ilikuwa kwamba ili aweze kutekeleza wajibu wake wa kuyahubiri makabila yote ya Waisraeli, ukweli ambao ameutaja katika Injili.

Kwa hiyo si jambo la kushangaza ya kwamba alilazimika kuja India na Kashmir. Bali lingelikuwa jambo la kushangaza sana iwapo angepaa mbinguni bila kutekeleza wajibu wake. Na kufikia hapa naufunga mjadala wa sasa.

Amani iwe kwa wale wenye kuongozwa njia iliyosawa.

MIRZA GHULAM AHMAD

MASIH ALIYEAHIDIWA

Qadian, Wilaya ya Gurdaspur.

KIAMBATANISHO Na. 1

P. W. Rhys Davis, M. A., Phd.

Buddhism

Kilichotangazwa na: *The Society for Promoting Christian Knowledge, Northumberland Avenue, Charing Cross W. C. 43, Queen Victoria street, London, E. C. 1887.*

"Mama yake Buddha anasemekana kuwa alikuwa bikra." Ukurasa wa 183. "Mama yake alikuwa mbora na mtakatifu kuliko mabinti wote wa binadamu."

Zingatia: Chini kabisa ya ukurasa wa 183 Davis anamnukulu Mtakatifu Jerome.

Mtakatifu Jerome anasema (Contra Sovian bk. 1). "Imepokelewa kama simulizi mionganoni mwa firqa ya wanafalsafa wa kale wa Kihindu wa India kwamba Buddha, mwanzilishi wa mfumo wao alizaliwa na bikra kutoka ubavuni mwake."

KIAMBATANISHO Na. 2

The Hibbert Lectures - 1831

Indian Buddhism. kilichotungwa na T. W. Rhys Davis, Chapa ya 2.

Kimetangazwa na: Williams & Norgate, 14,

Henrietta Street, Covent Garden

London. 1891

Ukurasa wa 147. "Yote haya yana faida ya aina yake kutokana na mtazamo wa kimalinganisho. Ni usemi unaotokana na msimamo wa Kibuddha ambao unaiweka kando ile nadharia ya kuwepo kwa Mungu Mkuu, au wazo linalofanana sana na lile ambalo limeelezwa katika maandiko ya kistaarabu wakati Yesu anapoonyeshwa kama Udhahirisho wa Mungu lililofanywa kuwa mwili, kama Mkate wa uhai, na si suala la bahati nasibu kwamba wafuasi wa dini hizi mbili wenye imani iliyo tofauti

na walio wengi baadae walizitumia dhana za Buddha na Neno kama misingi ya nadharia zao za chanzo. Ni mfano mpya tu wa njia ambayo kwayo mawazo ya namna moja katika akili zinazolingana yanakuja kubadilishwa kwa njia zinazofanana sana. Kwa wafuasi w a Buddha wa mwanzoni, Chakka-Vatti Buddha alikuwa kama alivyokuwa Masihi Neno kwa Wakristo wa mwanzoni. Katika kadhia zote mbili, yale mawazo ya namna mbili yanafanana, yanaingiliana na yanajalizana. Katika kadhia zote mbili mawazo hayo ya aina mbili kwa pamoja yanafunika takriban uwanja ule ule kama unaoruhusiwa na misingi tofauti ya mafundisho hayo ya aina mbili. Na ni mzunguko wa mawazo ya Chakka-Vatti Buddha katika kadhia moja, na Masihi Neno katika kadhia nyingine, ambao ndio wenye ushawishi katika kuamua kwamba maoni ya maandiko ya habari za maisha ya watu ya Wakristo wa mwanzo kuhusu mabwana wakubwa wao mbalimbali yalikuwa ni yale yale, na yaliongoza kwenye matokeo yanayofanana; ingawaje maelezo ya kinaganaga ya maoni hayo hayafanani kwa hali yo yote ile katika kadhia hizi mbili."

KIAMBATANISHO Na. 3

Sir M. M. Williams, Buddhism (John Muray, London 1889).

Ukurasa wa 135. Alisema kujihusu ye ye mwenyewe (Maha-Vagga 1.6.8) "Mimi ni mtiishaji wa kila hali (Sabbabhibha) mwenye hekima kwa kila hali; sina madoa, ninayo elimu niliyopata kwa njia yangu mwenyewe; sina mshindani (Patipuggalo); mimi ndiye Chifu Arhat - mwalimu mkuu. Mimi peke yangu ndiye mwenye hekima kikamilifu (Sambuddha); mimi ndiye mshindi (Jina); mioto yote ya tamaa huzimwa (Sitibhuto) katika nafsi yangu; ninayo raha ipatikanayo baada ya kifo (Nibbuto)." Ukurasa wa 126. Usiue kiumbe cho chote chenye uhai. 2. Usiibe. 3. Usifanye zinaa. 4. Usiseme uwongo. 5. Usinywe vinywaji vikali. 6. Usile chakula isipokuwa katika nyakati zilizowekwa. Usitumie maua, mapambo au manukato. Usitumie kitanda chenye miguu mirefu au kipana, bali mkeka tu uliotandikwa ardhini. Jiepushe na kucheza ngoma, kuimba, muziki na matamasha ya kidunia. 10. Usimiliki dhahabu

au fedha ya aina yo yote na usipokee vitu hivyo." (Maha-Vagga 1.5.6). Amri hizi kumi za Kibuddha zaweza kuwa zimeambukizwa kutoka Amri kumi za Musa."

KIAMBATANISHO Na. 4

Mtunzi: H. T. Princep

Kitabu: *Tibet, Tartary and Mongolia.*

"Misafara ya mwanzo katika Tibet yenyewe ambayo imewasilishwa kwetu ni ile ya Mapadre wa Usharika wa Yesu, Grueber na Dorville ambao walirejea kutoka Uchina kwa kupitia njia ile mnamo mwaka 1661 baada ya safari ya Marco Polo kuelekea Magharibi. Walikuwa ndio Wakristo wa kwanza kutoka Ulaya ambao wanajulikana kuwa walipenya katika sehemu zenye watu wengi za Tibet, kwani kama tulivyokwisha eleza, safari ya Marco Polo ilikuwa upande wa Kaskazini Magharibi kutokana na vyanzo vya Oxus. Padre Grueber alishitushwa sana na kufanana kwa ajabu alikoona na pia itikadi kama vile katika taratibu za dini za wafuasi wa Buddha walioko Lassa na zile za Imani yake mwenyewe ya Kiroma. Aligundua, kwanza: Kwamba vazi la Walama linafanana na lile tulilorithishwa katika michoro ya kale kama ndilo vazi la wanafunzi wa Yesu. Pili: kwamba ile nidhamu ya majumba ya watawa na ya sharika mbalimbali za Walama au Mapadre ilikuwa na mfanano ule ule kama wa Kanisa la Roma. Tatu: Kwamba ile dhana ya kugeuka mtu ilikuwa ya kawaida kwa pande zote mbili kama pia ilivyokuwa ile imani ya pepo na barzakh. Nne: akanena kwamba walichagua viongozi, walitoa sadaka, walisali na kutoa dhabihu kwa ajili ya wafu kama wafanyakyo Wakatoliki wa Roma. Tano: Kwamba walikuwa na majumba ya watawa yaliyojawa na watawa na mawalii waliofikia idadi ya 30,000 karibu na Lassa, ambao walifunga nadhiri zao za umaskini, utii na utaratibu kama wafanyakyo watawa wa Kiroma, licha ya nadhiri zingine. Na sita: Walikuwa na waungamaji waliopasishwa na Walama wakubwa au maaskofu; na kwa hiyo walikuwa na uwezo wa kusikiliza maungamo na kutoa adhabu ya kutubisha, na kutoa msamaha. Licha ya yote haya ilikutikana desturi ya kutumia maji

matakatifu, ya ibada ya kuimba kwa zamu, ya kuwasalia wafu, na mfanano uliokamilika kati ya mavazi ya kawaida ya Walama wakuu na wakubwa na yale ya sharika mbalimbali za jamii ya Mapadre wa Kiroma. Zaidi ya hayo wamisionari hawa wa mwanzo waliongozwa katika kufikia uamuzi kutokana na yale waliyoyaona na kuyasikia, kwamba vitabu vya kale vya Walama vilikuwa na alama za dini ya Kikristo ambayo ni lazima, walifikiria, iwe imehubiriwa katika zama za wanafunzi wa Yesu." (Ukurasa wa 12 -14)

Kisha kuhusu kutokea kwa Mkombozi, mtunzi huyo H. T. Princep anaandika katika kitabu hicho hicho (*Tibet, Tartary and Mongolia*) kwenye ukurasa wa 171:

"Matazamio ya wengi ya kuzaliwa kwa Mtume Mkubwa, Mkombozi au Mwokozi, ambayo yametajwa hata na Tacitus kama yaliyokuwa yameenea sana katika kipindi cha kutokea kwa mwanzilishi wa dini ya Kikristo, hapawezi kuwa na shaka yalikuwa na asili ya Kibuddha na kamwe hayakuwa ya Wayahudi peke yao au yenye kutokana na msingi wa tabiri za maandiko yao matakatifu tu."

Yakiwa maelezo yaliyoandikwa chini ya ukurasa wa 171 mtunzi huyo aliendelea kuandika:

"Kutokea kwa Buddha mwingine miaka elfu moja baada ya Gautama au Sakhya Muni kumetabiriwa wazi wazi katika Pitakattayan na Atha-Katha. Gautama anajitangaza mwenyewe kuwa ndiye Buddha wa ishirini na tano na anasema, "Bagwan Metteya bado atakuja. Hili jina Metteya lina mfanano usiokuwa wa kawaida na neno Masihi."

KIAMBATANISHO Na. 5

Hapa kuna maneno yaliyochotwa kutoka katika kitabu kiitwacho "*The Mystery of the Ages*", kilichotangazwa mnamo mwaka 1887.

"Dini ya Kibuddha ni Ukristo wa Mashartiki na kwa hali hiyo imehifadhiwa vizuri zaidi kuliko Ukristo, dini ya Kibuddha ya Magharibi."

Kitabbu cha Sir M. Monier Williams, ukurasa wa 541, maelezo yaliyopo chini ya ukurasa.

1. Tsing. *A Record of The Buddhist Religion practised in India and the Malaya Archipelago*. (671 - 695 A.D.).

Kimetafsiriwa na J. Takakusu B. A. Ph. D. (Oxford. the Clarendon Press - 1896).

Kwenye ukurasa wa 223-224

"Ni jambo la ajabu kweli kweli kulikuta jina la Masihi ndani ya maandiko ya Kibuddha ingawa jina hilo limeingia humo kwa bahati mbaya sana. Kitabu hicho kinaitwa "*The New catalogue of the Buddhist Books* kilichotungwa katika zama za Chiang Yuan,: (A.D. 785 - 804), katika chapa ya Kijapani ya *Chinese Buddhist Books (Bodlerian). Library, Jap, 65 DD*, p. 73). (Kitabu hiki hakimo katika Katalogi ya Nanges)

"Isitoshe, jumba la Sanghayama la Sakya na jumba la watawa la Ta-Chin (Syria) yanatofautiana sana katika mila zao, na vitendo vyao vya kidini vinapingana kabisa vyenyewe kwa vyenyewe. King-Ching (Adam) alipaswa kupokeleza mafundisho ya Masihi (Mi-Shi-Ho), na Sakya Putiyiya-Sramanas aeneze maneno yenyeh hekima ya Buddha."

KIAMBATANISHO Na. 6

The Nineteenth Century, London, October 1894.

Vol. 3 July - December.

British Museum wo. P.P. 56, 39.

Kwenye ukurasa wa 517. "Katika makala ilioandikwa na Max Muller chini ya kichwa cha habari "Madai ya kukaa kwa Yesu nchini India" ambamo anamkosoa Nicolas Notovitch, ambaye alikwenda Tibet na kuona baadhi ya kumbukumbu za zamani za miswada katika Jumba la watawa wa Kibuddha la Himis ikizungumzia kuhusu Yesu Kristo kuwa aliywahi kuizuru nchi ya Tibet na Kashmir, na ambaye wakati wa kurejea kwake aliandika kitabu kwa lugha ya Kifaransa "*Vie inconnue de Je'sus-Christ*" Paris 1894. Nicolas Notovitch alikuwa Mrusi kiuraia."

"Lakini ingawa Notovitch hakuileta nyumbani hiyo miswada, kwa vyo vyote vile alionia, na bila kujifanya kuwa anajua lugha ya Kitibet, maneno hayo ya Kitibet yalitafsiriwa kwa ajili yake na mkalimani na ametangaza kurasa sabini za miswada hiyo kwa lugha ya Kifaransa katika kitabu chake "*Vie inconnue de Je'sus-Christ*". Ni dhahiri alikuwa amejitayarisha kwa ajili ya ugunduzi wa maisha ya Kristo mionganoni mwa wafuasi wa Buddha. Mifanano kati ya Ukristo na Dini ya Kibuddha imekuwa ikionyeshwa mara kwa mara hivi karibuni, na lile wazo kwamba Kristo alikuwa chini ya ushawishi wa itikadi za Kibuddha limewekwa mbele ya watu zaidi ya mara moja na waandishi mashuhuri. Tatizo hadi sasa limekuwa kugundua njia yo yote ya kweli ya kihistoria ambayo kwayo dini ya Kibuddha ingeweza kufika Falastin katika zama za Kristo. Notovitch anafikiri kwamba muswada alioukuta pale Himis unalieleza jambo hili kwa njia iliyo rahisi zaidi. Hakuna shaka, kama asemavyo, kuna katizo katika maisha ya Kristo, tuseme kuanzia mwaka wake wa kumi na tano hadi wa ishirini na tisa, wakati wa kipindi hicho Maisha ya Kristo yaliyokutwa nchini Tibet yanadai kwamba Yesu alikuwa nchini India, kwamba alijifunza lugha ya Kipali ya Sanskrit, kwamba aliyasoma ma-Veda na Kanuni za Kibuddha, na kisha akarejea Falastin akipitia nchi ya Uajemi ili kuja kuhubiri Injili. Kama tunamwelewa sawasawa Notovitch, maisha haya ya Kristo yamechukuliwa kutoka vinywa vya baadhi ya wafanyabiashara wa Kiyahudi waliokuja nchini India mara tu baada ya Kitendo cha Kusulubiwa. (ukurasa wa 237). Yalikuwa yameandikwa kwa Kipali, iliyo lugha takatifu ya Dini ya Kibuddha ya Kusini; nyaraka hizo za kuviringishwa baadae zililetwa Nepal na Makhada (Quaere Mazadhe) kutoka India yapata mwaka 200 A.D. (ukurasa wa 236) na kutoka Nepal zikapelekwa Tibet, na hivi sasa zimehifadhiwa kwa uangalifu mahali paitwapo Lhassa. Tafsiri za Kitibet za maandiko ya Kipali zinapatikana, anasema, katika majumba ya watawa mbalimbali ya Kibuddha, na mionganoni mwa mengine, zinapatikana katika jumba la watawa la mahali paitwapo Himis. Ni miswada hii ya Kitibet ambayo ilitafsiriwa pale Himis kwa ajili ya N. Notovitch alipokuwa amelazwa katika jumba hilo la watawa akiwa na mguu uliovunjika, na ni kutoka katika miswada hii ambamo ameyachukua Maisha yake mapya ya Yesu Kristo na kuyatangaza kwa

lugha ya Kifaransa pamoja na taarifa ya misafara yake. Kitabu hiki, ambacho kimekwisha pitia katika chapa kadhaa za Kifaransa, hivi punde kitatafsiriwa katika lugha ya Kiingereza."

KIAMBATANISHO Na. 7

Kitabu: *Buddha; His Life, His Doctrine, His Order.*

Mtunzi: Dr. Hermann Oldenberg,

Kimetafsiriwa kutoka Kijerumani

na

William Hoey, M.A., D. Lit

Mtangazaji: Williams & Norgate, 14,

Henrietta Street, Covent Garden, W.C.

London. 1882

Ukurasa wa 142. "Katika tukio la utabiri wa Buddha kumhusu Metteyya, Buddha anayefuata ambaye atatokea duniani katika siku za baadae sana inasemwa:

"Atakuwa kiongozi wa kundi la wanafunzi wenye kufikia idadi ya mamia ya maelfu, kama mimi nilivyo kuwa hivi sasa kiongozi wa makundi ya wanafunzi yenye kufikia idadi ya mamia". Cakkana Hisuttanta.

Ukurasa wa 149. "Kuhusu mke na mtoto wa Buddha fungu kuu la maneno ni 'Mahauagga', 154; Rahula anatajwa mara kwa mara katika maandiko ya Sutta kama mwana wa Buddha bila shughuli muhimu kunasibishwa kwake mionganoni mwa duru za wanafunzi na hadithi hiyo ya kale.

Ukurasa wa 103. Rahula ni jina la mwana wa Buddha. Yeye (Buddha) anasema, "Rahula ni mzaliwa wangu, Silsila imeanzishwa kwa ajili yangu."

Kwenye maelezo chini ya ukurasa wa 103. Katika jina Rahula yaonekana kuna kutajwa kwa Raha, Jua na Mwezi kumtiisha (Kumtia giza) Shetani.

KIAMBATANISHO Na. 8

Kitabu: *Travels in the Moghul Empire*

Mtunzi: Francois Bernier

Watangazaji: Archibald Constable, London 1891

"Lakini kuna alama nyingi za dini ya Kiyahudi zinazoweza kuonekana katika nchi hii. Wakati wa kuingia katika Ufalme huu baada ya kuivuka milima ya Peer-Punchal, wakazi katika vijiji vya mpakani walinishtusha kuwa wanafanana na Mayahudi. Nyuso zao na tabia zao na ile hali ya kipekee isiyoweza kuelezeaka ambayo inamwezesha msafiri kuwatofautisha wakazi wa mataifa mbalimbali, yote hayo yalioneckana kuwa yanapatikana kwa watu hao wa kale. Usiyachukulie haya ninayoyasema kuwa ni mawazo ya kujifurahisha tu, kwa vile kuonekana kama Wayahudi kwa wanavijiji hawa kulikwisha semwa na Padre wetu wa usharika wa Yesu na baadhi ya Wazungu wengine muda mrefu kabla sijatembelea Kashmir." (Ukurasa wa 930 - 932).

KIAMBATANISHO Na. 9

Mtunzi: George Forster.

Kitabu: *Letters on a Journey from Bengal to England.*

Kimetangazwa na: R. Faulder, London, 1808

"Kwa kuwaona Wakashmiri kwa mara ya kwanza katika nchi yao wenyewe nilidhani, kutokana na vazi lao, uumbwaji wa nyuso zao ambazo zilikuwa ndefu na zenye mpangilio mzuri, na aina za chakula chao, kwamba nimekuja mionganoni mwa taifa la Mayahudi." (Jalada la 2, ukurasa wa 20).

KIAMBATANISHO Na. 10

Mtunzi: H. W. Bellews, C.S.I

Kitabu: *Races of Afghanistan*

Kimetangazwa na: Thacker Spink & Co. 1884.

"Mapokeo ya watu hawa (Waafghan) yanawarudisha katika Syria kama ndiyo nchi yao ya makazi katika wakati ambapo walipelekwa utumwani na Bukhtanasar (Nebuchadnezzar) na kupandikizwa kama watu wa koloni katika sehemu mbalimbali za Uajemi na Media. Kutoka mwahali humu walihama kuelekea Mashariki wakati wa kipindi fulani kilichofuatia na kufika katika nchi ya milima ya Ghor ambapo waliitwa na watu majirani 'Banii Afghan' au 'Banii Israili' yaani, wana wa Afghan au wana wa Israeli. Katika kulithibitisha hili tunao ushahidi wa Nabii Idris ya kwamba yale makabila kumi ya Israeli ambayo yalichukuliwa utumwani, hatimae yalitoroka na kujipatia hifadhi ya ukimbizi katika nchi ya Arsareth ambayo inadhaniwa kuwa inashabihiana na nchi ya Hazara ya hivi leo na ambayo Ghor ni sehemu yake mojawapo. Pia imeelezwa katika Tabaqati Nasiri kwamba katika zama za ukoo wa kifalme wa kizalendo wa Shan Sabi kulikuwako na watu walioitwa Banii Israili katika nchi ile na kwamba baadhi yao walikuwa wakijishughulisha sana kufanya biashara na nchi zilizowazunguka."

KIAMBATANISHO Na. 11

Balfour, Edward. Surgeon General.

Kitabu: "*The Cyclopaedia of India and of Eastern and Southern Asia.*"

Chapa: Chapa ya tatu

Watangazaji: Bernard Quaritch, 15, Piccadilly, W.1

Mwaka: 1885.

Chini ya Kichwa cha habari Afghanistan - ukurasa wa 31:

"Pakhtun ndilo jina la kitaifa la Waafghan halisi; lakini Waafghan na Mapathan wanajiita pia Banii Israili." Pakhtun ni mtu mmoja na Pukhtuna ni jina la wingi la Waafghan. Neno hili linaleezwa kuwa ni la asili ya Kiebrania (Ibraniy), ingawaje baadhi yao wanasesma lina asili ya Kisiria (Syrianiy) na lina maana ya kujifungua na kuwekwa huru. Neno Afghan pia linasemekana kuwa na maana hiyo hiyo. Simulizi moja inasema kwamba baada ya kuzaliwa kwa Afghan mama yake akasema ghafula

kwa sauti kuu na mshangao, "Afghan", niko huru, na akampa jina hilo; simulizi nyingine inadai kwamba wakati wa uchungu wa uzazi alilia Afghan, Afghan, au Fighan, Fighan, maneno ambayo kwa Kiajemi yana maana ya huzuni, majonzi, ole! Afghan linadaiwa kuwa ni jina la wazao wa Kais tu.

"Neno Pathan linasemekana kuwa limetokana na neno Pihtan, lakabu inayodaiwa kuwa ilitolewa na Muhammad kwa Muafghan mmoja aitwae Kais.

"Asili yao imo katika utata, lakini wandishi kadhaa wanawafikiria kuwa ni wazao wa moja mionganoni mwa yale makabila kumi ya Israeli na haya ndiyo maoni ya baadhi ya Waafghan wenyewe. Waandishi wachache wanafikiria kwamba taifa hili halina asili ya Kiyahudi, bali kwamba wale walioleta dini ya Kiislamu mionganoni mwao walikuwamo Wayahudi waliosilimu.

"Kisha katika ukurasa wa 34 kwa mamlaka ya kitabu cha Elphinstone '*Kingdom of Caubul*' (ukurasa wa 182 - 185) imeandikwa:

"Mionganoni mwa hao Yusufzai hakuna mtu anayemwona mkewe mpaka sherehe za ndoa zikamiliike, na pamoja na Burdurani zote hizo kuna stara kubwa baina ya wakati wahusika wanapofungishwa uchumba na wakati wanapoozwa. Baadhi yao huishi na wakwe zao wa kiume wa baadae na kujipatia chakula chao kutokana na huduma zao, kama alivyofanya Yakobo (alipotaka kumwoa) Raheli, bila kuona hata kidogo shabaha ya matakwa yao.

"Mionganoni mwa Waafghan kama ilivyo mionganoni mwa Mayahudi, inafikiriwa kuwa ni jambo linalompasa ndugu wa marehemu kumwoa mjane wa marehemu huyo na ni jambo la aibu kubwa kwa ndugu huyo kwa mtu mwengine ye yote kumwoa mjane wake, na ni jambo la aibu kubwa kwa ndugu huyo kwa mtu mwengine ye yote kumwoa mjane huyo bila kibali cha ndugu huyo."

KIAMBATANISHO Na. 12

Narrative of a Mission to Bokhara in the years 1843 - 1845, (kipo katika majalada mawili), Rev. Joseph Wolff D. D., LL.D.

Kimetangazwa na John W. Parker, West Strand,
London, 1845.

Jalada la 1. Chapa ya pili.

Ukurasa wa 9.

"Kutokana na mazungumzo mbalimbali na Waafghan mjini Khorassaun na kwingineko nilijifunza kwamba baadhi yao wanaona fahari ya kuwa na asili itokanayo na wana wa Israeli, lakini natilia shaka ukweli wa simulizi hiyo upande mmoja."

Ukurasa wa 13.

"Mayahudi wote wa Turkistan wanadai kwamba Waturuki ni wazao wa Togarmah, mmoja mionganoni mwa wana wa Gomar walijotajwa katika Mwanzo 10:3."

Ukurasa wa 14.

Mayahudi katika Bokhara ni 10,000 kwa idadi. Rabbi Mkuu alinithibitishia mimi kwamba Bokhara ndiyo Habor, na Balkh ndiyo Halah iliyotajwa katika 2 Wafalme 18:11 lakini kwamba wakati wa utawala wa Changis Khan walipoteza taarifa zao zote za kimaandishi. Pale Balkh masheikh wa Kiislamu walinithibitishia kwamba ulijengwa na mwana wa Adam, kwamba jina lake la kwanza lilikuwa Hanakh na baadae Halah, ingawa baadae waandishi waliuita Balakh, au Balkh. Mayahudi, wote wa Balkh na Samarcand wanadai kwamba Turkistan ndiyo nchi ya Nod, na Balkh ndipo mahali ilipokuwa nchi ya Nod wakati fulani."

Ukurasa wa 15.

"Simulizi hii ni ya zamani pale Bukhora, kwamba baadhi ya yale makabila kumi yako nchini Uchina. Niliwatahini Wayahudi hapa kuhusu nukta mbalimbali za tafsiri ya maandiko matakatifu, hususan ile moja ya muhimu katika Isaya 7:14 - bikira. Waliitafsiri kama tufanyavyo sisi Wakristo na hawajui kabisa ubishani muhimu uliopo kati ya Mayahudi na Wakristo kuhusu nukta hii."

Ukurasa wa 16.

"Nilipata hati ya kusafiria kutoka kwa Mfalme baada ya ukaaji huu wa kupendeza sana na kisha nikavuka Oxus na kuwasili baada ya siku chache Balkh na kutoka katika jiji lile ambapo pia nilizungumza na wale Waisreali waliotawanyika, nikaelekea Muaur."

"Baadhi ya Waafghan wanadai uzawa wenye asili ya Israeli. Kulingana na hao, Afghan alikuwa mpwawe Asaph, mwana wa Berachia, ambaye alijenga hekalu la Solomon. Wazao wa huyu Afghan, kwa vile walikuwa Mayahudi, walipelekwa Babylon na Nebuchadnezzar, ambapo kutoka hapo wakaondolewa na kupelekwa kwenye mlima wa Ghoree nchini Afghanistan, lakini katika zama za Muhammad wakasilimu. Wanaonyesha kitabu *Majma-ul-Ansab*, au mkusanyiko wa vizazi, ambacho kimeandikwa kwa lugha ya Kiajemi."

Ukurasa wa 17.

"Kwa hiyo nikapita hadi Peshawar. Hapa pia nikasomewa kitabu cha ajabu cha asili ya Waafghan, kitabu cha Kipushtuu cha Khan Lehaun Loote. Taarifa iliyomo katika kitabu hiki inakubaliana na ile iliyotolewa katika *MSS*, *Teemur Nemeh* na *Ketaub Ansbee Muhakkek Toose*. Nilidhani kwa ujumla sura zao si za Kiyahudi; lakini nilishtushwa kiajabu na kufanana na Mayahudi walikonako Yusufzai na Khalibarii, mawili mionganoni mwa makabila haya. Hawa Kaffreseeah Poosh, kama ni Waafghan, basi wanatofautiana kwa mbali sana na wengine mionganoni mwa taifa lao. Wasafiri wengi wamewadhania kuwa ni wazao wa jeshi la Alexander, lakini hawasemi hivyo."

Ukurasa wa 18.

"Kila mara nilidhani kwamba hawa Kaffr Seeah Poosh ni wazao wa Israeli na baadhi ya Mayahudi wasomi wa Samarcand wana maoni kama mimi."

Ukurasa wa 19 - 20

Kapteni Riley, niliyeshangaa kumwona, aliwaona Waafghan kama ni wazao wa Kiyahudi."

Ukurasa wa 58.

"Nilikaa siku sita na wana wa Rachab (Banii Arbal). Pamoja nao walikuwako wana wa Israeli wa kabilia la Dan, ambao wanakaa karibu na Terim katika Hatramawl, ambao wanatazamia, kwa kushirikiana na wana wa Rachab, kufika haraka kwa Masihi katika mawingu ya Mbinguni." Jalda la 2. ukurasa 131.

"Ni jambo la ajabu sana kwamba Nabii Ezekiel katika sura ya ishirini na saba, aya ya kumi na nne anatoa maelezo halisi ya biashara iliyoendeshwa kati a Waturuki na wakazi wa Bokhara, Khiva na Khokand. Nabii huyo anasema: "Wale walio wa nyumba ya Togarmah (yaani Waturuki) walifanya biashara katika mikusanyiko yao na farasi na wapanda farasi na nyumbu." Waturuki hadi leo, kama walivyo walinzi wa Kiyahudi, ni mamluki na hujikodisha kwa tenga chache kwa siku. Pia ni jambo la ajabu sana kwamba nilisikia mara kwa mara Waturuki wakijiita Toghamah, na Mayahudi huwaita Waturuki Toghamah."

"Kuyaangalia makundi ya ngamia yakija na bidhaa kutoka Kashmir, Kabul, Khokand, Keetay na Orenbough kunamkumbusha mtu lile fungu la maneno la Isaya 60:6 "Wingi wa ngamia utakufunika, ngamia vijana wa Midiani na Ephah, wote watakuja kutoka Sheba na wataleta dhahabu na uvumba." kwa kutaja dhahabu, nisije nikasahau kwamba karibu na Samarcand kuna machimbo ya dhahabu na feruзи."

Ukurasa wa 236.

"Maneno machache kuhusu wale watoto katika milima ya Kurdistan. Watoto hawa kama alivyosema vizuri sana marehemu muombolezwu Dakta Grant , wana asili ya Kiyahudi ingawa siwezi kwenda hadi kufikia mahali pa kuthibitisha kwamba wanatokana na yale makabila kumi, kwa vile wao wenyewe hawaijui nasaba yao. Hivi sasa wengi wao ni Wakristo."

"Kwa kiasi kikubwa wanafanana na Waprotestanti wa Ujerumani na Uingereza kwani hawana masanamu wala majumba ya watawa na mapadre wao huoa. Lakini heshima yao ya Kiaskofu ni ya urithi na pia ile ya askofu mkuu, na wakati mama wa askofu mkuu anapokuwa mja

mzito anaacha kunywa mvinyo na kula nyama; na endapo mtoto wa kiume anazaliwa, anakuwa Askofu Mkuu, na kama ni mtoto wa kike, analazimika kubakia bikira hadi milele."

KIAMBATANISHO Na. 13

The Lost Tribes; Kilichotungwa na Geroge Moore M. D.

Kwenye ukurasa wa 143.

"Tumevutwa mara moja kwenye nchi ya umuhimu mkubwa sana katika hali ya hivi sasa ya Mashariki, na la kufurahisha zaidi kwetu, kwa vile tunawakuta pale watu wanaoungama kuwa ndio Banii Israeil au wazao wa yale Makabila Kumi, yaani Afghanistan na nchi za jirani yake."

Kwenye ukurasa wa 145.

"Sababu zilizo bayana kwa kufikiria kwamba tabaka fulani za watu wa Bokhara na Afghanistan ni za asili ya Kiisraeli ni hizi: Kwanza: Kufanana kwao binafsi na familia ya Kiebrania. Hivyo, Dakta Wolff aliye m-misionari wa Kiyahudi anasema "Nilishitushwa kiajabu na kufanana kwa wale Yusufuzai (kabila la Yusuf) na wale Khybere, mawili mionganini mwa kabila yao, na Mayahudi." Moorcroft pia anasema kuhusu Wakhyberi, "Ni warefu, na wa maumbile yenye taswira za Kiyahudi kabisa." Pili: Wamejiita wao wenyewe Banii Israeil, wana wa Israeli tangu wakati usioweza kukumbukwa. Tatu: Majina ya makabila yao ni ya Kiisraeli, hususan lile la Yusufu, ambalo linajumuisha Ephraim na Manasseh. Katika kitabu cha ufunuo kabila la Yusuf linachukua mahali pa Ephraim (Ufunuo 7:6-8). Katika Hesabu 36:5 Musa anazungumzia kuhusu Manasseh kama "kabila la wana wa Yusufu", hivi kwamba ni dhahiri kwamba yote mawili, Manasseh na Ephraim yalikuwa yakijulikana kwa jina la kabila la Yusufu. Nne: Majina ya Kiebrania ya mahali na watu nchini Afghanistan yanajitokeza mara nyingi zaidi kuliko inavyoweza kuelezwu kuwa yametokana na uhusiano wa Kiislamu na nchi hiyo; na kwa hakika majina haya yalikuwapo kabla Waafghan hawajawa Waislamu.

Tano: Taarifa zote zinakubaliana kwamba waliikalia milima ya Ghor tangu zamani za kale za mbali sana. Ni jambo la uhakika kwamba Binti mfalme wa Ghor alitokana na kabilia la Waafghan la Sooree na kwamba ukoo wao wa kifalme uliruhusiwa kuhesabiwa kuwa ni wa kale ya zamani sana hata wakati wa karne ya kumi na moja. "Wanaelekea kuwa waliimiliki milima ya Soliman au Solomon tangu zamani ambayo inajumuisha yote mionganoni mwa milima ya Kusini mwa Afghanistan." (Elphinstone). Sita: Afghan ni jina lilopewa taifa lao na watu wengine. Jina walilolipa taifa lao ni Pushtoon, na Dakta Garey na Marshaman wanadai kwamba lugha ya Kipushtoon ina mizizi mingi ya Kiebrania kuliko nyingine yo yote."

Ukurasa wa 147;

"Kisha ukale wa jina la nchi ya Cabul au Cabool unabainishwa; na pia inaonyesha kwamba watu fulani wa pekee wajulikanao kama 'Makabila', 'Makabila Matukufu' waliishi pale wakati wa zamani sana. Kwa hiyo, kuna ushahidi mzuri kwamba wakazi wa sasa wa Cabul wanaweza kuwa na haki ya kudai kwamba tangu wakati wa mwanzo kabisa wa historia, wao na mababu zao wamekuwa wakiikalia Cabul na kwamba tangu wakati usioweza kukumbukwa wamekuwa wakijulikana kama 'Makabila'. Yaani, Makabila ya Kiisraeli kama wajichukuliavyo hivi sasa . . . Kulingana na Sir W. Jones watawala wa Uajemi - Magharibi wanakubaliana nao katika maelezo yao yahusuyo asili yao; na mamlaka kaaji na mashuhuri kama vile Sir John Malcom na yule m-mshionari Bwana Chamberlain wanatuhakikishia baada ya uchunguzi mkamilifu kwamba wengi mionganoni mwa Waafghan bila shaka wanatokana na mbegu ya Ibrahimu."

KIAMBATANISHO Na. 14

Mtunzi : Josephus Flavius

Kitabu : *Antiquities.*

Kimetafsiriwa na: Jewish W. M. Whitson

Kimetangazwa na: Hurst, Rees, Orme & Brown: London.

"Nini: Je mnayafikiria matumaini yenu ng'ambo ya mto Euphrates? Je mmoja wenu ye yote anafikiri kwamba makabila yaliyo ndugu zenu yatakuja kuwasaidieni na kuwatoeni nje ya Adiabene? Isitoshe, kama yakifanya hivyo Waparthian hawatayaruhusu." (XI, V.2).

Hii ni nukuu kutoka kwa Mfalme wa Kirumi (Agrippa) akiwaambia Mayahudi kujisalimisha kwa Warumi na siyo kuwategemea Mayahudi kutoka nga'mbo ya mto Euphrates.

Josephus alikuwa katika utawala wa Vespasian, katika sehemu ya mwisho ya karne ya kwanza ya Kikristo.

KIAMBATANISHO Na. 15

A personal narrative of a visit to Chuzin, Cabul, in Afghanistan.

Kimetungwa na: G. T. Vigne Esq., F.R.G.S. London:
Whittaker & Co. Ave maria Lane, E.C. 1840.

Ukurasa wa 166 -167.

"Moolah Khuda Dad, mtu aliye msomi katika historia ya watu wa nchi yake alinisomea kutoka katika Majma-ul-Ansab (Makusanyo ya Vizazi) taarifa fupi ifuatayo ya asili yao. Wanasema kwamba mwana mkuu wa wana wa Yakubu alikuwa Yudha ambaye mwanawe mkuu alikuwa Osruk ambaye alikuwa baba wa Okour, baba wa Moslib, baba wa Farlai, baba wa Kys, baba wa Talut, baba wa Ermiah, baba wa Afghans, lilikotoka jina la Waafghan. Alikuwa wa rika moja na Nebuchadnezzar, alijiita Banii Israeil na alikuwa na wana arobaini amba majina yao hakuna nafasi ya kuyaweka. Mzao wake wa thelathini na nne katika mstari ulionyooka, baada ya kipindi cha miaka elfu mbili alikuwa Kys. Tangu Kys ambaye aliishi wakati wa Mtume Muhammad pamekuwapo na vizazi sitini. Salum, mwana mkuu wa Afghans ambaye aliishi mahali paitwapo Sam (Demeshki) aliondoka mahali hapo na kuja Ghura Mishkon nchi iliyopo karibu na Herat, na wazao wake wakajisambaza polepole katika nchi ambayo hivi sasa inaitwa Afghanistan."

KIAMBATANISHO Na. 16

Ukurasa wa 121

Encyclopaedia of Geography Kilichotungwa na James Bryce, M.A. LL.D; F.R.S.E. na Keith Johnson F.R.G.S.

Chapa ya 2

Kimetangazwa na: William Collins, Sons & Co. Ltd;
London & Glasgow.

Mwaka 1880

Chini ya kichwa cha habari Afghanistan - ukurasa wa 25.

"Historia na Mahusianao " . . ." Jina Afghan halitumiwi na watu wenyewe; wao wanajiita Pooshtoon na uwingi wake ni Pooshtauneh ambalo kutokana na hilo pengine ndipo likapatikana jina Puten wanaloitwa nchini India. Wanafuatiliza asili yao kutoka kwa Saul, Mfalme wa Kiisraeli na kujiita Israili. Kulingana na Sir A. Burnes, mapokeo yao ni kwamba walihamishwa kutoka katika nchi Takatifu na Mfalme wa Babylonia na kuja kupandikizwa katika nchi ya Ghore iliyio Kaskazini Magharibi mwa Cabul, na waliishi kama Mayahudi hadi mwaka 682 A.D. walipoingizwa katika Uislamu na Chifu wa Kiarabu Khalid ibn Abdallah aliyemwoa binti wa Chifu wa Kiafghan. Hakuna ushahidi wa kihistoria uliowahi kutolewa katika kuunga mkono asili hii, na pengine ni ubunifu tu uliotokana na mambo ya hakika yaliyotajwa katika 2 Wafalme 18:11. Lakini yawezekana, wasafiri wote wanakubaliana kwamba watu hawa wanatofautiana kiajabu na mataifa jirani, na wao kwa wao wanayo asili moja inayowaunganisha wote. Wanasemekana na baadhi ya watu kufanana sana na Mayahudi katika taswira na maumbile na wamegawanyika katika makabila kadhaa, yakikalia maeneo tofauti na yakibakia takriban bila kuchanganyika."

KIAMBATANISHO Na. 17

History of Afghanistan. Kilichotungwa na Colonel G. Malleson, C.S.I., W.H. Allen & Co., 13, Waterloo Place, Pall Mall, SW 1. Kimetangazwa kwenye Ofisi ya India, 1878.

Ukurasa wa 39. "Sasa nawageukia watu wa Afghanistan. Nayageukia makabila yanayoikalia nchi ile na ambayo yanazimiliki njia za milimani. Mada hii imeshughulikiwa kwa kirefu na Mountstuart Elphinstone, imeshughulikiwa na Ferrier - ambao wanamnukuu kwa wingi sana Abdullah Khan wa Herat, imeshughulikiwa na Bellews na wengine wengi.

Kufuatia Abdullah Khan na waandishi wengine wa Kiafghan, Ferrier anashawishika kuamini kwamba Waafghan wanayawakilisha yale makabila kumi yaliyopotea, na kuwadaia uzawa wa moja kwa moja kutoka kwa Saul, Mfalme wa Israel. Miiongoni mwa waandishi wengine wanaoafiki maoni haya linaweza kutajwa jina tukufu la Sir William Jones. Kwa upande mwingine, Profesa Dorn wa Kharkov ambaye amelichunguza suala hili kwa kirefu anaikataa nadharia hii. Mountstuart Elphinstone anaiweka katika kundi moja na ile nadharia ya uzawa wa Warumi kutoka kwa Wetrojan. Pingamizi dhidi ya maoni ya Abdullah Khan zimetolewa hivi punde kwa hamaki na kwa nguvu na Profesa Dowson katika barua aliyoliandikia gazeti la 'Times'. "Iwapo", anaandika muungwana huyo, "lilikuwa na thamani ya kuweza kufikiriwa, bado haliendani na ile fikra kwamba Waafghan ni wazao wa yale makabila kumi yaliyopotea. Saul alikuwa ni mtu wa kabilia la Benjamin na kabilia hilo halikuwa mojawapo miiongoni mwa yale kumi yaliyopotea. Linasalia suala la maumbile. Hili hapana shaka lina umuhimu wake, lakini haliwezi kulipiku lile suala la muhimu zaidi la lugha. Kisha Profesa Dowson anaendelea kuonyesha kwamba lugha ya Kiafghan haina alama za Kiebrania ndani yake, na akamalizia kwa kuitangaza ile dhana kwamba taifa lote la Kiafghan laweza kuwa limebadilisha lugha yao kadiri wakati ulivyopita kuwa ni "jambo lisilosadikika kupita kiasi."

KIAMBATANISHO Na. 18

Ukurasa wa 122

L.P. Ferrier

History of the Afghans. 1858

Kimetafisiriwa na W. M. Jesse.

Kimetangazwa na: John Murray, London

Ukurasa wa 4. "Wakati Nadir Shah alipowasili Peshawar, alipokuwa akienda kuiteka India, Chifu wa kabila la Yusufu Zai alimzawadia Biblia iliyoandikwa kwa lugha ya Kiebrania na vitu vingine kadhaa ambavyo vilikuwa vikitumika katika ibada yao ya kale na ambavyo walivihifadhi. Vitu hivi vilitambuliwa mara moja na Mayahudi walioufuata msafara huo wa Kijeshi."

Kwenye ukurasa wa 1 katika maelezo chini ya ukurasa anaandika:

"Mtunzi wa muswada wa historia ya Waafghan anasema kwamba baadhi hulipata jina Afghan kutoka katika maana yake ya Kiajemi 'maombolezo' kwa sababu makabilaya yaliomboleza kuhamishwa kwao mbali na Judea. Wengine wanasema kwamba Afghan alikuwa mjukuu wa Saul na aliajiriwa na Solomon katika kulijenga Hekalu. Mtunzi huyu anazirejea historia mbili za taifa hili:

Tarikh - Afghanah, na Tarikh - Ghor, yaani Historia ya Waafghan na Historia ya Ghor. Yaelekeea, anasema, kutokana na vitabu hivi viwili, kwamba Waafghan wanajihesabu kuwa kwa kiasi fulani wametokana na Wakristo walio wenyeji wa asili wa Misri, na kwa kiasi fulani wametokana na Waisraeli, lakini hakuna ushahidi wo wote unaotolewa katika kuunga mkono dai hili.

Tunaambiwa na mmoja wa waandishi hawa kwamba baada ya kuwaua wafungwa wengi, Nebuchadnezzar aliwahamishia kwenye

milima ya Ghor wale waliosalia, ambako walizaliana kwa wingi sana na Mayahudi kutoka Arabia; na wakati wale walipobadilisha dini yao na kujiunga na ile ya Muhammad, barua ilipokelewa kutoka kwa Myahudi aliyesilimishwa aitwaye Khalid, ikiwajulisha kuhusu kutokea kwa Mtume Mpya na kuwasihhi wajunge na bendera yake takatifu. Waafghan wachache walio watukufu walikwenda Arabia; mkuu wao alikuwa Kais ambaye tunajulishwa na watunzi wa Kiafghan alifuatiliza uzawa wake kupitia vizazi arobaini na saba hadi kumfikia Saul na kupitia hamsini na tano hadi kumfikia Ibrahimu". (History of the Afghans, Persian MSS).

"Takriban waandishi wote wa Kiislamu wanawadaia Waafghan uzawa huu na kwa wakati fulani nilikuwa na jedwali la nasaba ambamo jaribio lilifanywa la kuthibitisha kuwa familia zote kuu za Afghanistan ni wazao waliotokana moja kwa moja na wafalme wa Israeli."

Iwapo unapenda kununua vitabu zaidi vya Dini ya Kiislamu au kwa maelezo zaidi ya mafundisho ya Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya, wasiliana na anuani iliyo karibu nawe katika hizi zifuatazo:

1. P. O. Box 376, Simu: 2110473 Dar es Salaam.
2. P. O. Box 1, Simu: 2603477 Morogoro.
3. P. O. Box 260, Simu: 2646849 Tanga.
4. P. O. Box 359 Iringa. (Simu 2700633).
5. P. O. Box 196, Simu: 243043 Dodoma.
6. P. O. Box 94, Simu: 2600847 Songea.
7. P. O. Box 10723 Arusha.
8. P. O. Box 54, Simu: 2603291 Tabora.
9. P. O. Box 547 Ujiji - Kigoma.
10. P. O. Box 306, Simu: 2333919 Mtwara.
11. P. O. Box 86, Simu: 2510082 - Masasi.
12. P. O. Box 1812 Bukoba.
13. P. O. Box 28, Simu 97 Kibiti - Rufiji.
14. P. O. Box 391 Tarime.
15. P. O. Box 605 Ifakara.
16. P. O. Box 17 Kilosa.
17. P. O. Box 40554, Simu: 764226 Nairobi Kenya.
18. P. O. Box 97011, Simu: 492624 Mombasa Kenya.
19. P. O. Box 421, Simu 40269 Kisumu Kenya.
20. P. O. Box 77, Simu 52 Shianda Kenya.
21. P. O. Box 552 Limbe Malawi.

Jesus' escape from death on the cross and journey to India

JESUS IN INDIA

This is an English version of an Urdu treatise written by the Holy Founder of the Ahmadiyya Movement in Islam, Hazrat Mirza Ghulam Ahmad (1835 - 1908). The theme is the escape of Jesus from death on the cross, and his journey to India in search of the lost tribes of Israel. Christian as well as Muslim scriptures, and old medical and historical books including ancient Buddhist records, provide evidence about this journey. Jesus is shown to have reached Afghanistan, and to have met the Jews who had settled there after deliverance from the bondage of Nebuchadnezzar. From Afghanistan Jesus went on to Kashmir, where other Israelite tribes had settled. There he made his home, and there in time he died; his tomb has been found in Srinagar.